

**TAFSIRI KAMA UANDISHI UPYA: TATHMINI YA BIBLIA TAKATIFU YA
KISWAHILI NA ‘BUKUIT NE TILIL’ YA KIKALENJIN**

NA

SINGOEI JANE JEPKOECH

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMIFU YA KISWAHILI KATIKA IDARA YA
KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

CHUO KIKUU CHA MOI

2021

IKIRARI**Ikirari ya Mtahiniwa**

Kazi hii ni yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa hapo awali katika chuo kingine chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote. Hairuhusiwi kuiga, kunakili au kurudufisha sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ridhaa yangu au ya Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Jane Jepkoech Singoei**SASS/DPHIL/KIS/02/12****Ikirari ya Wasimamizi**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama washauri walioteuliwa na Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Dkt. Mosol Kandagor

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Dkt. Mwanakombo Noordin

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wanangu Tim, Faith, Mike na Mark. Mkatafute maarifa na zaidi ya yote, hekima.

SHUKURANI

Shukurani zangu za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu aliyezifanya mbingu na nchi na kuamuru niwepo kwa majira kama haya kwa makusudi yake mwenyewe. Amenipa nguvu na hekima ya kuanza na kuitamatisha kazi hii. Amenipa afya na ulinzi mkuu hadi kufika nilipo sasa. Daima nakushukuru Ebeneza.

Pili, ningependa kushukuru Chuo Kikuu cha Moi, hasa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunisajili na kunipa fursa ya kujiinua kimasomo. Nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Mosol Kandagor na Dkt. Mwanakombo Noordin ambao daima walinielekeza kwa kunipa mawaidha si haba kuhusiana na kazi hii, juhudi zao za kunichochea ndizo zilizonipa msukumo hadi kukamilisha kazi hii.

Isitoshe, sitawasahau wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi kwa kuchangia mawaidha kem kem ya kiakademia na hivyo kuniwezesha kuzalisha mada hii. Vilevile, shukurani zangu ni kwa wazamifu wenzangu Dkt. Hilda Pembe, Noah Keitany na Reuben Kisiroche. Tulifaana sana wakati dhoruba ilizidi kuwa kali.

Ninatoa shukurani zangu pia kwa familia yangu. Mume wangu Philip Biamah; asante kwa kunichochea na kunishika mkono wakati nilihisi kukata tamaa. Ulimitia moyo na kunipa motisha kila nilipohisi kuchoka. Kwa wanangu Tim, Faith, Mike na Mark, asanteni kwa kunistahimili wakati sikuwapa muda uliofaa kama mama mzazi.

IKISIRI

Mawasiliano hufanyika iwapo pana maelewano kati ya watumiaji lugha husika. Ikiwepo changamoto ya kuelewana kilugha, basi kutakuwa na haja ya kuitafsiri matini hiyo ili msomaji aweze kupata ujumbe wa mwandishi. Ili kufikia hadhira pana, Biblia imefanyiwa tafsiri kwa lugha nyingi, ikiwemo Kikalenjin. Wakati wa kutafsiri, mtafsiri huiandika kazi tafsiri kwa namna tofauti na ilivyo matini asilia. Hii inatokana na hali kwamba, kila lugha ina upekee wa kisarufi na utamaduni. Isitoshe, hadhira inayopokea matini tafsiri ni tofauti na ile iliyoandikiwa matini asilia. Hali hizi husababisha mtafsiri kuiandika upya kazi tafsiri, ili kuafikiana na wasomaji wa matini pokezi. Utafiti huu, ulilenga kuchunguza tafsiri kama uandishi upya. Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua hali ya uandishi upya katika matini tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin, yaani, *Bukuit Ne Tili*. Lengo la kwanza likiwa kubaini jinsi tofauti za kitamaduni baina ya wazungumza lugha ya Kikalenjin na Kiswahili zilivyosababisha uandishi upya wa *Bukuit Ne Tili*. Pili, kuchunguza mikakati iliyotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tili* na hivyo kupelekea uandishi upya. Tatu, ni kubaini mbinu zilizotumika kutafsiri *Bukuit Ne Tili* na kupelekea uandishi upya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili, ambazo ni nadharia ya Tafsiri Vitendo ambayo ilitumika kubaini jinsi tofauti za kimazingira kati ya hadhira ya matini asilia na ya matini pokezi ilivyopelekea uandishi upya kufanyika wakati wa kutafsiri. Nadharia ya pili ni ya Ulinganifu, ambapo matini asilia ililinganishwa na matini pokezi ili kubaini kama ujumbe ulihifadhiwa katika matini tafsiri. Aidha, tamaduni, matumizi ya msamiati na sarufi zililinganishwa kwa kuchunguza mikakati na mbinu zilizotumika kutafsiri matini asilia, na hivyo kubaini uandishi upya katika matini pokezi. Data zilikusanywa kupitia uchunguzi maktabani na vilevile kuwasaili washikadau katika Ofisi ya Utafsiri wa Biblia ya Kapsabet na Shirika la Kutafsiri Biblia nchini. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa ili kupata data iliyotumika katika uchanganuzi. Kitabu cha Mithali katika Agano la Kale kiliteuliwa kwa minajili ya utafiti huu. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kimaelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa: utamaduni wa Waswahili na wa Wakalenjin ni tofauti na hii ilipelekea uandishi upya ufanywe katika tafsiri. Pili, matumizi ya mikakati ya kutafsiri ilichangia uandishi upya wa kazi tafsiri: mwisho ni, mbinu alizozitumia mtafsiri zilipelekea kazi tafsiri kuwa uandishi upya. Matokeo haya yalibainisha wazi kuwa japo Biblia ni matini takatifu inayostahili isibadilishwe, lakini tafsiri inasababisha matini hii iandikwe upya ili kukidhi mahitaji ya hadhira pokezi. Aidha, matokeo haya yalitoa picha halisi kuhusu tafsiri kwamba hata kama matini ni ya kidini, haiwezi kukwepa kuandikwa upya inapotafsiriwa. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutoa mchango kwa wataalamu wa kutafsiri kuhusiana na namna ya kutekeleza tafsiri. Matokeo ya uchunguzi huu yatawapa watafiti mwelekeo kuhusu namna ya kubaini ubora wa kazi tafsiri. Aidha, wanaotafsiri Biblia kwa lugha za kienyeji watanufaika na matokeo ya uchunguzi huu. Vilevile, mashirika ya kutafsiri yatanufaika na matokeo haya. Watafsiri wa matini za kidini na zisizo za kidini wanatarajiwa kunufaika na utafiti huu. Utafiti unapendekeza yafuatayo: Sera za elimu kuhusu lugha za kienyeji zinafaa kutilia maanani tafsiri ya matini za kufundishia. Mashirika ya kufanya tafsiri yaimarishwe kwa kupewa udhamini ili kutafsiri makala nyingi zaidi. Somo la tafsiri lizidi kuimarishwa katika vyuo vikuu.

ABSTRACT

Communication between parties is said to be complete when the message is understood. In case of miscommunication brought about by language barrier, then, there is need to translate the text for the reader to get the message. The Bible has been translated into various languages in order to reach a wider audience, this includes the Kalenjin community. When translating, the translator rewrites differently from the original writer. This is because every language has particular grammar and traditions. Moreover, the target readers are different from the original readers. All these result to the text being rewritten during translation, so as to address the needs of the target readers. The objectives of the study was to analyze the state of rewriting in the translated text of the Kalenjin Bible (*Bukuit Ne Tilil*) from the Kiswahili Bible (Bibilia Takatifu). The research also sought to find out the effects of cultural difference on translation, hence rewriting when translating. This research sought to analyse the approaches that were used in translating *Bukuit Ne Tilil*. At the same time, finding out the methods that were adopted in this translation, resulting in regarding the Bible as rewritten text. The research used two theories; the first is the Translation Acts Theory that was used to analyse the environmental difference between the writer of the original text and the translator, causing the translation to be rewriting. The second is the Equivalence Theory, which was used in comparing the messages of the original and the translated text. The traditions of the two communities, their grammar and various terms were compared using this theory. The research methods that were employed included the use of secondary data from the library, where the researcher went through previous researches on the topic and in analyzing texts that were basically used for the research, i.e. the Kiswahili and Kalenjin Bibles. Field research was also engaged, where the researcher approached some translators who are involved in translation of Bible at the Kapsabet Bible Translation office and the Bible Translation and Literary office. Some Kalenjin speakers were of help in getting some of the data. From the purposeful sampled data, descriptive analysis was done, based on the objectives of the study. The book of Proverbs in the Old Testament was analysed and the outcome was that the cultural difference between the Waswahili and the Kalenjin people made translation to be rewritten. Also, the approaches used in translation together with the methods used, amounted to making translation a process of rewriting the text, which makes it possible for the target reader to understand it. The outcome of this research will be beneficial to translators in carry out translation activities. More so, the Bible translators will benefit from the outcome of this research, as well as the translation firms. Translators of both religious and non-religious texts will find this work useful to them. Moreover, various translators and researchers on translation will have this findings and the recommendation of this research to be of great importance to them. This research has recommended that: the education policies on vernacular should be supported by translating teaching materials in various vernaculars. Translating firms should be sponsored in order to translate as many texts as possible. Translation studies should be emphasized in the universities.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	iii
SHUKURANI.....	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA JEDWALI	xi
ORODHA YA PICHA.....	xii
UFAFANUZI WA ISTILAHI MAALUM	xiii
TAFSIRI YA MANENO	xiv
MAELEZO YA VIFUPISHO	xv
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.1.1 Tafsiri na mawasiliano	3
1.1.2 Historia fupi ya tafsiri	4
1.1.2.1 Kipindi cha kale.....	6
1.1.2.2 Kipindi cha kati	7
1.1.2.3 Kipindi cha mfufumko na usasa wa kale.....	7
1.1.2.4 Kipindi cha sasa.....	8
1.1.3 Kazi ya kutafsiri Biblia nchini Kenya.....	8
1.1.4 Biblia katika lugha ya Kikalenjin	9
1.1.5 Tafsiri na teknolojia	10
1.1.6 Uandishi upya katika tafsiri ya Biblia.....	10
1.2 Suala la Utafiti	13
1.3 Malengo ya Utafiti	14
1.4 Nadharia Tete za Utafiti.....	15
1.5 Sababu za Kuchagua Mada	15
1.6 Umuhimu wa Utafiti	16
1.7 Upeo wa Utafiti.....	17
1.8 Hitimisho.....	19

SURA YA PILI.....	20
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA	20
2.0 Utangulizi.....	20
2.1 Dhana ya Tafsiri.....	20
2.2 Tafsiri kama Uandishi Upya	22
2.3 Tafsiri na Utamaduni	32
2.4 Mikakati ya Kutafsiri	41
2.4.1 Utohozi wa kimuktadha	44
2.4.2 Ukopajiwa msamiati	44
2.4.3 Uradidi wa maneno	45
2.4.4 Ufidiaji wa maneno.....	45
2.4.5 Udondoshwaji wa maneno.....	45
2.4.6 Ufafanuzi wa istilahi	46
2.4.7 Ulinganisho wa kimaana.....	46
2.4.8 Upanuzi wa ujumbe wa L.A	46
2.4.9 Ujumuishaji wa dhana katika L.P	46
2.4.10 Tafsiri ya moja kwa moja	47
2.4.11 Urekebishaji wa maelezo	47
2.4.12 Ubainishaji wa hali maalum.....	47
2.4.13 Matumizi ya vibadala.....	48
2.4.14 Uhamishaji wa maana	48
2.3.15 Ubainishaji wa sajili.....	48
2.5 Mbinu za Kutafsiri	49
2.6 Misingi ya Nadharia.....	54
2.7 Hitimisho.....	63
SURA YA TATU.....	64
MBINU ZA UTAFITI NA UCHANGANUZI WA DATA	64
3.0 Utangulizi.....	64
3.1 Mpango wa Utafiti	64
3.2 Uteuzi wa Sampuli	66
3.3 Utafiti Mwigo.....	67
3.4 Ukusanyaji wa Data	69
3.4.1 Uchunguzi maktabani	69
3.4.2 Uchunguzi shirikishi	70

3.4.3 Usaili	70
3.5 Vifaa vya Kukusanya Data	71
3.5.1 Mwongozo wa usaili	71
3.5.2 Kinasa sauti	72
3.6 Unukuzi wa Data.....	73
3.7 Uchanganuzi wa Data	73
3.8 Hitimisho.....	74
SURA YA NNE	75
VIPENGELE MUHIMU KATIKA KUTAFSIRI DHANA ZA KITAMADUNI 75	
4.0 Utangulizi.....	75
4.1 Utamaduni wa Wakalenjin.....	75
4.1.1 Tafsiri inayohusu vyakula.....	76
4.1.2 Tafsiri ya dhana zinazohusu jinsia	79
4.1.3 Taasubi ya kiume katika tafsiri	83
4.1.4 Tafsiri Inayohusu hali za kimazingira.....	87
4.1.5 Tafsiri ya mila na desturi	88
4.2 Hitimisho.....	91
SURA YA TANO	93
MIKAKATI ILIYOTUMIKA KATIKA KUTAFSIRI <i>BUKUIT NE TILIL</i>.....	93
5.0 Utangulizi.....	93
5.1 Utohozi wa Maneno ya L.A katika L.P	93
5.2 Upanuzi wa Maana ya Maneno.....	95
5.3 Udondoshaji wa Sehemu za M.A katika Tafsiri	97
5.4 Ufafanuzi wa Ujumbe wa M.A katika Tafsiri	102
5.5 Urekebishaji wa Maelezo katika Tafsiri	107
5.6 Ujumlishwaji wa Msamiati Husika katika Tafsiri	111
5.7 Hitimisho.....	112
SURA YA SITA.....	114
MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA KUTAFSIRI <i>BUKUIT NE TILIL</i>	
KUTOKA KWA BIBILIA TAKATIFU YA KISWAHILI.....	114
6.0 Utangulizi.....	114
6.1 Mbinu Zilizotumika Kutafsiri <i>Bukuit Ne Tilil</i>	114
6.1.1 Tafsiri ya Neno kwa Neno	115
6.1.2 Tafsiri ya Kisemantiki.....	121

6.1.3 Tafsiri ya kimawasiliano /huru/sabilia.....	126
6.2 Hitimisho.....	131
SURA YA SABA	132
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	132
7.0 Utangulizi.....	132
7.1 Muhtasari wa Tasnifu	133
7.2 Matokeo ya Utafiti	133
7.2.1 <i>Bukuit Ne Tilil</i> kama uandishi upya wa Biblia Takatifu kutokana na tofauti za kitamaduni.....	134
7.2.2 Mikakati ya kutafsiri na uandishi upya wa <i>Bukuit Ne Tilil</i>	138
7.2.3 Mbinu za kutafsiri na uandishi upya wa <i>Bukuit Ne Tilil</i>	141
7.3 Mchango wa Utafiti	143
7.4 Mapendekezo ya Utafiti.....	145
7.5 Mapendekezo kuhusu Tafsiri za Baadaye	147
MAREJELEO	148
MATINI TEULE	153
VIAMBATISHO.....	154
Kiambatisho I: Data Iliyochanganuliwa Kutoka Kitabu Cha Mithali	154
Kiambatisho II: Barua Kutoka Kwa Ofisi Ya Utafsiri Wa Biblia Ya Kapsabet.....	166
Kiambatisho III: Maswali ya Usaili	167

ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 1: Jedwali linaloonyesha maneno yaliyotafsiriwa kwa kutoholewa.....	94
---	----

ORODHA YA PICHA

Picha 1: Mchakato wa tafsiri.....57

UFAFANUZI WA ISTILAHU MAALUM

Agano la Kale	Sehemu ya Biblia, aghalabu vitabu vya kwanza ishirini na saba, vilivyoandikwa na manabii mbalimbali kabla ya kuzaliwa kwa Masiha, Yesu Kristo.
Hadhira Pokezi	Wasomaji wa matini tafsiri (Wakalenjin)
Lugha asilia	Lugha iliyotumiwa katika matini asilia (Kiswahili)
Lugha Pokezi	Lugha iliyotumika katika matini pokezi (Kikalenjin)
Matini Asilia	Matini ambayo imetumika kutafsiri kwenda kwa lugha nyingine.(Biblia ya Kiswahili, katika utafiti huu)
Matini Pokezi	Matini iliyotafsiriwa kutoka kwa lugha nyingine. (Biblia ya Kiswahili katika utafiti huu)
Uandishi Upya	Kutafsiri M.A kwa namna inayoegemea tamaduni, muktadha, sarufin.k za L.P kwa minajili ya kuiwezesha hadhira pokezi kuelewa matini hiyo kama matini asili.

TAFSIRI YA MANENO

Cross Fertilization Theory - Nadharia ya Mtambiko Mawazo

Translational Action Theory - Nadharia ya Tafsiri Vitendo

MAELEZO YA VIFUPISHO

B.Y.M	- Baada Ya Masiha
FY	- Fasiri Yangu
H.A	- Hadhira Asilia (Waswahili)
H.P/ H.L	- Hadhira Pokezi / Hadhira Lengwa (Wakalenjin)
K.Y.M	- Kabla Ya Masiha
k.v	- Kama Vile
L.A	- Lugha Asilia (Kiswahili)
L.P	- Lugha Pokezi (Kikalenjin)
M.A	- Matini Asilia (Biblia Takatifu)
M.L.A	- Matini ya Lugha Asilia
M.L.P	- Matini ya Lugha Pokezi
M.P	- Matini Pokezi (<i>Bukuit Ne Tilit</i>)
M.T	- Matini Tafsiri
n.k	- na kadhalika
R.o.K	- Republic of Kenya

TEKNOHAMA- Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia mambo ya kimsingi katika utafiti huu: Usuli wa suala la utafiti umeangaziwa huku wataalamu mbalimbali wakirejelewa pamoja na matokeo ya tafiti zao kuzungumziwa. Suala la utafiti limeangaziwa, vilevile, malengo ya mtafiti katika kutekeleza utafiti wake. Nadharia tete zimetajwa pamoja na sababu zilizompelekea mtafiti kukita utafiti wake kwenye suala hili. Isitoshe, sura hii imeweka wazi umuhimu wa utafiti huu kutekelezwa na mwishowe, mtafiti ameonyesha upeo wa utafiti huu.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano miongoni mwa wanadamu Odeo na Maina (2008). Kulingana na Ogechi (2002), lugha ni dhana inayotumiwa kurejelea uwezo wa kimaumbile wa akili ya mtu ambao humwezesha kuwasiliana kilugha. Kwa upande mwingine, Shitemi (2001), anasema kwamba lugha ni kifaa muhimu kinachotumiwa na mwanadamu katika mawasiliano. Anataja lugha kama gari la mawasiliano. Hii ina maana kuwa, ufanisi wa mawasiliano baina ya binadamu hutegemea lugha tumizi. Wanadamu wanapowasiliana, ndipo wanapojenga uhusiano wao kama anavyodai Buliba (2001:54):

Lugha husaidia sana kuudhibiti uhusiano wa kijamii.....lugha ndiyo huwaleta watu hao pamoja kwa kujenga uhusiano wa kibinafsi katika kiwango cha mtu kwa mtu, mtu kwa jamaa yake, mtu na jamii yake, mtu na taifa lake na mtu na ulimwengu wake.

Ili uhusiano kama huu ujengwe, ina maana kuwa lugha hii lazima iwe inaeleweka kati ya mtuma-ujumbe na mpokea-ujumbe. Hapo ndipo tunaweza kusema kuwa mawasiliano yamekamilika kwa kuwa pametokea maelewano.

Mawasiliano kwa upande mwingine ni matokeo ya uwezo wa lugha. Ogechi (2002) anafafanua mawasiliano kama usafirishaji wa ujumbe kutoka kwa mtuma-ujumbe hadi kwa mpokea-ujumbe kwa kutumia nyenzo kama vile lugha. Ili kukamilisha mawasiliano, lazima nyenzo husika iwe inafahamika kwa mtuma na mpokea ujumbe. Hii ina maana kuwa ikiwa lugha itatumika kama njia ya kuwasiliana, basi wazungumzaji sharti wawe wana uwezo wa kuwasiliana katika lugha husika.

Mawasiliano baina ya wanadamu hutekelezwa kupitia kwa lugha andishi, zungumzi na ishara. Mawasiliano haya wakati mwingine huweza kutatizwa ikiwa wanaohusika kwenye mawasiliano hayo si wanaumoja lugha. Nchini Kenya kwa mfano, kuna idadi ya takriban lugha arobaini na mbili; hali inayopelekea mawasiliano kuwa na changamoto katika ufanisi wake. Hii ina maana kuwa ili kufikia wananchi wote, ni lazima lugha inayoeleweka kwa watu wote itumike. Hali hii basi, ndiyo iliyopelekea Kiswahili kiteuliwe kuwa lugha ya taifa, na kuimarishwa kuwa lugha rasmi kwa mujibu wa katiba mpya ya Kenya (R.o.K, 2010). Hatua hii imeimarisha kiwango cha mawasiliano humu nchini kwa kuwa wananchi wanafikiwa kwa lugha wanayoimudu.

Panapokuwa na jukumu la kimawasiliano linalotokana na kutoelewana kilugha, na ikatokea kuwa wahusika katika mawasiliano hayo hawana lugha unganishi, basi, patakuwa na haja ya kutekeleza tafsiri. Tafsiri itamwezesha mzungumzaji au mwandishi wa matini asilia aweze kuwasiliana namsomaji wa matini husika. Hii ina maana kuwa, iwapo mwandishi wa matini fulani anakusudia ujumbe wake uwafikie watu wa lugha nyingine tofauti na yake, atahakikisha kuwa anaitafsiri kazi hiyo kwa lugha ya walengwa. Kupitia kwa tafsiri, mwandishi wa matini asilia ataweza kuifikia hadhira pana zaidi. Hii ndiyo sababu Picken (1989), anafafanua kuwa kutafsiri ni kule kuwasilisha ujumbe hadi lugha nyingine tofauti na ile ya mwandishi wa matini asilia.

Kuna vitabu vingi ulimwenguni vilivyoandikwa kwa lugha mbalimbali. Ili kupanua usomaji wa matini hiyo, vitabu hivi hutafsiriwa ili kuifikia hadhira pana. Maendeleo ya nchi huenda sambamba na utoaji wa habari kwa wananchi kwa lugha wanayoielewa. Kwa mfano, nchini Kenya, tafsiri ya katiba kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili ilisababisha Wakenya wengi kujumuika katika welewa wa katiba yao. Hii ilikusudiwa kuhakikisha kuwa aghalabu wananchi wote wanapokea ujumbe uliomo kwenye katiba hiyo. Kutokana na wananchi kuelewa katiba, tunapata kuwa nchi inapiga hatua ya kimaendeleo kwa kuwa wananchi hufuata kanuni zifaazo ili kuchangia amani, umoja na utangamano wao. Katika hali kama hii, tafsiri inakuwa ni nyenzo muhimu katika ukuaji wa mawasiliano miongoni mwa wananchi na hivyo kuimarisha uchumi.

1.1.1 Tafsiri na mawasiliano

Wataalamu mbalimbali wamefafanua dhana ya tafsiri kwa namna tofauti tofauti. Mukuthuria (2007) anasema kuwa kutafsiri ni kuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa matini asilia katika lugha pokezi kama ilivyowakilishwa na lugha asilia. Na ujumbe huu usiwe na ugeni wowote isipokuwa matumizi ya maneno yenye visawe katika lugha pokezi. Bitugi (2007) kwa upande wake anaeleza kuwa tafsiri inahusu kubadilisha ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine huku ukihifadhi maana na mantiki.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni kweli kwamba tafsiri huhusu uhamishaji wa ujumbe kutoka lugha moja hadi lugha nyingine kimaandishi. Lengo kuu huwa kukamilisha mawasiliano. Tafsiri katika hali hii huwa njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa mawasiliano baina ya mwandishi wa matini asilia na hadhira ya matini pokezi yanafanikiwa. Ufanisi huu kwa kweli hutegemea uaminifu wa mtafsiri katika kuhifadhi ujumbe wakati anatafsiri.

Mawasiliano kutokana na tafsiri ya matini hufanikiwa iwapo msomaji wa matini pokezi na mwandishi wa matini asilia wataelewana. Mwandishi wa matini asilia huenda akawa na haja ya kufikia hadhira pana; labda hata wale walio nje ya nchi yake. Lakini kutokana na kupatwa na changamoto ya kukosa umilisi wa lugha ya hadhira lengwa, huenda hiyo ikawa sababu ya kukosa kuwafikia. Kwa hali kama hii, anaweza kumtafuta mtafsiri wa kazi yake ili kuifikia hadhira lengwa. Wakati mwingine, mtafsiri mwenyewe anaweza kuwa na haja ya kuitafsiri kazi fulani labda kwa nia ya kujipatia mapato au labda kwa kuipenda ile kazi na kutaka wengine pia wanufaike. Hali hizi zote husaidia kufanikisha mawasiliano baina ya wanadamu.

Ili kufanikiwa katika tafsiri, mtafsiri atahitaji kutumia mbinu mahsusi ya kuitafsiri kazi yake ili kuhakikisha kuwa anawasilisha ujumbe wa mwandishi pasipo kuzua utata. Mbinu anazochagua mtafsiri huathiri jinsi atawasilisha mawazo ya mwandishi wa matini asilia na hivyo kuamua ama kutimia au kukosa kutimia kwa mawasiliano (Nida na Taber, 1969; Gumperz, 1971). Mtafsiri ana jukumu la kuteua namna ya kuhakikisha kuwa kazi tafsiri inapokewanahadhira pokezi kwa namna alivyokusudia mwandishi wa matini asilia. Ufanisi huu utategemea mbinu za tafsiri anazotumia mtafsiri na hivyo kukamilisha mawasiliano.

1.1.2 Historia fupi ya tafsiri

Tafsiri imekuwa ikiendelezwa kwa miaka mingi iliyopita kwa hivyo ina historia ndefu. Zakhir (2010) akielezea historia ya tafsiri anasema kuwa tafsiri inaaminika kuanza pale wanadamu walipoanza kuwa na lugha tofautitofauti. Hii ni kutokana na historia ya Biblia kuhusu wakati wanadamu walishirikiana kujenga mnara wa Babeli wakiwa na nia ya kumfikia Mungu mbinguni. Mungu alipoona ushirikiano wao, aliamua kuwatawanya. Aliwapa lugha tofautitofauti ili wasielewane na hivyo kutoendeleza ujenzi huo (Biblia: Kitabu cha Mwanzo 11:9). Hapo ndipo

panapoaminika kuwa chanzo cha tafsiri. Hata hivyo, McGuire (1980) anaamini kuwa tafsiri ni uvumbuzi wa Warumi.

Mwansoko (1996) anaelezea tafsiri kama taaluma iliyotokana na haja ya kuieneza elimu ya Wamisri kule Ulaya. Hata hivyo, elimu hii ilipigwa vita kule Ulaya kwa kudhaniwa kuwa ni mafundisho ya kipagani. Baadaye, elimu hii ilionekana kuwasaidia Waarabu kujiendeleza kisayansi. Wataalamu wa Ulaya walichukua vitabu vya sayansi vya Kiarabu na kuvitafsiri ili kupata maarifa hayo. Huu ulikuwawakati wa mwamko mpya wa taaluma hii ya tafsiri kule Ulaya.

Munday (2001) anasema kuwa tangu karne ya nne, tafsiri iliendelezwa kwa kiwango cha juu. Maendeleo haya yalisitishwa kuanzia karne ya sita hadi ya kumi na moja, almaarufu kama 'zama za giza'. Hata hivyo, hali ilibadilika kuanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita. Kulikuwa na mvuvumko wa Kikristo ambapo tafsiri za Bibilia zilizidishwa mno. Panapo karne ya kumi na saba, mtafsiri alilinganishwa na msanii anayejukumika kwa mwandishi wa matini asilia na kwa mpokezi wa matini tafsiri. Kwa hivyo kazi hii iliendelea kushika kasi sana. Kufikia karne ya kumi na tisa, kulitokea mgogoro kati ya makundi mawili. Kundi la kwanza lilimtaazama mtafsiri kama msanii mashuhuri katika fasihi na lugha, huku kundi lingine likimwona mtafsiri kama anayejaribu kuonyesha umashuhuri wa mwandishi wa matini asilia. Watafsiri hasa katika nchi zilizoendelea walitafsiri vitabu vya wanasayansimashuhuri kwa minajili ya maendeleo nchini. Mwansoko (1996) anaendelea kueleza jinsi taaluma ya tafsiri ilivyoshika kasi katika karne ya ishirini, kwamba kulikuwa na wingi wa mfumko wa kazi za tafsiri. Kwa mfano, mikataba ya kimataifa baina ya mashirika ya umma na ya kibinafsi yalitafsiriwa kwa yeyote yule aliyehitaji taarifa hizo. Karne hii ya ishirini na moja imeshuhudia ukuaji mkubwa wa taaluma hii ya tafsiri. Uimarikaji

wa teknolojia umechangia ongezeko la kazi za tafsiri. Kiwango cha tafsiri kimezidi kupanda hasa kwa kuwepo kwa programu mbalimbali za tafsiri kwenye mtandao.

Tafsiri hivyo basi ni taaluma yenye historia ndefu na inazidi kupanuka kila uchao. Taaluma nyingi zimebobeza kwenye ulingo wa tafsiri kwa nia ya kupanua hadhira yake. Kwa mfano, vyombo vya matangazo na burudani kama vile magazeti, televisheni, majarida mbalimbali, video na kadhalika vinatafsiri jumbe zao kwa lugha mbalimbali. Kwa mfano, matangazo kwenye runinga hupeperushwa kwa lugha ya Kiingereza na ujumbe uleule ukawasilishwa hapo baadaye katika lugha ya Kiswahili. Huu ndio mfano wa tafsiri kwa sababu ujumbe uleule unabakia vile ila unawasilishwa kwa lugha nyingine kando na ile ya awali.

Biblia ikiwa moja kati ya matini inayotegemewa na kutumiwa na watu wengi wa imani ya Kikristo, imekuwa ikipanua hadhira yake kwa kasi kutokana na ongezeko la wasomaji wake. Ongezeko hili limesababishwa na matini haya kutafsiriwa katika lugha mbalimbali na kuifanya iwafikie watu katika lugha wanayoilewa zaidi. Biblia imekuwa ikitafsiriwa hadi lugha mbalimbali na katika awamu tofautitofauti kama tunavyoona katika sehemu ifuatayo:

1.1.2.1 Kipindi cha kale

Katika awamu hii, tafsiri ya kwanza ilihusu tafsiri ya sheria za Wayahudi iliyofanyika wakati wana wa Israeli walikuwa mateka katika nchi ya Babeli. Wakati huu, lugha ya Kiarabiki ilikuwa ndio *lingua franca* ya Wayahudi. Kwa hivyo, tafsiri kutoka Kiebrania hadi Kiarabiki ikatekelezwa kwa kuwa lugha ya Kiebrania haikuwa inaeleweka kwa watu wengi.

Mfalme Ptolemy wa pili wa Filadelfia, aliwaajiri wataalamu sabini na wawili wa Kiyunani kati ya 285 na 246 K.Y.M ili kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kiebrania hadi

Kigiriki. Biblia hiyo ilijulikana kama ‘Septuagint’ ambayo baadaye kanisa lilikubaliana kuwa ndiyo Agano la Kale. Kisha baada ya hapo, Jerome alitafsiri Biblia kutoka lugha Kiebrania hadi lugha ya Kilatini kati ya 382 hadi 420 B.Y.M. Katika kipindi hiki, tafsiri nyingi za Biblia zilitekelezwa kwa lugha za Kiebrania na Kigiriki. Tafsiri ziliendelezwa na kufikia karne ya tano, Biblia ilikuwa imetafsiriwa kwa lugha chache mno zikiwemo: Kiarmenia, Kigothi (Gothic), Kisiria na Kilegi (lugha ya Ethiopia).

1.1.2.2 Kipindi cha kati

Hiki ni kipindi ambacho tafsiri ya sehemu ya Agano la Kale ilipingwa. Hata hivyo, kulikuwa na tafsiri chache kwa mfano, Bede alifanikiwa wakati huu kutafsiri Injili ya Yohana katika Kiingereza cha kale. Toleo la Kijerumani pia lilimalizika mnamo 748. Kipindi hiki pia kilihakikisha kuwepo kwa sehemusehemu za Biblia zilizotafsiriwa katika lugha ya mama; hasa sehemu yenye sheria kumi za Mungu. Mnamo 990, kulikuwa na vitabu vinne vya injili vilivyokuwa katika Kiingereza cha kale, vilitafsiriwa hadi lahaja ya ‘West Saxon’.

Mnamo 1199, baadhi ya tafsiri katika lugha ya mama zilikubalika huku nyingine zikipingwa na Papa Innocent wa tatu. Biblia nzima ilitafsiriwa katika lugha ya Kifaransa cha kale mwishoni mwa karne ya kumi na tatu, huku Biblia katika lugha ya KiCzech ikikamilishwa mnamo 1360. Biblia katika lugha ya Kihangaria ilipatikana katikati mwa karne ya kumi na tano. William Caxton nayealikamilisha tafsiri yake ya sehemu kubwa ya Biblia mnamo 1478 katika lugha ya Kivalensia.

1.1.2.3 Kipindi cha mfufumko na usasa wa kale

Mtafsiri mashuhuri katika kipindi hiki alikuwa ni Martin Luther, ambaye katika mwaka wa 1521 alitafsiri Agano Jipya kutoka lugha ya Kigiriki hadi Kijerumani.

Biblia ya kwanza ya Kidachi iliyotokana na tafsiri ya Luther ilichapishwa mnamo 1526.

Mfufumko wa makanisa ya Kiprotestanti ulisababisha Biblia kutafsiriwa na kuchapishwa kwa lugha nyingi. Vilevile kazi za kimishenari zilisababisha kutekelezwa kwa tafsiri nyingi za karne ya kumi na saba, ambapo Biblia ilitafsiriwa katika lugha za dunia ya sasa.

1.1.2.4 Kipindi cha sasa

Biblia katika kipindi hiki inaendelea kuongoza kama kitabu mashuhuri kinachotafsiriwa duniani hivi sasa. Kufikia mwaka wa 2005, Biblia ilikuwa imetafsiriwa hadi aghalabu lugha 2400 duniani; ikiwemo lugha 680 katika Afrika. Shirika la kufanya tafsiri za Biblia liitwalo ‘United Bible Societies’ lilitangaza kuwa kufikia tarehe thelethini ya Desemba mwaka wa 2007, Biblia ilipatikana katika lugha 438, huku sehemu za Bibliazikipatikana katika lugha 848 kati ya jumla ya lugha 2400. Kufikia mwaka wa 2009 Shirika la ‘The Wycliff Bible Translators’ kwa upande wake lilitangaza kuwa lengo lao ni kuhakikisha kuwa kufikia mwaka wa 2025, lugha zisizokuwa na Biblia katika lugha yao ziweze kushughulikiwa.

1.1.3 Kazi ya kutafsiri Biblia nchini Kenya

Majilio ya Wamishenari humu nchini ndiyo chanzo cha Biblia kutafsiriwa katika lugha ya kiasili. Wamishenari walipofika pwani ya Kenya mnano 1844, walikuwa na lengo moja la kueneza dini ya Kikristo. Jambo moja lililokwamiza kazi hii lilikuwa ni kutoelewana kilugha na wenyeji wa bara. Hali hii ilikwamiza maenezi ya dini hii kwa muda na wamishenari wakiongozwa na Ludwig Krapf walibuni mikakati mwafaka ya kuikabili hali hii. Hapo ndipo walipoamua kujifunza lugha ya wenyeji na kisha kutafsiri sehemu za Biblia katika lugha itakayoeleweka kwa wenyeji. Kazi ya kutafsiri

Biblia ilianzishwa na mmishenari Ludwig Krapf ambaye alitafsiri kitabu cha Mwanzo katika lugha ya Kirabai mwaka wa 1845 (Wikipedia 12/01/2015).

Mbiti (2015) anasema kuwa kazi ya tafsiriya Biblia katika lugha ya mama imeendelea kunawiri tangia wakati wa wamishenari, sio tu hapa nchini bali hata katika Afrika nzima. Mbiti anasema kuwa kufikia Januari mwaka wa 2013, kati ya takriban lugha 2000 za Afrika, tafsiri ya Biblia imetekelezwa kwa lugha 748 ikiwemo lugha ya Kikalenjin.

1.1.4 Biblia katika lugha ya Kikalenjin

Kazi ya kutafsiri Biblia ya Kikalenjin ilianzishwa na mmishenari aliyeitwa Stuart M.Bryson, kutokana na haja yake ya kuifikishia jamii ya Wakalenjin imani kumhusu Yesu kristo. Bryson alianzia kazi ya umishenari Kijabe katika chuo cha Biblia cha Moffat na baadaye akaenda sehemu ya Kapsabet ambapo alisimamia kituo cha Africa Inland Mission (A.I.M). Akiwa Kapsabet, alianzisha shughuli za kutafsiri Biblia katika lahaja moja ya Kikalenjin ambayo ni Kinandi. Alisaidiwa na mchungaji mmoja kwa jina Rev. Samuel Gimnyige, na wakafaulu kumaliza kazi hii mwaka wa 1939; baada ya miaka kumi (Bryson 1959). Hii ilikuwa Biblia ya kwanza nchini kutafsiriwa katika lugha ya wenyeji wa Kenya. Baadaye, ilibainika kuwa lahaja hii ya Kinandi haikumudu matakwa ya kimawasiliano baina ya Wakalenjin wote kwa sababu ya tofauti za kilahaja. Hapo ndipo walipoanzisha mikakati ya kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin (inayojumuisha lahaja mbalimbali). Kazi hii ilikamilika mwaka wa 1969 chini ya kamati ya wazee wasomi kwa wakati huo (akiwemo Hayati rais Toroitich Arap Moi) kutoka lahaja mbalimbali za Kikalenjin, ili kuwezesha watu wa lahaja mbalimbali za Kikalenjin kushiriki kwa kutumia Biblia kwa lugha moja.

1.1.5 Tafsiri na teknolojia

Uimarikaji wa mitandao ya kimawasiliano pamoja na uimarikaji wa teknohama kutokana na utandawazi, umewezesha kuingiliana kwa tamaduni kati ya mataifa. Hali hii imeimarishwa na watafsiri kubuni mikakati ya kuendeleza tafsiri kwa kutumia nyenzo na mbinu mbalimbali. Kwa mfano, vifaa vya kiteknolojia vya kisasa kama vile sinema, video, televisheni na kadhalika, vina programu zinazoweza tafsiri kwa wepesi. Hata kama teknolojia hii wakati mwingine hudaiwa kutekeleza tafsiri hafifu, lakini cha mno ni kuwa imewezesha mawasiliano kati ya wana uwingi lugha duniani.

Tafsiri ya matini mbalimbali imewezesha walengwa kufikiwa na ujumbe wa mwandishi wa matini asilia kwa kuwa wanaipata katika lugha wanayoielewa. Hii ina maana kuwa, iwapo matini imeandikwa kwa lugha isiyofahamika kwa walengwa, basi ni lazima itatafsiriwa kwa lugha wanayoifahamu ili wapate ujumbe wa mwandishi. Kama wanavyofafanua Hatim na Mason (1994), mtafsiri ana jukumu la kupitisha mawazo yaliyokusudiwa na mwandishi akiongozwa na ukweli uliopo kwenye matini aliyoisoma na kuelewa. Hiki ni kile alichokiita Shitemi (1997), uaminifu wa tafsiri; yaani mtafsiri anafaa kuitafsiri kazi kiasi cha kuwa hapatatokea upungufu wowote utakaopelekea matini tafsiri kushukiwa kuwa si matini asilia. Endapo kile kilichokusudiwa na mwandishi wa matini asilia hakitabainika katika matini tafsiri, basi matini hiyo haiwezi ikaaminika. Hata hivyo, kuna uwezekano wa ujumbe kukosa kuwasilishwa kwa kutumia mbinu na muundo wa lugha asilia na hivyo kuipa matini pokezi sura mpya. Hali kama hii basi itakuwa ni uandishi upya wa matini ileile.

1.1.6 Uandishi upya katika tafsiri ya Biblia

Biblia ni kitabu kimojawapo cha vitabu vitakatifu ulimwenguni. Hiki ni kitabu mashuhuri chenye misingi ya imani ya Kikristo, na ambacho kinaaminika kubeba mawasiliano maalumu kutoka kwa Mungu hadi kwa binadamu. Hii ndiyo sababu

kitabu hiki kinajulikana kuwa kikongwe sana ulimwenguni. Mungu alipomuumba mwanadamu, moja kwa moja, alianza kuwasiliana naye. Maandishi ya kwanza ya Biblia yalitekelezwa na Mungu mwenyewe pale ambapo aliandika amri kumi na kumpatia Musa ili awape wana wa Israeli (Biblia: Kutoka 20:1-17). Baadaye, Musa alirudia kuziandika amri zile kwa sababu alikuwa ameziharibu zile zilizoandikwa na Mungu mwenyewe. Kuanzia hapo, vitabu vingi vya Biblia viliendelea kuandikwa na watu mbalimbali wakiongozwa na uwezo wa Mungu, kama vile manabii Isaiah, Ezekieli, Amosi, Ezra na wengine, waliojumuika kuandika Agano la Kale. Baada ya Yesu Kristo kuja na kuondoka ulimwenguni, mitume waliandika sehemu ya pili ya Biblia inayoitwa Agano Jipya; wengi wa waandishi hawa walitoa ushuhuda wa kazi zake Yesu akiwa ulimwenguni, pamoja na shuhuda za watu waliomjua Yesu Kristo baada ya yeye kuondoka duniani, kama vile barua zake Paulo.

Kwa hivyo, ni kweli kuwa Biblia ni kitabu kitakatifu, na kinachoaminika kubeba ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wanadamu. Hii ina maana kuwa mtafsiri anapotekeleza kazi yake, anafaa kuzingatia kuhifadhi ujumbe kwa makini sana kwa kuzingatia onyo hili:

“Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.” (Biblia: Ufunuo wa Yohana 22:18-19)

Wataalamu kama vile Catford (1965), Nida na Taber (1969), Toury (2012), Pym (1995) na Biamah (2012) wanadahili kuwa tafsiri inahusu ulinganifu wa ujumbe wa matini asilia na matini pokezi; kwamba mtafsiri ana jukumu kuu la kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye matini tafsiri ni yale yaliyomo kwenye matini asilia. Ulinganifu huu wakati mwingi hubainika kuwa tata mno kwa kuwa ni vigumu kuwa na lugha mbili

zinazofanana au kuafikiana kimuundo na hata kimtindo. Isitoshe, wakati mwingi tamaduni huweza kutofautiana baina ya lugha ya matini asilia na matini pokezi. Mtafsiri katika hali kama hii, atajipata akiandika kazi ile upya tena.

Kila lugha huwa na muundo wake bainifu na ili kuwasiliana kikamilifu, ni lazima kaida za lugha hiyo zifuatwe. Kwa mfano, kila lugha ina muundo wake wa virai, vishazi na sentensi. Ili kufanikisha tafsiri, lazima mtafsiri azingatie muundo wa lugha lengwa; vilevile uteuzi wa maneno na msamiati unafaa kuzingatiwa ili kutekeleza tafsiri kamilifu. Lugha nyingine huweza kuwa na hali ambapo neno huwa na zaidi ya maana moja. Mtafsiri hivyo anastahili kufanya uchunguzi zaidi kuhusu muktadha wa kimatumizi wa neno husika kabla ya kuamua kulitumia. Hii ina maana kuwa atakuwa anaandika upya neno hilo.

Hatim na Mason (1994), Newmark (1988) pamoja na wataalamu wengine wa tafsiri wameeleza kuwa ili kutafsiri, mtafsiri lazima atoe mbinu mwafaka za kutumia ili kufanikisha kazi yake. Ujumbe wa mwandishi wa matini asilia hufanikiwa kutegemea mbinu anazotumia mtafsiri. Mbinu hufanikisha au kutofanikisha mawasiliano. Ili mawasiliano yafaulu, itagharimu mwasilishaji wa ujumbe (mtafsiri) kuchukua jukumu la kuteua njia mwafaka ya kutumia ili kuwasiliana na hadhira pokezi kama alivyofanikiwa mwandishi asilia katika hadhira yake. Ili kutafsiri Biblia, mtafsiri atachagua mbinu mwafaka ilmuradi aweze kupitisha ujumbe kwa namna itakavyoeleweka kwa hadhira pokezi. Kwa kuwa lugha mbili haziwezi kuwa sawa, mbinu za kutafsiri huweza kuchangia kazi tafsiri iwe ni uandishi upya. Biblia imetafsiriwa katika lugha nyingi duniani. Hivyo, kuna uwezekano kuwa ikiwa mbinu za kutafsiri zilizotumika katika tafsiri hizo ni tofauti na zile za Biblia ya kwanza, ina maana kuwa kuna uandishi mwingi mpya wa Biblia ulimwenguni.

Lengo kuu la kuandika Biblia ni kupitisha ujumbe wa Mungu kwa watu wote ulimwenguni. Biblia iliandikwa mwanzoni kwa kutumia lugha za Kiebrania, Kiaramaiki na Kigiriki. Baadaye, ujumbe haukuweza kufikia watu wasiokuwa wazungumzaji wa lugha hizi tatu. Upungufu huu ulizua haja ya tafsiri zaidi. Tafsiri ingehakikisha kuwa watu wote wanapata ujumbe wa Mungu, kama alivyokusudia. Hii ilipelekea kubuniwa kwa mikakati ya kutafsiri Biblia aghalabu katika lugha zote ulimwenguni.

Mtindo wa kiuandishi huweza kutofautiana baina ya lugha asilia na lugha pokezi, hasa ikizingatiwa kuwa mwandishi wa matini asilia (M.A) - Biblia ya Kiswahili- ni tofauti na mtafsiri wa matini pokezi (M.P)- Biblia ya lugha ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*). Isitoshe, hadhira ya matini ya lugha ya Kiswahili ni tofauti na hadhira ya matini ya lugha ya Kikalenjin; wao wana utamaduni tofauti na falsafa zao ni tofauti kabisa; hasa kutokana na tofauti za kimazingira. Hali hii humlazimu mtafsiri kujikwamua kwayo ili kuifikia hadhira yake kwa njia ambayo kazi yake haitaonekana kuwa ni kazi tafsiri ila kazi asilia na yenye kuafiki hadhira lengwa. Ili kufaulu, mtafsiri aliandika upya M.P.

Tafsiri ni kitendo kinachoongozwa na mfumo pamoja na itikadi zilizopo katika jamii husika. Kwa kuwa itikadi na mifumo ya jamii husika ni tofauti, utafiti huu ulichunguza mtafsiri alivyofaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi asilia, huku akizingatia tofauti hizi.

1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umelenga kuchanganua uandishi upya wa Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit NeTilil*) Utafiti huu umejikita hasa katika kuchanganua kitabu cha Mithali. *Bukuit Ne Tilil* ilitafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiswahili katika miaka ya sitini. Kama

tujuavyo, Lugha ya Kiswahili na Kikalenjin ni tofauti kwa kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu huku Kikalenjin ikiwa ni lugha ya Kinailoti. Hii ina maana kuwa lugha hizi mbili zinatofautiana kisemantiki, kisintaksia, kifonetiki na hata kimofolojia. Isitoshe, Katika kipindi kile cha kutafsiri *Bukuit Ne Tilit*, Wakalenjin waliishi sehemu za Bonde la Ufa huku wazungumza lugha ya Kiswahili wakiishi pwani. Mazingira kwa kawaida huchangia kwa wanadamu kujihusisha na shughuli mahsusi ili kujiendeleza kijamii na kiuchumi. Shughuli hizi ndizo zinazozalisha tamaduni zinazopelekea lugha kutofautiana. Kutokana na ukweli huu, ndipo lugha ya Kiswahili inatofautiana na lugha ya Kikalenjin. Wakati wa kutafsiri, mtafsiri anafaa kuangazia tofauti hizi ili kumudu tafsiri yake.

Biblia Takatifu iliandikwa kwa lugha ya Kiswahili ikiwalenga wazungumza lugha ya Kiswahili. Mtafsiri wa lugha ya Kikalenjin alizingatia ukweli kuwa anaowatafsiria, ambao ni Wakalenjin, wana mila na tamaduni tofauti na za Waswahili. Katika kutafsiri, alilazimika kuandika upya M.P kwa namna inayoeleweka kwa Wakalenjin na kuafikiana na mila na desturi zao. Ni kwa msingi huu ambapo utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza sababu zilizopelekea mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilit* kuandika upya M.P, ili kuwafikia Wakalenjin na ujumbe uliopo kwenye Biblia Takatifu.

1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua uandishi upya unaobainika katika Biblia ya Kikalenjin iliyotafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Ili kulitimiza lengo hili utafiti uliongozwa na madhumuni mahsusi yafuatayo:

1. Kuchunguza jinsi vipengele vya kitamaduni katika matini teule ya Kiswahili na Kikalenjin vilivyosababisha mtafsiri kuiandika upya *Bukuit Ne Tilit*.

2. Kupambanua namna matumizi ya mikakati ya kutafsiri ilivyochangia katika uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*.
3. Kutathmini mbinu za tafsiri zilivyochangia katika uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*.

1.4 Nadharia Tete za Utafiti

Nadharia tete zilizoongoza utafiti huu ni zifuatazo:

1. Tofauti kati ya vipengele vya kitamaduni baina ya matini teule ya Kiswahili na Kikalenjin ndizo zinazosababisha uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*.
2. Mikakati iliyotumika kutafsiri Biblia Takatifu ndiyo iliyopelekea uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*.
3. Mbinu zilizotumika katika kutafsiri Biblia Takatifu, zilipelekea uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Kuendelea kwa taaluma ya tafsiri hasa katika karne hii ya ishirini na moja kumesababisha kuwepo kwa tafsiri nyingi. Vitabu vingi, majarida, magazeti na maandishi mengi yanaendelea kutafsiriwa kila uchao. Biblia ya Kikalenjin ni mojawapo ya kazi tafsiri zilizoendelezwa kwa karne nyingi zilizopita. Tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin haijawahi kuchunguzwa ili kupambanua hali ya uandishi upya wake. Hii ndiyo sababu iliyompelekea mtafiti kuchunguza kazi hii ili kukadiria kiwango cha uandishi upya.

Miundo na mitindo ya lugha mbalimbali hutofautiana. Hali hii huweza kutatiza tafsiri kwa namna mbalimbali. Sababu ya kutafitia mada hii ni kutathmini tofauti kati ya lugha ya Kiswahili na Kikalenjin wakati wa kutafsiri. Tathmini hii haujawahi

kufanywa wakati mwingine kulingana na uchunguzi huu, hivyo kuwa kichocheo cha kutekeleza utafiti huu.

Hamu ya kutaka kubaini tofauti za vipengele vya kitamaduni baina ya lugha ya Kiswahili na Kikalenjin imekuwa ni kichocheo cha utafiti huu. Vilevile, nilitaka kujua ni vipi tofauti hizi zilikabiliwa na mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil* ili kuhakikisha kuwa anahifadhi ujumbe asilia. Isitoshe, palikuwa na haja ya kuchunguza ufanisi wa mtafsiri katika kazi yake.

Mwisho ni kuwa, uchunguzi wa kazi tafsiri umelenga kwa uchache sana tafsiri za matini ya Biblia. Hali hii imechochea utafiti huu kwa kuwa uwanja huu wa kidini ni mashuhuri sana tukitazama idadi ya kazi zilizotafsiriwa kwa lugha za kasili. Kazi zilizotafsiriwa zilimpa mtafiti mawanda makubwa ya kudurusu na kupata mchango wa utafiti wake. Isitoshe, hakuna uchanganuzi wowote wa awali, kadri ya uchunguzi wa mtafiti, kuhusiana na mada aliyoitafitia, kwa hivyo, utafiti huu umezua data za kipekee.

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatakuwa na manufaa ya kitaaluma, hasa kwa kuchangia katika kuboresha taaluma ya tafsiri ambapo matokeo yake yataongezea kwenye marejeleo ya kitaaluma na hivyo kuwafaa wanafunzi, hasa wanaozamia kwenye kozi ya tafsiri. Wanafunzi watatumia matokeo ya utafiti huu kuendeleza welewa wao kuhusiana na tafsiri za kazi za fasihi. Aidha, iwapo kutazuka upungufu kutokana na utafiti, utaweza kutumika kuzua suala jengine litakalofanyiwa utafiti na wanafunzi hao.

Vilevile, matokeo ya kazi hii yatatoa mchango mkubwa kwa watafsiri kwani kupitia mapendekezo yaliyowasilishwa mwishoni mwa utafiti huu, wanaweza kupata

mwanga kuhusiana na namna ya kuhakikisha kuwa tafsiri inatekelezwa kwa kiwango cha juu. Wataona kutokana na matokeo ya utafiti huu kuwa, uandishi upya katika tafsiri ni muhimu katika kuhifadhi ujumbe wa M.A. Aidha, Kwa kuzingatia mbinu zitakazopendekezwa na uchunguzi huu, watafsiri watafanikiwa katika kazi zao.

Wahakiki wa kazi tafsiri wanaweza kunufaika kutokana na utafiti huu kwa kuweza kufahamu hali mbalimbali zinazowakumba watafsiri hivi kwamba nia yao ya kutafsiri matini asilia huishia kuwa ni kuandika upya matini asilia. Na labda kwa hali hiyo, kukubali matini hiyo kama ni tafsiri ya matini asilia wala wasiitazame kama kazi iliyoandikwa upya. Huenda pia wahakiki wakakubaliana na hali kuwa hakuna tafsiri iliyo kamilifu kwa asili mia moja.

Isitoshe, kwa kuwa utafiti huu unachanganua makala ya kidini, matokeo ya kazi hii yatakuwa ya manufaa sana kwa watafsiri wa makala ya kidini, hasa dini ya Kikristo. Watafsiri hasa wa Biblia za lahaja mbalimbali za Kikalenjini watatumia matokeo ya utafiti huu kama marejeleo katika kufanikisha kazi zao. Hii ni kwa sababu upungufu wowote utakaopatikana kutokana na tafsiri ya Biblia ya Kikalenjini utaweza kuzingatiwa kwa makini ili kukwepa upungufu kama huo katika tafsiri zao.

1.7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza uandishi upya unaojitokeza katika kazi za tafsiri. Tulichunguza tafsiri ya Biblia kutoka kwa lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjini; hii ikiwa ni mfano mzuri wa tafsiri aliyotaja Jakobson (1959) kuwa ni tafsiri baina ya lugha mbili tofauti. Lugha ya Kikalenjini ni lugha ya Kinailoti huku Kiswahili ikiwa ni Kibantu. Lugha hizi mbili hutofautiana kisarufi na hata kisintaksia. Tofauti hii ilitusaidia kufikia malengo yetu ya utafiti kwani tuliweza kubaini jinsi tofauti kama hizi huchangia katika uandishi upya katika kazi za tafsiri.

Biblia kijumla, imegawika katika sehemu mbili kuu, yaani, tunapoanza kufunua Biblia, tunapata Agano la Kale lenye vitabu 39 na baadaye tunafikia sehemu ya Agano Jipya lenye vitabu 27; ambavyo vina maandishi yanayohusu mafunzo ya Yesu Kristo, wafuasi wakepamoja na mashahidi wake. Katika hivi vitabu vyote, tulichagua kitabu kimoja katika Agano la Kale, kiitwacho Mithali. Hiki ni kitabu kilichoandikwa na mfalme Suleimani; mtu mashuhuri sana katika dini ya Kikristo kutokana na hekima aliyopewa na Mungu (Biblia: I Wafalme 4:29-30). Kitabu hiki kilifaa kutokana na wingi wa vipengele vinavyohusu tamaduni. Isitoshe, vifungu vya kitabu hiki vimekamilika kimaana, na hivyo kurahisisha uchanganuzi wake, hasa katika kulinganisha maneno na maana yake. Vipengele hivi vilitupa nafasi nzuri ya kulinganisha matini ya Kiswahili na ya Kikalenjin ili kufikia malengo ya utafiti huu.

Kwa sababu ya tofauti za kitamaduni kati ya lugha ya Kiswahili na Kikalenjin, mtafsiri kwa kweli hupatawa na changamoto katika kazi yake. Mandhari ya kiuandishi mara nyingi, huweza kuleta kizingiti kikubwa wakati wa kutafsiri dhana mbalimbali. Hii ndiyo maana tulikiteua kitabu hiki pekee kati ya vitabu vyote kwenye Biblia kwa kuwa ilikuwa rahisi kupata data iliyobainisha mandhari ya kiuandishi wa M.A na ya M.P.

Kitabu cha Mithali kina jumla ya sura thelathini na moja. Katika uchunguzi wetu, tulikuwa tukinukuu vifungu kadha wa kadha kutokana na sura mbalimbali katika kitabu kizima, bila kubagua sura wala vifungu vyovyote. Tulilenga tu vifungu vilivyoakisi malengo ya utafiti wetu.

Mwisho, kitabu cha Mithali kina vifungu vifupi. Vilevile, ujumbe hufungiwa katika kifungu kimoja au viwili. Isitoshe kitabu hiki hakina masimulizi marefu yanayohitaji msomaji kuyafuatilia kwa urefu ili kupata ujumbe mzima. Hali hii ilinifanya

kukipendelea kitabu hiki. Uchambuzi wake uliwezekana kwa kuwa wakati wa kulinganisha ujumbe, kifungu kimoja kilichanganuliwa pasipo kukihusisha na kifungu kingine. Jambo hili ndilo lililompelekea mtafiti kuchagua kitabu hiki.

1.8 Hitimisho

Sura hii imeangazia mambo mbalimbali yenye kutilia msingi utafiti huu. Kwa mfano, tumeangazia mambo yanayohusu suala kuu lililotafitiwa, malengo ya mtafiti kutekeleza utafiti wake, nadharia tete zilizoongoza utafiti wenyewe, upeo wa utafiti huu miongoni mwa mambo mengineyo. Mambo haya yote yamezingatiwa na mtafiti na hivyo kumwezesha kuibuka na matokeo ya utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura hii inatalii kazi za wataalamu na watafiti wa awali wa tafsiri na maandishi mbalimbali ya kitafsiri. Wataalamu hawa ni pamoja na Nida (1964), Baker (1992), Lefevere (1992,2004), Mwansoko (1976), Shitemi (1997), Munday (2001), Orudari (2007) na Inaba (2009) miongoni mwa wengine wengi. Vipengele muhimu katika utafiti huu viliangaziwa kwa kina, huku tukiegemea kwenye matokeo na mapendekezo ya waliochunguza mada hii ili kujaliza upungufu unaotokana na tafiti hizi za awali kuhusiana na malengo ya utafiti huu. Vipengele vinavyoangaziwa katika sura hii ni: tafsiri kama uandishi upya, dhana nzima ya tafsiri, tafsiri na utamaduni, mikakati ya kutafsiri pamoja na mbinu mbalimbali za kutafsiri. Mwisho, tuliangazia kiunzi cha kinadharia ambapo tulitathmini nadharia mwafaka katika utekelezaji wa kazi hii, kwa kuchunguza vipengele vya nadharia kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu.

2.1 Dhana ya Tafsiri

Venuti (1995) anadahili kuwa tafsiri kwa kweli ni uandishi upya wa matini asilia. Anaona matini asilia kama itikadi na falsafa ya mtu au jamii ya mwandishi na kwa hivyo, ili kukidhi mahitaji ya jamii au hadhira pokezi, lazima ifinyangwe kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji hayo; na huu ndio uandishi upya. Matini tafsiri hukubalika kwa wachapishaji, wasomaji au hata watazamaji inaposomeka kwa ufasaha, kutokana na kutokuwepo kwa makosa ya kiisimu, kimtindo n.k. Kupitia kazi tafsiri aina hii, umbo ‘asilia’ hudhihirika kwa kuwa msomaji anaweza kusoma kazi kama hii kwa wepesi kutokana na uhalisia wa kisintaksia. Haya yote huwezekana

kama anavyosema Venuti kuwa uandishi upya utazingatiwa katika muktadha ya hadhira pokezi.

Venuti (1995) katika ufafanuzi wake, anaendelea kudokeza kuhusu kitendo cha kutafsiri kama mkakati ambao viashiria vya M.L.A vinabadilishwa na viashiria kwenye M.L.P kutokana na ufasiri wa mtafsiri. Hii ina maana kuwa viashiria vya kitamaduni vya L.A vinabadilishwa na vile vya L.P. Kwa kufanya hivi, ujumbe wa mwandishi wa matini asilia unafikia H.P bila ya kupotoka au hata kutokea kwa utata katika uwelewekaji wake. Hata hivyo, endapo mtafsiri hataelewa viashiria muhimu vya kitamaduni vya L.P, atapatwa na ugumu wa kutafsiri matini hiyo.

Lefevere (1992) akizungumzia namna ya kutekeleza tafsiri, anaorodhesha kanuni zinazoweza tafsiri kufanyika kwa ufasaha. Ili kubaini kiwango cha matini kutafsirika, yafuatayo huzingatiwa na mtafsiri.

- i) Matini kubwa hupelekea tafsiri kufanyika kwa wepesi. Tunatarajia kuwa tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin ilifanyika kwa wepesi kwa sababu ya ukubwa wa matini hiyo.
- ii) Iwapo ujumbe ni mdogo, basi muundo utakuwa si tata na hivyo kupelekea uwezekano wa tafsiri.
- iii) Tafsiri huwezekana kwa kiwango cha juu iwapo kuna uhusiano kati ya M.A na M.P. K.m Biblia ya Kikalenjin na ya Kiswahili hutafsirika kwa wepesi kwa sababu zote huhusu ujumbe mmoja kwa hadhira moja, yaani, Wakristo.
- iv) Tafsiri huwa bora Zaidi iwapo L.A na L.P zipo kwenye kiwango kimoja cha kitamaduni. Kulingana na kanuni hii, ni dhahiri kuwa tafsiri ya Biblia kwa lugha ya Kikalenjin haikuwa rahisi kwa kuwa

tamaduni za wanalugha hao ni tofauti. Ukweli huu hata hivyo, tuliweza kubaini katika utafiti huu na pia kuchunguzajinsi mtafsiri alivyokabiliana na hali hii.

- v) Tafsiri huwezekana baina ya lugha mbili zisizohusiana iwapo sheria ya 3 na 4 zinawezekeka na uhusiano wao kuzingatiwa kwa makini.
- vi) Wakati wa kutafsiri, (kwa kuwa hakuna lugha mbili zinazofanana) vipengele fulani vya kitamaduni vitaachwa huku vingine vikiongezwa kutokana na tofauti za kimsamiati na kileksia ya M.P. Utafiti wetu umejishughulisha na vipengele hivi ili kupata namna vipengele hivi vilivyoshughulikiwa na mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin.

Kwa mujibu wa Mwansoko (1996), tafsiri ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwake, ufanisi wa tafsiri hulazimu kwamba mawazo yanayoshughukiwa sharti yawe katika maandishi, na kwamba ujumbe kati ya L.A na L.P lazima ulingane. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa kazi hii inashughulikia kazi tafsiri kwa kuwa ni ya kimaandishi, na vilevile, ujumbe ulioko kwenye matini ya Biblia ya Kiswahili ndio uliowasilishwa katika Biblia ya Kikalenjin.

Dhana ya tafsiri inaweza kuelezwa kama kule kuandika upya M.A katika lugha nyingine pasipo kubadilisha maana. Maumbo ya maneno na sentensi yanaweza kubadilika katika lugha pokezi ila maana itahifadhiwa.

2.2 Tafsiri kama Uandishi Upya

Tafsiri imefafanuliwa na wataalamu wa tafsiri kama kuhamisha matini iliyo katika lugha asilia hadi lugha pokezi; yaani kutoka kwa lugha moja hadi lugha nyingine kimaandishi. Mtafsiri anachokifanya ni kuchukua ujumbe mzima uliomo kwenye

matini asilia kisha mwenyewe akafikiria namna ya kuuwasilisha ujumbe huo kwa lugha nyingine; bila kujali jinsi utakavyowalishwa, mradi H.P ipate ule ujumbe. Mara kwa mara, mtafsiri hujipata katika hali ngumu ya kutafsiri ujumbe wa M.A, kwa kuwa L.P haiwi sawa na L.A, wala H.A si sawa na H.P. Kutokana na changamoto kama vile tofauti za kitamaduni na kisarufi, mtafsiri hujipata akijaribu kutafsiri kwa kutumia mikakati mbalimbali ili kufaulu katika shughuli hii nzima. Matokeo hata hivyo, hayawi kama yale ya awali, bali yanakuwa kazi mpya kabisa. Kwa hivyo, huyo mtafsiri atakuwa ameandika matiniasilia kwa njia mpya kabisa na kuipelekea kazi hiyo kuwa uandishi upya.

Kulingana na Ordudari (2007), vipengele vinavyochangia katika kutatanisha tafsiri huhusisha miundo ya sentensi, maana ya maneno, mtindo, methali, misemo n.k na kusababisha kazi tafsiri iwe na sura mpya kando na ile ya awali. Kitabu cha Mithali kinachochanganuliwa katika utafiti huu kina methali na misemo chungu nzima, hivyo tulichunguza jinsi vipengele hivi vinavyopelekea uandishi upya wakati wa kutafsiri. Mbinu za kutafsiri vilevile huhusisha uchanganuzi wa miundo ya sentensi ambayo huchangia maana mahsusi katika matini tafsiri. Utafiti huu ulibaini hali hii ilivyo katika tafsiri ya Bibilia ya Kikalenjin.

Mwasisi wa nadharia ya uandishi upya katika tafsiri ni Lefevere. Katika kazi yake, alipendelea dhana ya uandishi upya kuliko tafsiri; aliona mkakati wa kuhamisha utamaduni kutokana na lugha hadi nyingine ukihusiana na uandishi upya wala sio tafsiri. Kulingana naye, uandishi upya una maana ya tukio la kijamii linalohusu uwezo wa kudhibiti jamii nyingine; yaani, mtafsiri ana hayo mamlaka ya kuandika M.A ili kuafiki mahitaji ya jamii pokezi. Kuafikiana huku ndiko kunakopelekea uandishi huo kuwa mpya (Lefevere 1992).

Lefevere (2004:vii) anawasilisha dhana ya tafsiri kama uandishi upya wa matini asilia anaposema:

Uandishi upya huweza kuingiza dhana mpya, vipera vipya, mbinu mpya na historia ya kibunifu katika fasihi na kuweza kubadilisha utamaduni mmoja na mwengine (FY)

Madai haya vilevile yameshikiliwa na Hermans (2004) anapodai kuwa haiwezekani tafsiri iwe bila ubunifu wa mtafsiri kuingizwa kwenye M.P. Maana yake ni kwamba tafsiri huathirika kwa kiwango fulani na hali mbalimbali zinazomkabili mtafsiri katika kazi yake na kumsababisha asihawilishe M.A moja kwa moja hadi M.P kwa kiwango cha asili mia moja.

Mwansoko (1996:1) anaunga mkono mawazo ya Lefevere kuhusiana na dhana hii ya uandishi upya anaposema kuwa:

..tofauti za kiisimu, kiutamaduni, kihistoria na kimazingira katika lugha hufanya iwe vigumu kufasiri mawazo ya lugha moja katika lugha nyingine bila kupoteza, kupotoshaau kubadili maana, hata kama ni kwa kiwango kidogo tu.

Anachomaanisha Mwansoko ni kuwa haiwezekana kuyapeleka mawazo ya lugha moja hadi lugha nyingine moja kwa moja na ikabaki jinsi ilivyo katika L.P kisintaksia na kimofolojia. Hii inapelekea mtafsiri kutumia mofolojia na sintaksia ya L.P na kwa hiyo sentensi zitabadilika na hata mpangilio wa maneno. Mabadiliko haya ndiyo yanayotelea mtafsiri kuandika upya matini tafsiri. Mtafsiri atakuwa ameandika upya kazi hiyo kwa L.P.

Utafiti wake Mwansoko ulihusu fasihi ambapo alichanganua tafsiri ya tamthilia na ushairi teule ili kuonyesha dhana hii ya uandishi upya katika tafsiri. Tofauti na utafiti wa Mwansoko, kazi hii ilijikita katika maandishi ya kidini ambayo ni ya Biblia. Kanuni ni kuwa ujumbe wa Biblia unafaa kubaki vilevile bila kupunguza wala kuongeza jambo lolote. Lugha za Kiswahili na Kikalenjin hutofautiana sana kisarufi

na isitoshe, tamaduni za Wakalenjin na Waswahili hutofautiana. Tofauti hizi kama alivyobaini Mwansoko ni kuwa huchangia kwenye uandishi upya kwa kuwa hutoa changamoto kwa mtafsiri wakati wa kutafsiri, na hivyo kupelekea kuzaliwa kwa matini mpya. Katika utafiti huu tulibainibaadhi ya changamoto alizokumbana nazo mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin na kumpelekea kuandika upya kitabu cha Mithali.

Newmark (1988) anajadili kuwa kuna vigezo vya kufuatwa wakati wa kutafsiri ili kufaulu katika tafsiri yoyote ile. Vigezo hivyo ni:

- i) Azimio la makala
- ii) Azimio la mtafsiri
- iii) Msomaji na mandhari ya uwasilishaji wa makala tafsiri
- iv) Ubora wa maandishi na uaminifu wa makala tafsiri

Ni vigumu kuoanisha vipengele hivi vyote pasipo kuzuia uandishi upya. Kwa mfano, mtafsiri anaweza kukosa azimio la mwandishi hasa ikiwa si yeye aliyeandika kazi hiyo, na hivyo akatafsiri kulingana na makusudi yake pamoja na azimio lake. Kwa mfano, ikiwa haja yake ni biashara atatafsiri matini kwa kuegemea mkondo wa kibiashara. Vilevile, mandhari ya utunzi huweza kuwa tofauti na yale ya usomaji, hii ina maana kuwa mtafsiri lazima azingatie mandhari ya hadhira yake anapotafsiri. Isitoshe, kazi tafsiri huweza kuwa ya kiwango cha juu zaidi au chini zaidi kuliko ya matini asilia, hivyo kukosa kuaminika. Jumla ya mambo haya yote huzua uandishi upya. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulichunguza uandishi upya unavyojitokeza katika Biblia ya Kikalenjin; na kiasi cha uandishi upya huo katika Biblia ya Kikalenjin.

Mwandishi wa Biblia ya Kiswahili ni tofauti na yuko kwenye mandhari tofauti na yule anayetafsiri hadi lugha ya Kikalenjin. Tofauti hii huweza kuathiri ujumbe unaonuiwa na mwandishi wa matini asilia. Ujumbe ule, ama huweza kuwa na

mashiko sana baina ya Wakalenjin au dhaifu mno kiasi kwamba wanajamii hawa wanaposoma, hukosa kupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa matini asilia. Uchunguzi huu umebaini tofauti hizi kama zinavyodhihirika katika kazi tafsiri hii.

Nida (1988) anaelezea dhana ya uandishi upya kama matokeo ya uteuzi wa maneno usiofaa. Yaani, maneno mengine yanapotumiwa jinsi yalivyo katika lugha asilia yataonekana kama ni uradidi usiofaa. Wasomaji wa kazi ya tafsiri wanaweza kukosa kabisa kubaini kuwa kazi waisomayo ni tafsiri. Katika kuzungumzia hoja hii, Gromova (2004) akihakiki kitabu cha “Mkaguzi wa Serikali” ikiwa ni tamthilia iliyotafsiriwa kutoka, “The Government Inspector” ambayo nayo ilitafsiriwa kutoka lugha ya Kirusi, alibaini kuwa dhana fulani fulani zinaposazwa katika tafsiri na kusalia katika hali zao za awali; hukosa kabisa kuonekana kuwa ni kazi ya tafsiri. Biblia ya Kikalenjin ilitafsiriwa kutoka kwa lugha kadhaa huku lugha ya Kiswahili ikiwa lugha pekee ya Kiafrika iliyotumika. Hii ina maana kuwa, mtafsiri anapojikakamua kujenga uhalisia wa kazi hii katika lugha ya Kikalenjin, huenda akaonekana kuwa anatekeleza uandishi upya. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulitekelezwa ili kubaini ukweli wa madai yao Nida na Gromova.

Fawcett (1997) anadahili kuwa hatuwezi kuhamisha maana katika lugha bali tunabadilisha maana ya lugha asilia na lugha pokezi. Maana ya neno fulani inaweza kuwa pana au finyu mno na ikawa inaleta maana tofauti na ilivyokusudiwa katika matini asilia, basi hapo, uandishi upya utakuwa umetekelezwa. Kubadilisha huku anakosema Fawcett ndiko kule kuandika upya matini. Kwake, anaona kuwa dhana ya tafsiri ni ndoto na haina uhalisia wowote. Utafiti wetu ulichanganua data kutoka *Bukuit ne Tilil* na Biblia Takatifu ya Kiswahili na kukubaliana na Fawcett kuwa ni vigumu kutekeleza utafiti bila kuandika upya M.A.

Askoy (2001) alifanya utafiti wake katika Jamhuri ya Uturuki uliohusiana na tafsiri. Katika utafiti wake, alibaini kuwa kazi nzima ya tafsiri inachukua umbo la uandishi upya kwa kutegemea hali kwamba jamii ina kanuni zake zinazoathiri mchakato wa tafsiri kwa madhumuni ya kuathiri hadhira pokezi kulingana na itikadi zilizomo kwenye jamii husika. Sababu ni kwamba utoshelevu na ukubalifu huhitajika katika tafsiri. Tafsiri inatarajiwa kuwa uandishi upya wa matini asilia, na yenye lugha inayokubalika ili isomwe na umma. Uchunguzi huu ulibaini ikiwa uandishi upya ulihitajika katika kutafsiri kitabu cha Mithali kwa kuwa utamaduni wa Waswahili na wa Wakalenjin ni tofauti. Chanzo ni kwamba jamii hizi huishi katika mazingira tofauti na masafa kijiografia ni mbali.

Kwingineko, Inaba (2001) alifanya uchunguzi kuhusu tafsiri kama uandishi upya. Utafiti wake hata hivyo unatofautiana na huu kwa kuwa ulihusu tafsiri ya matini ya magazeti ya “The Japan Times” na tafsiri yake; “The Japan Times Editorial” inayoandikwa kwa minajili ya wasomaji wa Kijapani wanaojifunza lugha ya Kiingereza. Hata hivyo, utafiti huu uliangazia sajili ya kidini wala si ya gazetini. Hii ina maana kuwa tafsiri ya gazetini ina dhima tofauti na ya kidini; kwa hivyo, tafsiri pia huenda ikawa na uzito tofauti. Hili ndilo lilojibiwa na matokeo ya utafiti huu.

Oduori (2008) akimnukuu Bal (2002) anaonyesha tafsiri kama uandishi upya anaposema kuwa tafsiri inahitaji kuikomboa lugha pokezi kutokana na mipaka inayowekewa ya kuitazama tafsiri kama ni aminifu au linganifu ikihusishwa na lugha asilia. Tafsiri nyingi za Kiswahili kutoka Kiingereza zimejikita katika hali hii ya kutaka kujifungia katika misingi na miundo ya lugha asilia na hivyo kupata tafsiri ambayo ni kama uandishi upya. Je, Biblia ina uhuru huu unaozungumziwa na Oduori? Mtafsiri anapotumia uhuru huu atafanikiwa vipi katika kazi yake? Je, uhuru huu

utumike kwa kiwango gani ili usiathiri tafsiri ile? Majibu ya maswali haya yamebainika mwishoni mwa utafiti huu, kama yalivyodhihirishwa kwenye matokeo ya utafiti.

Inaba (2009) alifanyia utafiti wake tafsiri ya gazeti la Kijapani lililotafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiingereza; na kubaini kuwa tafsiri huchukua muundo wa uandishi upya unaotekelezwa chini ya muktadha wa L.P, utamaduni na itikadi kulingana na mapendekezo ya mteja au mfumo pokezi. Vilevile anadai kwamba ijapokuwa watafsiri hufanya kazi zao kwa bidii na umakini, ni vigumu kwao kuandika kazi inayolingana kabisa na M.A kwa sababu ya changamoto mbalimbali. Hadhira pokezi hutegemea tafsiri ili kupata ujumbe wa M.A. Kulingana na Lefevre (1992), uandishi upya huathiri hadhira pokezi kutokana na kutoeleweka au kutofahamika kwa M.P kwa sababu ya uandishi upya. Kwingineko, Lefevre (1999) anasema tafsiri ni matini yenye ujumbe uliopinduliwa kwa kupewa sura mpya inayoipa tafsiri taswira fulani tofauti na ile ya awali, kutokana na ugumu wa kuwasilisha ujumbe kwa L.P. Ukweli huu unaonekana pale watafsiri walipoingiza visehemu visivyo vya asilia katika M.T. Utafiti huu umejishughulisha na kuchunguza wa vipengele vinavyopelekea Biblia ya Kikalenjin kukubalika kama uandishi upya. Tulibaini kuwa hata ingawa tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil* ililazimu kuandikwa upya, mawasiliano yalikalimika baina ya mtafsiri na H.P, kinyume na anayodai Fawcett.

Nida (1988) anaeleza kuwa kila lugha ina misingi tofauti ya maneno: Uundaji wake, sentensi tofauti, vishazi na virai tofauti, mitindo tofauti ya kuunganisha sentensi na kadhalika. Zaidi ya hayo, kila lugha ina msisitizo wa tamaduni zake na hivyo basi, kuwa na istilahi tofauti. Nida anasema kuwa ni vigumu mtu kuelewa dhana mbalimbali iwapo dhana hizo hazipatikani katika mazingira yao. Kwa mfano, msemu wa Kiingereza “as white as snow” unapotafsiriwa kama ‘nyeupe kama theluji,’

inakuwa vigumu kwa mtu asiyeishi kwenye mazingira yenye theluji kufahamu weupe huo ni wa aina gani. Ili kueleweka, dhana hii itatafutiwa kisawe cha kitu cheupe kinachopatikana miongoni mwa hadhira pokezi. Katika utafiti wetu, tulichunguza namna ambavyo mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin alivyokabiliana na hali hii. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na watu wenye mazingira na tamaduni tofauti sana na jamii ya Wakalenjin. Uchunguzi huu umebaini namna mtafsiri alivyokabiliana na tofauti hizi kwa kuteua msamiati na uundaji wa sentensi kuambatana na sarufi ya L.P.

Mish (1988) anaonekana kufafanua zaidi hoja hii ya Nida anapotoa mfano wa wakati wamishenari wa Kikristo walipozuru Uchina. Walipokuwa wakitafsiri Biblia, walikosa neno lenye maana sawa na “sin”. Kwa hivyo, waliishia kutumia neno “tsui” linalotokana na dini ya Kibudha. Lakini dhana hii haikuwasilisha vilivyo dhana ile ya Kikristo. Hii ni dhihirisho kuwa wakati mwingine, inakuwa vigumu kupata tafsiri inayolingana moja kwa moja na lugha asilia. Ukosefu huu wa kisawe mwafaka unasababisha uandishi upya wa matini tafsiri. Utafiti huu umechunguza mbinu zilizotumiwa na mtafsiri ili kufidia msamiati mbalimbali kwenye matini pokezi.

Isitoshe, tafsiri hutofautiana miongoni mwa watu. Ni makosa kuamini kuwa watu wana welewa sawa wa kazi tafsiri. Hali hii hutokana na misingi ifuatayo, kama anavyodokeza Nida (1988):

- i) Tofauti kutokana na viwango vya elimu.
- ii) Kazi anayojihusisha nayo msomaji.
- iii) Upendeleo wa msomaji.

Tofauti hizi ndizo nguzo ambazo huathiri jinsi ambavyo kazi moja iliyotafsiriwa inaweza kuwa tofauti na nyingine. Hii ina maana kuwa uandishi upya hujitokeza kila

wakati tafsiri inapotekelezwa. Hata hivyo, utafiti wetu ulinuia kubaini madai haya, hasa kwa kuchunguza matini iliyotafsiriwa. Matini haya yalichunguzwa ili kutambua kama inawasilisha ujumbe wa mwandishi asilia au iliathiriwa na upendeleo alio nao mtafsiri. Tumeangalia iwapo kuna uandishi upya katika Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilit*) inayotokana na upendeleo wa mtafsiri.

Lefevere (1992) anaonyesha kuwa itikadi huwa kizuizi kikuu katika kazi ya kutafsiri. Itikadi si iliyoko kwenye ulingo wa kisiasa pekee bali pia inayohusiana na imani inayoathiri vitendo vyetu. Uandishi upya kulingana naye hutokana na hali zifuatazo tatu:

- i) Welewa wa mtafsiri: Uandishi upya hutokana na hisia binafsi za mtafsiri kutokana na namna alivyoisoma na kuelewa M.A. Kila mtu ana namna ya kibinafsi kuhusiana na jinsi anavyoelewa mambo. Hii hupelekea kazi tafsiri iandikwe upya na mtafsiri.
- ii) Udhibiti wa mteja: Kazi inayotafsiriwa huweza kudhibitiwa na mtu mwingine, vikundi vya watu, dini, siasa, wachapishaji, vyombo vya habari k.v magazeti n.k. Kipengele cha udhibiti husukuma watafsiri kuzalisha M.P inayoafikiana na itikadi ya wateja wao. Kutokana na matakwa hayo, mtafsiri huishia kuandika upya kazi tafsiri ili ilingane na maelekezo ya mteja wake. Kwa mfano, ikiwa mtafsiri anafanya kazi chini ya shirika fulani la uchapishaji, atalazimika kutafsiri kulingana na maelekezo ya mwajiri wake. Hapa, mtafsiri hataruhusiwa jinsi apendavyo, ila ni kulingana na matakwa ya mwajiri wake. Kwa hali kama hii, M.P itakuwa ni uandishi upya wa M.A. Iwapo mteja analenga kumvutia mnunuzi, atataka kazi hiyo itafsiriwe kwa jinsi ya kumvutia mnunuzi au kama analenga wasomaji wa umri fulani, atataka

kazi hiyo itafsiriwe kwa namna itakayomfaa msomaji huyo. Katika tafsiri hii, mtafsiri labda atalazimika kukwepa tafsiri kwa kutumia mbinu ya neno kwa neno na badala yake kutumia tafsiri ya kimawasiliano ili kukimu mahitaji ya mteja.

- iii) Masharti kutoka kwa H.P: Ikiwa kazi tafsiri inalenga jamii fulani na asasi athirifu, mtafsiri atalazimika kuandika upya M.A ili kukubaliana na wanajamii pamoja na itikadi zao. Iwapo H.P ina imani fulani kuhusu wahusika au kile kinachozungumziwa kwenye M.A, itabidi mtafsiri kuandika upya M.P ili kupendelea H.P na kukuza hadhi yao kama wanajamii husika, na kuipatia umaarufu kazi tafsiri hiyo miongoni mwa wanajamii hao.

Biblia ya Kikalenjin ni maandiko matakatifu na kwa hivyo H.P ni Wakristo. Watafsiri pia wanadhibitiwa na wateja ambao ni waajiri wao- Muungano wa Biblia nchini Kenya (The Bible League Society of Kenya). Kazi yao inafaa kuafiki ile ya M.A kwa asilimia moja. Jambo ambalo utafiti huu umeegemea na kubaini mtafsiri aliandika upya M.P ambayo ni Biblia ya Kikalenjin, kulingana na kwamba haingewezekana kuwasilisha kutafsiri Biblia ya Kikalenjin moja kwa moja bila kuandika upya ili kuafiki utamaduni wa H.P na semantiki ya L.P.

Shuping (2013) anakubaliana na Lefevere kuhusiana na kuwepo kwa uandishi upya katika fasihi anaposema kuwa tafsiri hutekelezwa chini ya masharti fulani kwa makusudi fulani. Kando na yale masharti aliyoyataja Lefevere (1992), yeye anaongezea masharti mengine mawili; yaani:

- i) Fasihi. Fasihi lazima iwe na dhamira, inayoambatana na mfumo wa kijamii ili kukubalika kama fasihi. Fasihi hubadilika kiwakati, na

uamilifu wake hubadilika pia. Hata hivyo, kila fasihi lazima ijiwasilishe kwa namna ambavyo itaeleweka kwa hadhira. Fasihi inayobadilika kiwakati kutokana na uandishi upya, hutoa maelekezo kuhusu ni upi uandishi upya unaofaa kwa wakati maalum.

- ii) Diskosi jumuisi: Haya yanahusu mambo fulani yasiyokubalika katika tamaduni husika. Kila jamii huwa na imani tofauti na hivyo tafsiri ya neno kwa neno haiwi mwafaka wakati wote. Mtafsiri basi atalazimika kuamua jinsi na kiwango cha kutafsiri. Mtafsiri atapima kile kilicho asilia na diskosi jumuisi inayokubalika na kufahamika kwa mtafsiri na H.P. Hivyo ataamua kiwango cha uandishi upya akizingatia mtindo na ujumbe wa mwandishi wa M.A. Vilevile ni bayana kuwa utamaduni wenye hadhi ya chini hukubali tafsiri yenye kuegemea utamaduni wa hadhi ya juu. Kwa mfano, katika hali hii, lugha ya Kiswahili ni ya hadhi ya juu kushinda Kikalenjin kwa sababu Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi humu nchini. Hii ina maana kuwa mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin labda aliegemea utamaduni wa Waswahili kwa sababu ya hadhi yake. Ukweli huu ulibainika katika utafiti huu.

Utafiti huu umetekelezwa ili kuchunguza namna hali hizi zilivyoathiri mtafsiri na kumsababisha aandike upya Biblia ya Kikalenjin. Katika kuchunguza mikakati iliyotumika katika kutafsiri, tutaweza kubaini ikiwa mtafsiri aliathiriwa na hali hizi hivi kwamba alilazimika kuandika upya Biblia ya Kikalenjin na hata kuhakikisha kuwa M.P inakuwa mashuhuri miongoni mwa Wakalenjin.

2.3 Tafsiri na Utamaduni

Utamaduni ni mchanganyiko wa kaida za jamii, elimu, sanaa, sheria, itikadi na tabia anazozipokea mwanajamii (Katan 1999). Utamaduni hubadilika kiwakati. Kadri muda

unavyopita ndivyo dhana ya utamaduni inavyobadilika ubongoni mwa binadamu. Mwanzoni, utamaduni ulikuwa sahili; yaani jinsi maisha yalivyoendelea kisanaa, kielimu na kadhalika. Lakini wakati maana ya pili kuhusu maisha ya watu ilipojumuishwa kwenye ufafanuzi wa utamaduni, hapo ndipo tamaduni nyingine zilipotengwa, nyingine zikawa bora na nyingine dhaifu. Kadri maendeleo ya kisosholojia na stadi za kitamaduni yalivyozi, ndipo maana ya tatu ya utamaduni ikawa inahusiana na uwezo wa jamii na itikadi. Utamaduni hupatikana katika lugha. Mtafsiri anapotafsiri, atajikuta akihamisha vipengele vya kitamaduni vya L.A hadi kwa L.P kwa sababu hivi viwili havitenganishwi. Matini ya lugha pokezi bila shaka itakuwa na elementi za kitamaduni za L.A na kuifanya matini hii kuwa na tamaduni mbili iliyochanganyikana, yaani utamaduni wa L.A na wa L.P.

Utamaduni ni hali ya maisha ya mtu katika jamii; iwe ni dini, tabia, mfumo wa elimu na vilevile familia. Inavyoishi jamii moja na kuchukulia maisha, huenda ikawa tofauti kabisa na jamii nyingine (Al Hassan 2013). Kwa kuwa tafsiri huhusu lugha mbili na tamaduni mbili kama anavyodai Toury (1995), basi inakuwa ni bayana kuwa mtafsiri hawezi kutenganisha tafsiri na utamaduni. Pym (2000:2) anaunga mkono dai kuwa tafsiri ni kitendo chakitamaduni kwa kusema kuwa:

Kuangalia tafsiri ni kama kujihusha moja kwa moja na uhusiano baina ya tamaduni (FY).

Mtafsiri anapotafsiri, hulazimika kuzingatia na kukabiliana na tamaduni hizi mbili kwa kutekeleza yale aliyoyapendekeza Al-Hassan (2013), yaani:

- i) Kukuza utamaduni wa hadhira asilia
- ii) Kubadilisha utamaduni asilia
- iii) Kuchanganya (i) na (ii).

Hivyo kulingana na Al-Hassan, hali ya pili ndiyo huitwa tafsiri ya utamaduni ila watafsiri huchanganya zote mbili. Katika utafiti huu, tunanua kuchunguza jinsi watafsiri wa Biblia ya Kikalenjin walivyoishughulikia matini tafsiri kwa kuwa hadhira asilia na pokezi zina tamaduni tofauti na kuwa watafsiri walikusudia kuifikia hadhira pokezi kwa namna ya uwazi na yenye kueleweka barabara.

Al-Hassan (2013) ameziainisha matini za kifasihi kuwa mbili kuu. Kwanza ni matini ya kisayansi. Hii aliiainisha kama matini yenye utamaduni jumuishii, ambapo kwayo, mtafsiri huitafsiri pweke bila kuzingatia tamaduni mahsusi ila anazingatia tu yaliyomo anapotafsiri bila kuzingatia muktadha wa kitamaduni. Katika kutafsiri matini aina hii, muktadha wa hadhira pokezi na hadhira asilia huchukuliwa kuwa sawa.

Aina ya pili ni ile aliyoiita tafsiri ya kibiashara au matangazo. Aina hii huhusu utamaduni mahsusi na kwa kawaida, haiwezekani kuitafsiri. Badala yake, huandikwa upya katika lugha ngeni ili iweze kufidia tamaduni za lugha ngeni au pokezi. Biblia huweza kuainishwa kama matini ya kisayansi kwa kuwa ni matini yenye hadhira kubwa sana duniani na hadhira hii, huwa na tamaduni mbalimbali. Utafiti wetu ulichunguza jinsi mtafsiri alivyomudu kutafsiri matini hii kwani utamaduni wa Wakalenjin ni tofauti na wa Waswahili. Isitoshe, ilichunguza jinsi tofauti za kitamaduni zilivyosababisha uandishi upya kwa Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilit*).

Lugha na utamaduni ni vipengele viwili vinavyoingiliana. Wakati wa kutafsiri, mara nyingi lugha pokezi huweza kubadilika kutokana na ongezeko la vipengele vya kitamaduni kutoka kwa M.A. Matokeo yake ni M.P yenye mchanganyiko wa utamaduni wa M.A na M.P. Isitoshe, mtafsiri hutafsiri ujumbe pamoja na mtindo wa M.A na kuzalisha matini iliyoandikwa upya. Polepole, vipengele hivi vya kigeni

huunganishwa na L.P pamoja na utamaduni pokezi na matokeo yake ni mchanganyiko wa vipengele vya M.A na M.P.

Utamaduni ni kipengele muhimu sana katika tafsiri. Mtafsiri anastahili kumudu tamaduni asilia na pokezi ili kufanikisha azma kuu ya tafsiri ya kuimarisha isimu na utamaduni wa L.P. Kwenye utafiti wake kuhusu changamoto zinazosababishwa na tofauti za kitamaduni, Guerra (2012) alibaini kuwa wakati wowote ambapo tamaduni mbili zinakabiliana, inakuwa vigumu sana kwa mtafsiri kufanikisha uhamisho wa maana ili kufaulu katika jukumu lake la kuwasiliana na hadhira pokezi. Newmark (1988) alibaini hali hii katika utafiti wake wa awali ambapo aliainisha matatizo haya ya kitamaduni kama yafuatayo:

Kwanza ni tofauti za kiekolojia. Ekolojia kwa mujibu wa mtaalamu huyu inahusu tofauti inayotokana na mazingira kama mimea, wanyama, hali ya anga n.k. Ikiwa jamii mbili husika zinapatikana katika mazingira mbali kimasafa, kutakuwa na uwezekano kuwa wanajamii hao watakuwa na welewa tofauti kuhusu ekolojia yao. Hii ina maana kuwa, mtafsiri atakuwa na kazi nzito ya kujaribu kusawiri mazingira yaliyozungumziwa na mwandishi wa matini asilia kwa namna itakayopelekea M.P kuwa na uhalisia kwa hadhira pokezi. Kile kinachopatikana katika mazingira ya wanajamii moja huweza kukosekana katika mazingira ya wanajamii wengine. Kwa mfano, wanyama wanaofugwa na Wakalenjin huweza kuwa tofauti na wanaofugwa na Waswahili. Isitoshe, sababu za kuwafuga mifugo hao huwa tofauti kati ya wanajamii. Hali hii huzua changamoto kwa watafsiri.

Jambo la pili ni nyenzo za kitamaduni. Hili linahusu mavazi ya wanajamii, vyakula, majina ya miji n.k. Kawaida, mavazi ya Waswahili na Wakalenjin pamoja na vyakula vyao ni tofauti kabisa. Mtafsiri akizingatia tofauti hizi, huweza kujikuta kuwa anapata

changamoto kwenye tafsiri yake. Majina ya watu na miji huwa pia changamoto kwa kuwa licha ya mtafsiri kutaka kuzingatia sintakasia ya L.P, ana jukumu la kuhakikisha kuwa hapotezi maana na dhana iliyozingatiwa na L.A katika kutumia majina husika.

Mwisho ni tabia ya wanajamii. Hii inahusu jinsi wanavyoishi, shughuli zao za kujipatia riziki na namna ya kustaarabu kwao. Vilevile kuna miundo ya imani ya wanajamii, mifanyiko ya kisiasa na mamlaka. Utafiti huu ulichunguza matini ya kidini ili kubaini iwapo mtafsiri alikumbwa na changamoto hizi alizozitaja Newmark na kuonyesha namna alivyokabiliana nazo katika tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin.

Tafsiri sio kubadilisha maana wala kubadilisha msimbo bali ni kusafirisha maana kutoka L.A hadi L.P (Snell-Hornby, 1989). Kazi ya mtafsiri ni kuwezesha uhamishaji wa maana na vipengele vya kitamaduni kutoka lugha moja hadi nyingine huku akihakikisha kuwa athari sawa na ile iliyopokewa na hadhira asilia inapitishwa kwa hadhira pokezi. Ujumbe uliopo kwenye L.A kwa kweli huwa umefumwa kwenye muktadha wa kitamaduni na inafaa kuhamishwa hadi kwa L.P (Nida, 1964). Uhamishaji huu unapotekelezwa, ni jukumu la mtafsiri kuhakikisha kuwa ujumbe unahifadhiwa lakini kwa kuegemea muktadha na utamaduni wa L.P.

Newmark (1988) na Agar (1994) katika fafanuzi zao, wanadai kuwa utamaduni ni maisha na mambo ya muhimu na ya pekee katika jamii husika inayotumia lugha kama njia ya kujieleza, na kuifanya jamii hiyo kujihisi kuwa tofauti. Larson (1984) anaona kuwa utamaduni ni mchanganyiko wa imani mielekeo, kaida na maadili ambayo wanakikundi hushiriki kwayo. Upekee wa Wakalenjin hutokana na lugha yao ambapo mtafsiri anastahili kutilia maanani ili kuhakikisha kuwa anakuza vipengele vya kitamaduni kama wanavyodai Newmark (1988), Agar (1994) na Larson (1984). Katika Biblia ya Kikalenjin, lugha inayotumika ni lugha inayostahili kuwasiliana na

wanajamii ambao wanajitambulisha na lugha yao ya Kikalenjin, kwa hiyo, utamaduni wao lazima uwepo ili mawasiliano yakamilike. Utafiti huu ulichunguza mawazo ya wataalamu hawa yalivyozingatiwa na mtafsiri ili kuhakikisha kuwa utamaduni wa Wakalenjin unazingatiwa katika kupitisha ujumbe wa M.A hadi kwa H.P hata kama kutakuwa na uandishi upya kwenye matini pokezi.

Alvarez na Vidal (1996) wanaeleza kuwa tafsiri hudhihirisha uwezo wa utamaduni mmoja dhidi ya mwingine. Tafsiri si kuzalisha matini inayolingana na nyingine bali ni mchakato changamano wa kuandika upya matini pokezi iliyosambamba na matini asilia na yenye athari zake tofauti na za matini asilia. Utafiti hata hivyo hautaweza kubaini athari ya matini pokezi kwa wasomaji wake, lakini uchunguzi huu uliazimia kuangalia vipengele ambavyo vinaaminika kuchangia kwa matini kuwa ni uandishi upya wala si tafsiri.

Kila jamii huwa na namna ambavyo huitazama dunia yake. Katika juhudi ya kuunganisha thamani ya lugha na utamaduni, tafsiri wakati wote hujaribu kusawazisha tamaduni tofauti ili kufikia kiwango kinachoeleweka kwa msomaji wa tafsiri (Lefevere, 1999). Hivyo basi, tafsiri hailingani na matini asilia sawa na anavyosema Bassnett (1980) kuwa: matini tafsiri ni tofauti sana na matini asilia na hivyo inafaa kuchukuliwa kama matini ya kipekee. Kama huu utachukuliwa kama ukweli, basi itakuwa dhahiri kuwa kamwe hakuna kazi tafsiri. Tunavyojua ni kuwa Biblia ya Kikalenjin ni tafsiri kutoka kwa Biblia ya Kiswahili. Vipi basi tutaiita uandishi upya wala si tafsiri? Matokeo ya utafiti huu yataweza kutupa mwanga kuhusiana na madai ya Bassnett. Mtafsiri ana kibarua kigumu katikakutoa tafsiri kwa kuwa changamoto ya tofauti za kitamaduni ni dhana nzima yenye vizingiti vyake. Tuliangalia jinsi mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin alivyofaulu katika utafsiri wake.

Hongwei (1999) anatoa maoni yake kuhusu utamaduni kwa kudahili kuwa lugha hutumika kuchora taswira ya utamaduni wa jamii husika. Kulingana naye, lugha ina umuhimu mkubwa ikilinganishwa na vipengele vingine vya kitamaduni kwa kuwa hufanya kazi ya kueneza, kukuza na kuimarisha vipengele vile vingine vya kitamaduni. Dai hili linaelekea kuunga mkono maoni yake Sapir (1949) katika tasnifu yake ya *Language Race and Culture*, ambapo anabaini kuwa lugha haiwi ila kutokana na utamaduni. Hata hivyo, Newmark (1988) anaonekana kupinga Hongwei na Sapir kuhusiana na wazo hili kuwa lugha ni kipengele cha utamaduni, kwa kudai kuwa ingekuwa hivyo, tafsiri kamwe haingewezekana. Lakini tunaona tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin inawezekana kwa kuwa lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii.

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa vipengele vya kitamaduni vilitafsiriwa kupitia lugha ya H.P. Ili mawasiliano haya yakamilike, mtafsiri alilazimika kuwasilisha vipengele vya kitamaduni kuptia lugha ya walengwa, na kisha kuiandika upya M.P ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa katika M.A. Hii ina maana kuwa utamaduni na lugha haviwezi kutenganishwa.

Kuhusu uhusiano wa lugha na utamaduni, Kramsch (1998) anaona lugha kama mfumo wa ishara yenye maadili ya kitamaduni. Wazungumzaji hutambulisha utamaduni wao kwa wenzao kupitia lugha. Huona lugha yao kama ishara ya kujitambulisha kijamii, na kutotumia lugha huchukuliwa na wazungumzaji kama uasi dhidi ya wanajamii na utamaduni wao. Hii ndiyo sababu lugha ni kitambulisho cha jamii. Nida (1964) anadahili kwamba tofauti baina ya tamaduni husababisha changamoto kubwa kwa mtafsiri kuliko ilivyo tofauti za kimuundo. Katika utafiti huu, tulinuia kuchunguza mikakati inayotumiwa na mtafsiri katika tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil* ili kukabiliana na chngamoto hizi. Halafu tukabaini jinsi mikakati hii inavyopelekea uandishi upya wa Bibilia ya Kikalenjin.

Tafsiri nzuri ni ile inayotimiza makusudi sawa katika L.P kama ilivyo katika L.A. Lazima M.P ionekane kama kazi asilia. Ni sharti kazi tafsiri ionyeshe uhalisia wa L.A katika L.P kwa kuzingatia mtindo wa L.A na kuwa na athari ileile kwa H.P. Suluhisho la mambo haya ni kiwango cha usambamba wa ulinganifu. Nida (1964) akizungumzia kuhusu jinsi ya kukabiliana na dhana za kitamaduni endapo kisawe hakipatikani, anapendekeza kuwa mtafsiri huweza kutumia faharasa na tanbihi ili kuelezea dhana za kitamaduni kwa uwazi. Katika utafiti wetu, tulijishughulisha na kuchunguza jinsi mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin alivyokabiliana na tafsiri ya dhana za kitamaduni.

Salehi (2012) andai kuwa matini hufasiriwa sio kwenye ombwe tupu bali kwa kugemea kaida za jamii husika ambamo wanajamii huzifafanulia tabia zao na za wenzao. Kaida za kitamaduni huzua changamoto kwa watafsiri na hivyo kuwalazimu kufahamu kwanza tamaduni pokezi kando na tamaduni asilia. Lazima pia atumie mikakati bora zaidi ili kuletea athari sawa. Athari ya kazi tafsiri iliyofaulu ni ile yenye kufanana kwa wasomaji wa L.P kama ilivyo kwa wasomaji wa L.A (Munday, 2001). Kama alivyopendekeza Munday kuhusu matumizi ya mikakati bora katika tafsiri, utafiti wetu ulibaini mikakati hiyo, na kisha kutambua iwapo kulikuwa na uandishi upya wa Biblia ya Kikalenjin katika harakati ya kutafsiri. Isitoshe, tulichunguza jinsi mtafsiri alivyozingatia kaida za tamaduni za Wakalenjin katika tafsiri yake kama anavyodai Salehi.

Kuhusu mwingiliano wa tafsiri na utamaduni, House (2009) anasema kuwa tafsiri sio tu tendo la kiisimu bali pia la kitamaduni; ni kitendo cha kuwasiliana baina ya tamaduni. Tafsiri kwa kawaida huhusu lugha na tamaduni kwa kuwa haviwezi kutenganishwa. Lugha imo ndani ya utamaduni, kwa kuwa hueleweka zaidi inapoelezwa ndani ya utamaduni. Mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin anapotafsiri,

hutumia lugha ya Kikalenjin kudhihirisha utamaduni wa Kikalenjin. Utafiti huu ulichunguza ufanisi wa mtafsiri katika utekelezaji huu.

Baker (1992) anaelezea kuwa neno katika L.A huweza kuwasilisha dhana iliyo tofauti kabisa katika utamaduni wa L.P. Kwa mfano, mambo yanayohusu dini na imani, itikadi na aina ya vyakula na mengine, hukosa visawe katika lugha nyingi. Mtafsiri huweza kusuluhisha tatizo hili kwa kutumia neno lenye kusababisha athari sawa kwa H.P sawa na ilivyo kwa H.A. Hapo, M.P itaonekana ikiwa sawa na M.A. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mikakati iliyotumika katika uteuzi na mpangilio wa maneno katika *Bukuit Ne Tilil*, na kuangalia iwapo uteuzi huo unaleta athari sawa na ile ya Biblia Takatifu. Athari sawa inapopatikana katika ujumbe uliotafsiriwa, husababisha matini hiyo iwe tafsiri ya kuaminika. Dhana ya uaminifu imechambuliwa kwa kina na Shitemi (1997). Akitafiti kuhusu dhana hii ya uaminifu katika tafsiri ya mashairi ya kale, anadahili kuwa ukosefu wa habari za kimsingi kwa mtafsiri, huweza kuchangia kuwepo kwa pengo linaloathiri utimizaji wa tafsiri. Hasa pale ambapo tamaduni na mazingira yanayorejelewa hayana uhusiano wowote wa kiisimu, kimazingira na kitamaduni na ile ya matini pokezi.

Katika utafiti wake Sun (2011), alibaini kuwa kuwepo kwa angalau uwiano wa kiasi fulani kati ya tamaduni, huchangia katika kuwezekana kwa tafsiri baina ya tamaduni. Utamaduni wa Wakalenjin na wa Waswahili huenda ukawa na uwiano wa kiwango fulani, uliosababisha kuwezekana kwa mawasiliano, la sivyoy, tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin haingewezekana. Waswahili na Wakalenjin ni watu wanaoshi katika taifa moja, chini ya utawala mmoja na siasa sawa, ingawa wametengana kimasafa. Uwiano huu wa utaifa unaosababisha mazingira sawa ya kisiasa, ndio Sun anadai kuwa humwezesha mtafsiri kufanikisha kazi yake.

Utamaduni vilevile, kama anavyoshikilia Sun (2011) ni kwamba huweza kuwa na maadili yasiyokubaliana kuhusu dhana fulani. Kwa mfano, katika jamii ya Waswahili, paka huweza kuhusishwa na bahati mbaya, huku Wakalenjini wakimchukulia paka tu kama mnyama anayehusishwa na utulivu. Katika kutafsiri dhana za kitamaduni, mtafsiri huenda akajikuta akirejelea dhana ileile kwa namna tofauti na ilivyokusudiwa na mwandishi wa M.A. Upotovu huu huchangia mara nyingi kwa M.P kuandikwa upya, na kuonekana kama ni matini tofauti na ile ya awali. Utafiti wetu ulichunguza jinsi dhana ya utamaduni ilivyoshughulikiwa na mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilit*. Vilevile, kutathmini namna alivyoikabili ili kuhakikisha kuwa tafsiri hiyo inafaulu kupitisha ujumbe uliomo kwenye Biblia Takatifu.

2.4 Mikakati ya Kutafsiri

Kulingana na Wolfgang (1991), mikakati ya kutafsiri ni namna ya kufikia suluhu ya shida ya kutafsiri. Mbinu zilizopendekezwa na watafsiri wa Biblia kama Nida, Tabor na Margot na wengine, ilinua kupendekeza baadhi ya suluhisho ya kutafsiri. Mikakati kama hii hata hivyo imeonekana kulenga matokeo ya tafsiri tu bali haishughulikii mikakati na kufikia tafsiri linganifu. Krings (1986) anashadidia ufafanuzi huu kwa kusema kuwa mikakati ya kutafsiri ni mipango ya kimakusudi ambapo mtafsiri anatekeleza ili kukabiliana na matatizo yanayotokana na kutafsiri. Mikakati hii hata hivyo, kama anavyodahili Kelly (1979), huwa ndani mwa mtafsiri (labda ubongoni mwake) na hutumika kutokana na msukumo uliomo ndani mwa mtafsiri pindi inapohitajika. Kwangu, mikakati ya kutafsiri ni njia inayofuatwa ili kutekeleza tafsiri.

Venuti (1998) anaonyesha mikakati ya kutafsiri kama kazi ya kimsingi ya kuchagua matini ngeni ya kuitafsiri na kisha kutafuta mbinu za kutumia kutafsiri. Graedler (2010) kwa upande wake, anapendekeza kuwa wakati wa kukabiliana na elementi za kitamaduni katika tafsiri, mtafsiri anastahili kuzingatia mikakati ifuatayo:

- i) Kuunda neno jipya ili kutafsiri dhana fulani ya kitamaduni
- ii) Kufafanua maana ya neno katika M.A kwa kutolea maelezo kutegemea fasiri ya mtafsiri
- iii) Kuacha M.A jinsi ilivyo
- iv) Kubadilisha M.A kwa kutumia istilahi yoyote ya L.P inayohusiana na maana ya M.A

Harvey (2012) naye anapendekeza njia nne ya kutekeleza tafsiri:

- i) Ulinganifu wa kiuamilifu: kutumia dhana inayolingana na matumizi ya dhana ya M.A
- ii) Ulinganifu wa kiisimu: ni sawa na kutafsiri M.A neno kwa neno
- iii) Kukopesha dhana katika lugha nyingine ili kutafsiri M.A
- iv) Kufafanua dhana ya M.A katika L.P kwa namna sahili kwa ajili ya welewa wa H.P

Baker (1992) anaeleza mikakati ya kutafsiri kama mbinu inayotumika kutafsiri kutokana na sababu kuwa lugha mbili tofauti hukosa visawe vyenye kuleta ulinganifu katika tafsiri. Ili kukabiliana na changamoto hii, Baker anapendekeza mikakati ifuatayo wakati wa kutafsiri maneno:

- i) Kutafsiri kwa kutumia maneno yenye maana jumuishi. K.m badala ya kutafsiri 'chamcha', mtafsiri huweza kutumia 'chakula' kwa kuwa ni neno jumlishi wala haibaini wakati maalum wa kukila chakula hicho.
- ii) Kutafsiri kwa kutumia neno lisilo na dhana jumuishi (bila maelezo mengi). K.m badala ya kutafsiri neno 'nyumbani', neno lenye maelezo jumuishi 'makaazi' litumike. Iwapo mtafsiri angependa kueleza mengi kuhusiana na neno hili, basi maelezo yake kwenye tanbihi.

- iii) Kutafsiri kwa kutumia vibadala vya kitamaduni. Hapa mtafsiri anapokosa neno linalofaa kutafsiri dhana fulani katika tamaduni ya L.A, basi atatumia neno lingine katika L.P lenye athari sawa. K.m ‘cream tea’ kule Uingereza, litatafsiriwa kama ‘pastry’ kwa Waitaliano kwa kuwa kwao hili neno lina dhana sawa na lile la Waingereza.
- iv) Kutafsiri kwa kukopesha maneno, ambapo neno linaporudiwa rudiwa, maelezo yake hutolewa kisha mtafsiri atakuwa na uhuru wa kulirudia rudia hilo neno kwa kuwa tayari linaeleweka kwa H.P.
- v) Kutafsiri kwa kutumia fasiri ya neno linalohusiana kimaana k.m katika lugha ya Kiingereza, maneno ‘overlooking’ hutafsiriwa kama ‘which overlooks’ na neno ‘related’ litatafsiriwa kama ‘kinship relation’ na kadhalika.
- vi) Kutafsiri kwa kutoa fasili; kwa kutumia maneno yasiyohusiana. Mfano katika Kiingereza, neno ‘accessible’ hutafsiriwa kwa maneno ya fasili kama ‘where human beings enter mostly’. Tafsiri kama hii hutoa maelezo kwa kina kulingana na welewa wa mtafsiri na kwa kutumia maneno yake mwenyewe.
- vii) Kutafsiri kwa kuacha maneno au sehemu ya M.A. Iwapo kile kinachofafanuliwa si muhimu sana kwa ujenzi wa matini, au labda kuchosha msomaji kutokana na maelezo mengi, basi mtafsiri anaweza kupuuza hayo maneno au maelezo na kufupisha sehemu hiyo.
- viii) Kutafsiri kwa kutumia kielelezo. Kielelezo ni muhimu iwapo neno limekosa kisawe mwafaka katika L.P. Tafsiri kama hii vilevile inafaa pale ambapo M.T inastahili kuelezwa kwa kifupi na ufasaha ilhali hamna nafasi ya kutosha, basi mtafsiri atatumia kielelezo kwa kuwa

huweza kupitisha ujumbe mpana na wenye maelezo mengi lakini kwa njia rahisi na fupi mno.

Guerra (2012) vilevile katika utafiti wake, alibaini kuwa matatizo na changamoto za kutafsiri ni nyingi ila tu mtafsiri anapotumia mikakati mbalimbali humwezesha kukabiliana nazo. Baadhi ya mikakati anayopendekeza ni kama ifuatayo;

2.4.1 Utohozi wa kimuktadha

Mkakati huu hutumika wakati hali inayoashiriwa na ujumbe kwa L.A haibainiki kwa H.P na mtafsiri akaumba hali ngeni inayoelezewa kama hali linganifu. Hivyo inaweza kulinganishwa na kile waandishi wengine wamekiita ulinganifu wa kiuamilifu. Yaani ni kujaliza kipengele cha utamaduni wa lugha moja na nyingine kutoka jamii husika. Mkakati huu wa kutafsiri ni muhimu katika tafsiri za matangazo au hadithi za watoto; mengine ni vipimo vya mizani, muziki, anwani katika kazi za fasihi au hata majina ya kijiografia na mengineyo. Azma ya mtafsiri anapotumia mkakati huu ni kurekebisha tafsiri ili kuwa na athari sawa kwa wasomaji wa M.L.

2.4.2 Ukopajiwa msamiati

Mkakati huu unahusu kuchukua neno au kijelezi moja kwa moja kutoka lugha asilia bila kutafsiri. Mkakati huu kwa kawaida hutumika wakati istilahi husika imekosa kabisa kisawe chake katika tamaduni lengwa au iwapo mtafsiri anajaribu kupata athari ya mtindo wa M.A. maneno yaliyokopwa huonekana kama halisia hasa iwapo mwendelezo wake unaafikiana na L.P na pengine mofolojia na fonetiki yake imeongezwa, mfano: skirt- skati, computer- kompyuta na mengine. Guerra (2012) anaongezea kwa kusema kuwa, kukopesha huku ni njia kuu ya kuitajirisha L.P kimsamiati. Ijapokuwa kukopa msamiati kwa wingi kutaifanya L.L kuonekana kama L.A wala si kazi iliyotafsiriwa.

2.4.3 Uradidi wa maneno

Ni mkakati wa kutafsiri leksia au muundo wa neno geni. Mtafsiri hapa huazima maelezo ya L.A au miundo yake kisha kusafirisha moja kwa moja hadi lugha pokezi. Tofauti ya kukopesha na uradidi ni kuwa katika kukopesha mofolojia na fonetiki ya neno au kishazi geni huigwa, huku uradidi ukiwa kusafirisha au kunakili namna ya mofolojia na umuhimu wa istilahi wala si katika kulitamka. Uradidi ni tafsiri sahihi na pia hufuata kanuni za kimofolojia na kifonetiki za maneno au vishazi vigeni huku kukopesha, huzingatia mofolojia na umuhimu wa dhana wala si matamshi yake.

2.4.4 Ufidiaji wa maneno

Mkakati huu unahusiana na hali kwamba neno lililoachwa katika M.A hufidiwa na lingine la L.P lenye madhara tofauti na ya M.A, mtafsiri anaweza kufanya hivi akiwa na sababu ya kusawazisha maneno, pale ambapo yale yanayopotezwa kisemantiki (ama athari za ujumbe au mtindo) hufidiwa kupitia misingi ya elementi za L.A ama athari za kimtindo kwenye matini ya L.P kwa sababu elementi hizo haziwezi zikafanana na zile za L.A kwa asilia mia moja. Hii ni kama vile tafsiri ya lafudhi, kejeli, upole na mengine.

2.4.5 Udondoshwaji wa maneno

Huu ni mkakati ambapo mtafsiri baada ya kuiangalia na kuchunguza kwa makini kazi ya kutafsiri, huweza kuondoa ujumbe au neno fulani la M.A katika M.P, hasa iwapo ujumbe wenyewe unaonekana kutobeba umuhimu au uzito mwingi, na kwamba dhana hiyo inapotafsiriwa huweza kumsababisha mpokezi au msomaji wa M.L kuelewa au kutenda vinginevyo. Mkakati huu si mashuhuri wakati wa kutafsiri tamaduni, na inapotokea, mara nyingi huwa ni kwa makusudi ya kukwepa uradidi au utohalisia.

2.4.6 Ufafanuzi wa istilahi

Mkakati huu huhakikisha istilahi au kijezezi kinatafsiriwa kwa kutumia ufafanuzi wa umbo au uamilifu wake. Kwa mfano, neno ‘supper’ linaweza kutafsiriwa kwa kufafanua kuwa ‘chakula cha jioni’. Hivyo, huweza kuchukuliwa kama namna ya kufafanua dhana kwa kutolea maelezo au mifano ili ipate kueleweka zaidi kwa H.P.

2.4.7 Ulinganisho wa kimaana

Katika mkakati huu, mtindo tofauti kabisa hutumika katika kuelezea hali ileile moja, au huweza kutumia maumbo tofauti kuzalisha matini linganifu. Hii ina maana kuwa mtafsiri hutumia istilahi au kijezezi kinachojulikana katika L.P kama ulinganifu wake. Ni sawa na kubadili na kurekebisha kwa kuwa hueleza hali sawa kwa kutumia njia tofauti. Hasa katika semi na lugha yenye fomula k.v ‘amani ya Bwana’, inapotafsiriwa kama ‘shalom’, na ‘Lamb of God’, inapotafsiriwa kama ‘Mwana wa Mungu na kadhalika.

2.4.8 Upanuzi wa ujumbe wa L.A

Upanuzu ni hali ambapo mtafsiri anawasilisha kitu au jambo katika L.P kwa uwazi zaidi akitumia muktadha wa L.A, au kwa kuongeza maelezo ya kindani zaidi kuliko yale ya L.A kwa kutolea habari zaidi. Ufafanuzi wa mtafsiri au maelezo yake katika L.P hutumia maneno mengi kuliko yale ya L.A kueleza hali ileile moja. Tafsiri hii husababisha M.P iwe kubwa zaidi kushinda M.A. Ukubwa huu hata hivyo haibadilishi ujumbe kwa namna yoyote.

2.4.9 Ujumuishaji wa dhana katika L.P

Mkakati huu wa ujumuishaji ni kinyume cha ubainifu, ambapo mtafsiri hutumia maneno ya kijumla zaidi au istilahi isiyo mahsusi kutafsiri dhana za M.A. Kwa mfano, neno ‘chai’ linaweza kutafsiriwa kwa kutumia neno jumlishi kama ‘kinywaji’.

Hali hii husababishwa na tofauti za kimtindo kati ya L.A na L.P. Ingawaje, mtafsiri huweza kutumia mkakati huu ili kukwepa uradidi usiofaa kwenye tafsiri yake.

2.4.10 Tafsiri ya moja kwa moja

Tafsiri ya neno kwa neno hutokea wakati neno au kishazi cha L.A kinatafsiriwa hadi neno au kishazi cha L.P, bila kujali mtindo, ila kuna kubadili matini kwa kaida za kisintaksia za L.P pamoja na marekebisho machache mno hivi kwamba huonekana kama sahihi. Ni uhamisho wa moja kwa moja wa M.L.A hadi kwa sarufi ya M.L.P ambapo kazi ya mtafsiri inapunguzwa hadi kufikia kufuata kanuni za kiisimu za lugha husika (yaani L.P) mf. John loves Mary, kwa maana ya, Yohana anampenda Maria. Ambapo kiambishi /m/ kimetumika kama kirejeshi cha Maria.

2.4.11 Urekebishaji wa maelezo

Mkakati huu huhusu matumizi ya kishazi cha L.P kilicho tofauti na kile cha L.A kuwasilisha jambo lile lile. Yaani, kuna mabadiliko kimaoni, kifalsafa au kategoria ya wazo ikilinganishwa na L.A. Ni sawa na uhamishaji na wakati mwingine ni muhimu ili kukwepa ukosefu wa mtiririko katika tafsiri.

2.4.12 Ubainishaji wa hali maalum

Ni kinyume cha ujumlishaji, ambapo ubainishaji wa hali maalum hutokea wakati mtafsiri anatumia hiponimia ya L.A au istilahi bainifu ambayo itatoa utata na kubainisha hasa kuhusu hali ya jinsia kwa mfano, iwapo mtu anayezungumziwa ni wa kike au kiume. Ili kutafsiri dhana kama vile 'she' na 'he' ya Kiingereza hadi Kiswahili, itabidi kubainisha kwa lugha ya Kiswahili kwa vile lugha ya Kiswahili haini visawe vya moja kwa moja ya dhana hizo.

2.4.13 Matumizi ya vibadala

Katika mkakati huu, elementi za lugha ishara kama vile kiimbo au ishara za mwili, hutumika badala ya elementi za kiisimu. Kwa mfano, badala ya kutafsiri neno la Kiingereza ‘wave’ kwa kutumia visawe vya maneno katika lugha ya Kiswahili, mtafsiri atatumia ishara za mwili kwa kuchora mkono wa mtu unaoonekana ukipunga hewani tubila kutumia maneno yoyote. Ishara hii huweza kutafsiriwa kwa Kiswahili kama ‘aga kwaheri’ na ikabeba maana sawa kabisa na ishara yenyewe.

2.4.14 Uhamishaji wa maana

Ni mkakati wa kubadilisha sarufi au kubadilisha sehemu moja ya sarufi ya L.A na nyingine ya L.P, bila kubadilisha maana ya ujumbe. Mfano;

L.A: *This computer is out of order*

L.P: Hii kompyuta haifanyi kazi

Katika mfano huu, mpangilio wa maneno kuanzia katikati ya sentensi ni tofauti katika L.P lakini ujumbe ni uleule. Uhamishaji wa kisarufi, pamoja na marekebisho ya kimofolojia na kisintaksia ni mwafaka sana ili kupata tafsiri inayoonekana kama M.A (iliyoandikwa kwa mara ya kwanza) inaposomwa na H.P. Uhalisi huu wa matini tafsiri huondoa ugeni katika M.P.

2.3.15 Ubainishaji wa sajili

Mkatati huu humgharimu mtafsiri kubadilisha elementi inayoathiri vipengele vingi vinavyohusiana na vibainishi vya kiisimu. Tofauti zinazotokana na toni, mtindo, lahaja za kijamii na kijiografia, ambapo rejista iliyotumika katika L.P hufanywa kuwa tofauti kabisa na ya L.A katika tafsiri.

Utafiti huu ulichanganua mikakati iliyotumiwa na mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin umetekelezwa, pamoja na kuchunguza namna alivyofaulu katika kutumia mikakati

hiyo. Tumeangalia kama mikakati niliyojadili hapo juu imetumika na kwa kiwango gani. Vilevile, hapa chini, tulibaini iwapo mapendekezo yaliyotolewa na mwanaisimu Leppihame (1997) yalizingatiwa na mtafsiri; kwamba ili kutafsiri vishazi kuu, mtafsiri atakuwa na jukumu la:

- i) Kutumia tafsiri sanifu
- ii) Kufanya mabadiliko ya kiwango cha chini kama katika tafsiri ya neno kwa neno
- iii) Kutumia maelezo zaidi kwenye M.P
- iv) Kutumia tanbihi, faharasa na maelezo ya mtafsiri
- v) Kutoa maelezo kwa kutumia hali inayoshabihiana na ile ya M.A
- vi) Kubadilisha M.A kwa kutumia vijelezi vya L.P
- vii) Kufafanua kwa kutumia L.P ili ipate kueleweka zaidi kwa H.P
- viii) Kuumba upya aya kwa kutumia maelezo yenye fununu za L.A
- ix) Kuondoa kabisa sehemu zinazoweza kupelekea M.P kuwa na utata

Kati ya mikakati hii iliyopendekezwa na Leppihalme (1997), Ordudari (2007) anaonekana kupendelea mkakati wa kutumia tanbihi. Anasema mkakati huu huipa H.P nafasi nzuri ya kuelewa M.T kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa M.A. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mikakati iliyotumika katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin (M.A) kutoka lugha ya Kiswahili (L.A). Aidha nilibaini umaarufu wa mikakati maalum inayoonekana kufanikisha tasfiri ya Bibilia ya Kikalenjin.

2.5 Mbinu za Kutafsiri

Mbinu za kutafsiri ni njia au mwelekeo anaouchukua mtafsiri ili kupata M.P kutokana na M.A. Mbinu anazochagua mtafsiri katika kutafsiri matini yoyote ile, husababisha afikie matini pokezi yenye ubora mwingi wa kupitisha ujumbe wa mwandishi asilia.

Lakini kabla ya kuanza kuchagua mbinu za kutafsiri, kuna mambo muhimu ambayo mtafsiri anafaa kuzingatia. Guo (1999), anapendekeza kuwa, kabla ya mtafsiri kuchagua mbinu mwafaka katika kufanya tafsiri, anastahili kujiuliza maswali yafuatayo:

- i) Je, nia au makusudi ya tafsiri yake ni nini?
- ii) Ni aina gani ya matini anayotarajia kuitafsiri?
- iii) Wasomaji (H.P) wa matini tafsiri ni nani?

Mengine ni hali ya uchumi, siasa, mwelekeo wa mtafsiri kuhusiana na utamaduni wa M.A na M.P na kadhalika. Sababu kuu ya kujiuliza haya maswali ni kwa kuwa, uteuzi wa mbinu za kutafsiri huzingatia mambo yafuatayo:

- i) Makusudi ya mtafsiri: Mtafsiri anapotafsiri, huwa na lengo mahsusi, k.v kupitisha ujumbe wa M.A hadi kwa M.P, kupitisha tamaduni za hadhira ya M.A kwa hadhira ya M.P, kuburudisha n.k. Iwapo hadhira itapokea kile alichonuia mtafsiri, basi mtafsiri atakuwa amefikia lengo lake. Kwa mfano, lengo la kutafsiri Biblia ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin ni ili Wakalenjin wapate ujumbe wa wokovu na kushawishika kuwa Wakristo. Hii ina maana kuwa iwapo Wakalenjin watasoma Biblia na kujiunga na dini ya Ukristo, basi mtafsiri atakuwa amefanikisha lengo lake.
- ii) Wasomaji: Mtafsiri huwa na wasomaji lengwa hata kabla ya kuanza kutafsiri. Hii ina maana kuwa mtafsiri lazima azingatie wahusika anaowalenga. K.m ikiwa ni watoto wachanga atatumia mbinu tafsiri maalum yenye kuwawezesha watoto kumwelewa

kinyume na ilivyo watu wazima. Hii ina maana kuwa mbinu ya kutafsiri lazima iafikiane na hadhira inayolengwa na mtafsiri.

- iii) Matini inayotafsiriwa: Aina ya matini inayotarajiwa kutafsiriwa hutegemea dhima zake. Yaani kueleza, kufahamisha na kupitisha ujumbe mahsusi kwa wasomaji. Mara nyingi kama ni matini ya kimatibabu mtafsiri anaweza kutohoa majina ya dawa hasa kama neno hilo halijabeba dhana yenye maana nzito.
- iv) Mwelekeo wa mtafsiri kuhusu utamaduni asilia na pokezi: Tamaduni nyingine huweza kuwa na hadhi kushinda nyingine. Hali hii husababisha watafsiri wa lugha ya hadhi kuhamisha vipengele vya utamaduni wa lugha hiyo hadi kwa L.P. Hii ina maana kuwa iwapo lugha iliyotumika kuandika M.A ni ya lugha yenye hadhi ya juu, basi vipengele vyake vya kitamaduni vitapatikana katika kazi tafsiri. Katika utafiti wetu, Kiswahili, ambayo ni lugha ya M.A ina hadhi ya juu (kwa sababu ni lugha ya taifa na pia ni lugha rasmi). Tunatarajia kupata vipengele vya utamaduni wa Waswahili katika M.L ambayo Bibilia ya Kikalenjin.

Nida (1988) anaendelea kusema kuwa tafsiri hutekelezwa akilini mwa binadamu. Hivyo tofauti za kibinafsi hufanya kazi tafsiri kuwa ya kipekee. Isitoshe, kuna baadhi ya changamoto ambazo hukumba mtafsiri nazo ni:

- i) Namna anavyomudu lugha pokezi
- ii) Mtagusano wake na lugha asilia
- iii) Mfumo wa mawasiliano
- iv) Utaratibu unaotumiwa katika tafsiri

- v) Upuuzaji wa mtafsiri kutokana na imani kuwa mtafsiriwa anajua kile kilichotafsiriwa.

Changamoto hizi huishia kwa mtafsiri yeyote yule kuzalisha kazi pokezi tofauti kwa kiasi fulani na kazi asilia, yaani kuandika upya M.P. Haya yanasababisha Traore (2005) kusema kuwa hakuna tafsiri ya asili mia moja. Mtafsiri anapokumbwa na changamoto hizi huweza kukosa kufikia malengo yake ya kuwasilisha ujumbe wa mwandishi asilia. Vipengele hivi alivyotaja Nida vinahakikisha kuwa mtafsiri anafanya uteuzi mwafaka wa maneno, misamiati, misemo, vitendawili n.k kulingana na mfumo wa lugha husika. Mwisho kazi hiyo inawasilishwa kwa msomaji kwa njia mwafaka na kubalifu. Utafiti huu ulichunguza kipengele cha kukamilika kwa mawasiliano, ili kubaini kufaulu kwa mtafsiri katika kazi yake ya kutafsiri Biblia ya Kikalenjin.

Mtaalamu Newmark (1988) ameeleza tofauti baina ya mbinu za kutafsiri na mikakati ya kutafsiri kwa kusema kuwa, huku mbinu za kutafsiri zikihusu matini nzima, mikakati ya kutafsiri huhusu matumizi ya sentensi na vipande vidogovidogo vya lugha. Mbinu alizoainisha ni pamoja na:

- i) Tafsiri ya neno kwa neno: Katika mbinu hii, neno katika L.A hutafsiriwa likiwa pweke pweke. Matokeo ya tafsiri hii huwa ni matini iliyoko nje ya muktadha.
- ii) Tafsiri sisisi: Huhusisha sarufi ya L.A inayobadilishwa hadi ikalingana na L.P. Tatizo hapo ni kuwa maneno ya kileksia hutafsiriwa pweke pweke nje ya muktadha.

- iii) Tafsiri aminifu: Tafsiri hii hujaribu kuwasilisha maana asilia kimuktadha kwa kufuata muundo wa sarufi katika sarufi ya L.P. Tafsiri kama hii hupelekea M.P kuwa ya kukubalika zaidi kwa H.P, kwa kuwa ule ugeni unafichwa kabisa.
- iv) Tafsiri ya kisemantiki: Hii tafsiri ni sawa na ilivyo katika tafsiri aminifu, ila tafsiri hii hujaribu kukuza thamani na urembo wa M.A. Mtafsiri, kwa kuwa ana haja ya kuwasiliana na H.P kwa namna rahisi iwezekanavyo, basi itabidi arahisishe tafsiri yake kwa vyovyote vile ili aweze kuwasiliana na H.P. Matini hiyo basi itakuwa ya kueleweka na huwa mbinu bora zaidi kutafsiri. Mwansoko (1996:25) anaongeza kwa kusema kuwa tafsiri hii huweka mkazo kwenye maana ya matini kama ilivyokusudiwa na mtafsiri. Mwansoka anaongeza kuwa faida ya tafsiri hii ni kwamba huingiza miundo ya misemo kutoka L.A na hivyo kuendeleza L.P.
- v) Tafsiri ya kiutohozi: Hii ni tafsiri huru zaidi na mara nyingi hutumika katika kutafsiri ushairi, maudhui, wahusika na ploti ili kukuza utamaduni wa L.A ambao hubadilishwa na ule wa L.P kisha matini kuandikwa upya.
- vi) Tafsiri kimisemo: Huzalisha ujumbe asilia ila hujaribu maana ndogondogo katika M.A kwa sababu ya kutumia misemo na nahau mahali ambapo vipengele hivi havipatikani, katika M.P.
- vii) Tafsiri kimawasiliano: Tafsiri hii huwasilisha maana kamili kimuktadha ya M.A kwa namna ambavyo ujumbe na lugha hukubalika na kueleweka kwa wasomaji. Mwansoko (1996) anaelezea zaidi kuhusu mbinu hii kwa kudai kuwa ni mbinu inayolenga H.P; kwamba mtafsiri yu huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya L.P. Mbinu hii hufuata pia sarufi ya L.P, ni lazima vilevile ifuate mwelekeo wake wa kijamii, kihistoria, kiutamaduni na kimazingira.

Kulingana na Holz-Manttari katika Oduori (2008), tafsiri inahusu uhamishaji baina ya tamaduni tofauti na katika uhamishaji huu, anazingatia au kuibua dhana ya kupitisha ujumbe. Ujumbe unaweza kupitishwa kimaandishi ukiambatana na matumizi ya picha na michoro mbalimbali. Ujumbe pia hupitishwa kupitia mbinu mbalimbali za kutafsiri ili kumfikia msomaji. Kufaulu au kutofaulu kwa mawasiliano haya kutategemea mbinu alizochagua mwandishi wa matini pokezi. Utafiti huu utachunguza mbinu zilizochaguliwa na mtafsiri ili kuifikia hadhira yake. Tulichunguza iwapo mbinu zilizochaguliwa na mwandishi asilia zinapelekea kuwa na uandishi upya wa matini tafsiri.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa mtafsiri anafaa kuzingatia mbinu mwafaka katika kutafsiri kazi yoyote ile ili kufanikiwa. Utafiti wetu ulichunguza mbinu za tafsiri zilizofanikisha tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil*.

2.6 Misingi ya Nadharia

Kulingana na Kerlinger (1973), nadharia hutumika kutoa maelezo na hata kumulika mbele kuhusu dhana fulani zinazoweza kuchunguzwa katika utafiti. Orodho (2009), anadai kuwa nadharia humwongoza mtafiti katika utafiti wake huku ikionyesha mianya ya utafiti au hata sehemu ambayo utafiti unaweza kujiegemeza.

Kwa mujibu wa Malangwa (2010) katika nadharia yake ya mtambuko mawazo, anapendekeza kuwa uchanganuzi wa kazi tafsiri hauwezi kufanyika kwa kutumia nadharia moja tu, kwa sababu hakuna nadharia inayojitosheleza yenyewe. Utafiti huu ulizingatia madai haya na hivyo kuongozwa na nadharia mbili. Kwanza ni, nadharia ya Tafsiri Vitendo. Nadharia hii iliasisiwa na Justa Holz-Manttari katika miaka ya themanini. Nadharia yake ilionekana kupendelea hadhira pokezi, kwani anapendekeza kuwa mtafsiri anafaa ajiulize iwapo yaliyomo kwenye M.A yanaafiki matakwa ya


H.P. Nadharia hii huona tafsiri kama inayochochewa na nia pamoja na matokeo yanayopatikana baina ya wanadamu huku msisitizo ukiwa kwenye mchakato mzima wa tafsiri kama njia ya kuwasilisha ujumbe au vitendo vya kutafsiri kutoka matini asilia hadi matini pokezi. Vilevile, kuchukulia tafsirikama mchakato wa kimawasiliano unaohusu wahusika wenye dhima mbalimbali. Wahusika hawa ni mwandishi wa matini asilia, mtafsiri na mpokezi au msomaji wa matini tafsiri.

Kutokana na maelezo haya, tulitumia nadharia hii ili kuchunguza mbinu za tafsiri alizotumia mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil*, na iwapo ziliwezesha mawasiliano yakamilike baina ya hadhira pokezi na mwandishi wa matini asilia, kupitia kwa tafsiri. Aidha mbinu mwafaka inapokosa kutumika katika tafsiri, kazi tafsiri inaishia kuwa uandishi upya wala si tafsiri tena. Wakati mtafsiri anakuwa ndiye mwandishi wa matini asilia, dhima anayokusudia itekelezwe na kazi yake hufanikiwa kwa kuwa ataweza kuwasilisha maudhui yake kwa namna anavyoikusudia, kinyume na ilivyo ikiwa mwandishi wa matini ni tofauti na mtafsiri. Mwandishi wa Biblia ya Kiswahili siye anayeitafsiri katika lugha ya Kikalenjin yaani mwandishi wa *Bukuit Ne Tilil*. Hali hii inasababisha mtafsiri kutafsiri kutokana na welewa wake wa matini asilia; ambao huenda ikawa tofauti na alivyokusudia mwandishi wa Biblia Takatifu.

Nadharia hii vilevile inasisitiza uzalishaji wa matini pokezi kama mawasiliano amilifu kwa wasomaji. Yaani umbo na aina ya matini pokezi, kwa mfano, lazima iongozwe na kile kilicho amilifu katika utamaduni wa hadhira pokezi. Hali hii huamuliwa na mtafsiri ambaye ana ujuzi katika kitendo cha kutafsiri na ambaye dhima yake ni kuhakikisha kuwa uhawilishaji wa utamaduni wa hadhira asilia unafikia hadhira pokezi kwa kiwango sawa. Utafiti huu ulichunguza M.P, yaani, *Bukuit Ne Tilil* iwapo ilifaulu katika kupitisha vipengele vya utamaduni kwa wasomaji wake kadri inavyokubalika katika jamii hiyo huku ikikuza ujumbe wa mwandishi asilia.

Mtafsiri katika kutekeleza kazi yake hawezi akajitenga na utamaduni wake na ule wa hadhira pokezi. Ili aweze kufikia hadhira yake, ni lazima awe anaelewa utamaduni wao ili awasilishe vipengele muhimu vinavyojenga ujumbe wa matini asilia. Wakati mwingine, mandhari ya mwandishi wa matini asilia huweza kutofautiana na ya mtafsiri; vilevile tofauti kati ya vipindi vya uandishi huweza kuchangia uandishi upya katika tafsiri. Hali hii ilichunguzwa katika utafiti huu.

Nord (2007) anaunga mkono nadharia hii kwa kusema kuwa, kutafsiri ni kitendo kinachokusudiwa; ni tabia inayofafanuliwa vyema katika mchoro uliopo ukurasa wa **57**. Ambapo tafsiri hubainika kama kipatanishi baina ya tamaduni tofauti ili kukamilisha mawasiliano.



Picha 1: Mchakato wa tafsiri: (umeasisiwa na Nord 2007)

Kulingana na mchoro wa Nord (ukurasa 57) kuhusu nadharia ya tafsiri vitendo, ni kuwa tabia au mwenendo wa mtu kama anavyotarajia mwandishi wa matini asilia utaweza kubadilika kupitia kutagusana naye. Mtagusano huu unafaa kuwa kati ya watu wawili. Mtagusano huu hata hivyo, huimarishwa na kuwepo kwa mawasiliano. Kitendo cha kutafsiri huwezesha mawasiliano yawepo kati ya watu wawili wenye tamaduni tofauti. Mwandishi wa matini asilia anapoandika kazi yake, ananua kuwasiliana na watu fulani wanaoelewana kwa kuwa wanatumia lugha moja na utamaduni wao ni mmoja. Lakini iwapo pana hitaji la kuwafikia watu wenye tamaduni tofauti, itabidi tafsiri ifanyike, ama kwa kuandika au kuzungumza. Utafiti huu uliangalia kazi iliyotafsiriwa kwa kutumia maandishi.

Nadharia hii inazidi kufafanua kuwa, endapo utamaduni wa mwandishi asilia hauafikiani na utamaduni wa hadhira lengwa, basi hana budi ila kutumia mpatanishi atakayemuunganisha na hadhira yake. Katika matini andishi, mpatanishi huyu ni mtafsiri atakayetekeleza kitendo cha kutafsiri kazi ile kwa kutumia lugha ya hadhira lengwa. Katika muktadha wa utafiti huu, lugha ya hadhira lengwa ni lugha ya Kikalenjin. Kupitia lugha ya Kikalenjin, wasomaji wasioelewa lugha ya Kiswahili watakaposoma Biblia kwa lugha yao ya mama, wataelewa ujumbe ule kwa kuwa lugha ni nyenzo ya kupitisha utamaduni. Watapata kujumuika katika utamaduni wao ambao umejikita katika lugha yao, na hivyo kukamilisha mawasiliano. Utafiti huu ulichunguza jinsi uandishi upya ulivyoathiri tafsiri kwa kuifanya ama ieleweke au kukosa kueleweka kwa H.P ambayo ni ya jamii ya Wakalenjin.

Nadharia ya pili iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya ulinganifu. Nadharia hii iliasisiwa na Nida na Taber katika mwaka wa 1982. Wataalamu hawa waliainisha nadharia hii kama ulinganifu rasmi na ulinganifu sambamba. Ulinganifu rasmi huzingatia ujumbe wenyewe katika umbo lake na ujumbe ulioko kwenye matini. Kwa

upande mwingine, ulinganifu sambamba, unazingatia kanuni na athari ya ulinganifu kwenye matini. Wataalamu hawa wanonekana kupendelea ulinganifu sambamba ambao ulitumika kwenye uchanganuzi wa utafiti huu. Ulinganifu rasmi kama anavyodai Fawcett (1997) husababisha ujumbe wa mwandishi kutoeleweka kwa msomaji wa matini pokezi. Huku Nida na Taber (1982) wakidahili kuwa upungufu ulioko kwenye nadharia hii ya ulinganifu rasmi ni kuwa, sarufi ya lugha asilia na ya lugha pokezi zinapolinganishwa wakati wa kutafsiri, huathiri ujumbe. Yaani, vipengele muhimu huachwa kwa kuvilinganisha moja kwa moja. Isitoshe, mtaalamu Carsons (1993) alitoa mapendekezo yake kuwa ulinganifu sambamba au amilifu ni bora zaidi katika kutekeleza kazi yoyote ya tafsiri. Utafiti huu ulichota kutoka kwa ulinganifu sambamba kwa kuwa nadharia hii humpa mtafsiri uhuru wa kujieleza kwa L.P. Hii itapelekea matini ya L.P kuwa mwafaka kwa H.P. Uhuru huu ndiyo inayosababisha mtafsiri kuandika upya M.P na kuweza kuwasiliana na hadhira pokezi. Nadharia hii ilibainika katika uchanganuzi wa *Bukuit Ne Tilit*.

Nadharia ya ulinganifu sambamba inafafanuliwa kama kanuni ya tafsiri. Mtafsiri hujaribu kutafsiri maana asilia kwa namna ambayo maneno ya lugha pokezi yatachochea athari sawa kwa hadhira pokezi kama ilivyo katika hadhira asilia. Nida na Tiber (1982), wanaendelea kudai kuwa mara nyingi, umbo la matini asilia hubadilika katika tafsiri lakini huhifadhi uaminifu wake. Utafiti huu uliangazia kipengele cha umbo kwa kuangalia sarufi ya Kikalenjin inavyobadilika na kuweza kuhifadhi uaminifu wa ujumbe wake. Kinachosisitizwa na wataalamu hawa ni kuhakikisha kuwa ujumbe unahifadhiwa katika matini pokezi.

Baadaye nadharia hii ya ulinganifu sambamba iliimarishwa na kuitwa ulinganifu wa kiuamilifu (De Waard na Nida, 1986). Kulingana na Nida (1964), lengo la kutafsiri ni kuzalisha ujumbe linganifu; yaani wenye sifa sawa kabisa na mawasiliano asilia.

Kwa hivyo tafsiri ni kuzalisha katika lugha lengwa, ulinganifu uliokaribiana sana na ujumbe wa lugha asilia; kwanza kimaana na pili ni kimtindo. Kwa hivyo ulinganifu sambamba husababisha athari fulani kwa wasomaji. Nida na Taber (1969:12) wanasema:

Ulinganifu sambamba unafaa kufafanuliwa kutegemea kiwango ambacho wapokezi wanavyopokea ujumbe huo ikilinganishwa na upokeaji wa ujumbe huo baina ya hadhira asilia. Upokeaji huu kamwe hauwi sawa kwa sababu utamaduni na mandhari ya kihistoria ni tofauti, lakini sharti pawe na kiwango cha juu cha ulinganifu wa mapokezi. La sivyo, tafsiri hiyo itakosa kukamilisha madhumuni yake.

Kulingana na maelezo yao, ni bayana kuwa mandhari na utamaduni kati ya lugha ya Kikalenjin na Kiswahili si sawa. Hata hivyo, wataalamu hawa wanapendekeza kuwa hali hii iweze kukwepwa na mtafsiri na kufanya kazi yake tafsiri ilingane na ile asilia. Kukwepa huku ndiko kunakosababisha mtafsiri kuandika upya matini lengwa ili kuleta uhalisia wa M.P.

Nadharia hii ya Nida na Taber iliungwa mkono na Eco (2001) kwa kudai kuwa mtafsiri hatafsiri matini kwa kujiegemeza kwenye fafanuzi za kamusi ila kwa misingi ya historia ya matini hizo mbili. Kwa hivyo, tafsiri haihusiani tu na umilisi wa kiisimu bali katika saikolojia ya umatini na umilisi wa kiusimulizi. Mtafsiri analazimika kila mara anapotafsiri kupiga hatua zaidi ya isimu ya lugha na utamaduni. Hii ina maana kuwa tafsiri haihusu ulinganisho kati ya lugha mbili ila ufasiri wa matini mbili katika lugha mbili tofauti. Ili tafsiri iwe hai, mtafsiri mzuri lazima azalishe athari iliyokusudiwa na matini asilia. Utafiti huu uliangazia athari za ujumbe uliomo katika M.P huku ukilinganishwa na athari zilizopo katika M.A.

Eco (2001) alibaini kuwa hamna lugha mbili zinazoweza kufanana kimaana kwa kuwa kila lugha ina fonolojia yake maalum, sarufi, msamiati au hata dhana mbalimbali za kitamaduni. Kulingana na hali hii, lazima patatokea kiwango fulani cha

upotoshaji au kudhoofika kwa maana ya ujumbe uliotafsiriwa. Tultumia kipengele hiki katika utafiti wetu kuchunguza mikakati aliyoitumia mtafsiri wakati wa kuchagua sarufi, msamiati na uteuzi wa maneno katika kuhakikisha kuwa hapotezi wala kudhoofika kwa ujumbe wa mwandishi wa M.A ili athari ya ujumbe wake iwe sawa na ilivyokuwa katika matini asilia. Tulichunguza mikakati iliyotumika kwa jumla katika utafsiri wa *Bukuit ne Tilit*.

Baker (1992) akizungumzia nadharia ya ulinganifu, aliangazia viwango mbalimbali vinavyogusia vipengele tofauti tofauti vya ulinganifu. Kwanza, ni ulinganifu wa kiwango cha maneno, ambapo anadai kuwa ni muhimu sana kwa mtafsiri, kwani mtafsiri anapoanza kazi yake, huangazia maneno ili kupata ulinganisho wa moja kwa moja katika lugha pokezi. Lugha mbalimbali huweza kuwa na neno lenye maana zaidi ya moja; kwa hivyo ni jukumu la mtafsiri kubaini maana ya neno husika.

Kiwango cha pili ni cha ulinganifu wa kisarufi. Baker aligundua kuwa kaida za kisarufi huweza kuwa tofauti kutoka lugha moja hadi nyingine, na hivyo, kuzua matatizo ya kupata ulinganisho unaofaa katika lugha pokezi. Maumbo ya kisarufi kwa kweli huweza kuzua tofauti katika ujumbe na kubadilisha ujumbe katika lugha pokezi. Mabadiliko haya husababisha mtafsiri ama kuongeza au kuondoa ujumbe katika lugha pokezi kwa kukosa zana za kisarufi kama vile njeo, idadi, uana na hali miongoni mwa mengine.

Kiwango cha tatu ni ulinganifu wa matini katika kiwango cha mshikamano wa ujumbe. Kuwepo kwa mshikamano na muwala wa ujumbe unaowasilishwa kwa hadhira pokezi kutasababisha kukamilika kwa mawasiliano. Maelezo mazuri ya matini asilia humwezesha mtafsiri kujenga muwala na mshikamano katika kazi yake. Ni jukumu la mtafsiri kuamua iwapo atadumisha mshikamano na muwala wa matini

asilia. Uamuzi wake utaongozwa na vipengele vitatu anuwai; yaani hadhira pokezi, lengo la tafsiri na aina ya matini.

Kiwango cha mwisho ni ulinganifu wa kipramantiki kwa kurejelea kiashiria na mikakati ya kile kisichostahili kukwepwa na mtafsiri wakati wa kutafsiri. Kiashiria ni kile kinachosemwa waziwazi wala si kile kinachoashiriwa. Katika tafsiri, mtafsiri anahitajika kutafuta maana inayoashiriwa ili kufaulu kupitisha ujumbe katika matini pokezi. Jukumu la mtafsiri ni kuumba upya makusudi ya mwandishi wa matini asilia katika utamaduni mwingine kwa namna ambavyo inaeleweka vyema na wasomaji wenye utamaduni mwingine tofauti na wa mwandishi asilia.

Vipengele vya ulinganifu vilivyoangaziwa na Baker vinajenga nadharia hii ya ulinganifu sambamba. Katika utafiti huu tulizingatia vipengele hivi katika uchanganuzi wa matini pokezi. Tuliwezesha na nadharia hii kubaini namna viwango hivi vilivyozingatiwa katika kutafsiri Biblia ya Kiswahili hadi *Bukuit Ne Tilil* ya Kikalenjini, ili kuibuka na matini ulinganifu kwa mujibu wa nadharia hii.

Utafiti huu vilevile ulifaidi kutokana na nadharia ya tafsiri vitendo. Nadharia hii ilitumika hasa katika kutathmini mbinu za tafsiri zilizotumika kutafsiri Biblia ya Kikalenjini; kwa kuwa mbinu hizi ndizo zinazochangia uhifadhi wa ujumbe wa matini asilia. Kwa upande mwingine, nadharia ya ulinganifu ambayo mtafiti alitumia katika kuchunguza ulinganifu wa tamaduni, mtindo na miundo ya matini asilia na matini pokezi kisha kutathmini uandishi upya ulivyobainika katika ulinganifu huu. Kijumla, nadharia hizi mbili zilioanishwa ili kutumika katika uchanganuzi wa data zilizotumika katika kutekeleza lengo la utafiti huu. Aidha, faida na dosari za nadharia hizi zilitathminiwa mwishoni mwa uchunguzi huu.

2.7 Hitimisho

Sura hii imetathmini kazi zilizotokana na wataalamu mbalimbali walioangazia mada hii ya utafiti, aidha, maoni na mapendekezo yao yalitufaa katika kutupa mwanga na mwelekeo wa utafiti wetu. Vipengele vilivyoshughulikiwa kwa undani ni pamoja na tafsiri ya vipengele vya utamaduni, mikakati ya kutafsiri na mbinu za kutafsiri matini tofautitofauti. Misingi ya kinadharia imefafanuliwa kwa kina katika sura hii. Nadharia mbili kuu, yaani, nadharia ya tafsiri vitendo na nadharia ya ulinganifu sambamba zilijadiliwa na kuonyeshwa jinsi zilivyomuhimu katika uchunguzi huu. Msingi wa nadharia hizi ndio uliofuatwa kwenye utafiti huu ili kuletea matokeo yaliyopatikana na kufafanuliwa katika sura ya mwisho ya kazi hii.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI NA UCHANGANUZI WA DATA

3.0 Utangulizi

Sura hii kwa muhtasari imeangazia mpango mzima uliyofuata katika kuendeleza utafiti huu. Aghalabu, jinsi sampuli iliyotumika katika utafiti ilivyofikiwa. Sura vilevile inaeleza jinsi utafiti mwigo ulivyotekelezwa na mtafiti kabla ya kufanya utafiti huu. Data ilivyokusanywa na mtafiti pamoja na vifaa vilivyofaa kwenye utafiti huu. Data zilizokusanywa kutokana na utafiti huu zilionyeshwa jinsi zilivyonukuliwa wakati wa kusoma M.A na M.P. Baadaye, uchanganuzi wa data unaonyeshwa vile ulivyotekelezwa.

3.1 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza uandishi upya katika tafsiri za matini ya dini ya Kikristo. Matini iliyochanganuliwa ni Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilit*) iliyotafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiswahili. Biblia ya Kiswahili iliandikwa na wamishenari baaada ya kuzuru Afrika Mashariki kwa lengo la kusambaza imani ya Kikristo katika bara la Afrika lililoaminika kuwa gizani; hawakumtambua Mungu. Baadaye, kwa sababu ya kuwafikia makabila mbalimbali ya Afrika Mashariki, ndipo Biblia hiyo ikatafsiriwa hadi lugha ya Kikalenjin. Isitoshe, watafsiri wa Biblia hii ni watu tofauti na mwandishi wa matini asilia. Biblia ya Kiswahili iliandikwa na kisha baadaye ikaja kutafsiriwa kwa lugha za kienyeji. Hii ina maanakuwa matini hizi mbili zinatofautiana kiwakati. Vilevile, utamaduni wa mwandishi wa M.A na wasomaji wa M.P ni tofauti na hali kama hizi huweza kusababisha kuwepo kwa uandishi upya wa matini pokezi wakati wa kutafsiri. Uchunguzi huu umejikita katika matini ya Biblia za Kiswahili na Kikalenjin. Uchanganuzi huu basi uliegemea tu kwenye matini hizi mbili pekee.

Kwenye utafiti maktabani, vitabu, majarida, maensaiklopedia na maandishi mbalimbali yalisomwa ili kupata habari muhimu kuhusu masuala kama vilemandhari, utamaduni, mbinu za kutafsiri na mengine mengi yaliyoafiki utafiti huu. Vilevile, kazi nyingine za maandishi mbalimbali zilisomwa ili kubaini matokeo ya tafiti zao zilizoweza kulinganishwa na utafiti huu pamoja na mbinu walizozitumia kufanikisha tafiti zao. Pamoja na hayo, mtafiti alidurusu mtandao ili kuelewa zaidi kuhusu utafsiri wa Biblia ya Kikalenjin, miktadha na mazingira ya uandishi wake. Biblia za lugha ya Kiswahili na Kikalenjin zilisomwa kwa undani ili kuelewa kazi tafsiri vyema. Aidha, tulipata kuifahamu zaidi nadharia ya ulinganifu ambayo iliongoza utafiti huu, kwa kuwa vipengele muhimu vilivyoangaziwa na nadharia hii vilichanganuliwa kwa minajili ya kufikia malengo ya utafiti.

Tahakiki zilizotumia nadharia ya ulinganifu sambamba na ile ya tafsiri vitendo zilisomwa na mtafiti ili kufahamumengi kuhusu namna nadharia zinavyoathiri tafsiri ya Biblia, hasa kutoka lugha moja hadi nyingine. Mtafiti aliangazia jinsi tafsiri ya Biblia ya Kiswahili na *Bukuit Ne Tilil* ilivyofanikishwa na watafsiri hao. Sababu zinazopelekea M.A na M.P kutofautiana huku ujumbe ukiwa umehifadhiwa.

Matini teule (Biblia za Kiswahili na Kikalenjin) na hasa kitabu kilichochanganuliwa (Mithali) vimerejelewa ili kupata data iliyotumika kuchunguza uandishi upya unavyobainika katika tafsiri ya *Bukuit NeTilil*. Data iliyoshughulikiwa ni ile ambayo ilituwezesha kutoa uamuzi kuhusu suala la uandishi upya katika tafsiri.

Isitoshe, wahusika kadha wa kadha wanaojihusisha na tafsiri ya Biblia katika Taasisi ya Tafsiri ya Biblia ya Kapsabet (Kapsabet Bible Translation and Literacy) pamoja na wenzao kutoka Shirika la Kutafsiri Bibilia la Kenya (Bible Translation Society of Kenya) walisaidia katika kutoa mwelekeouliokuwa na umuhimu mkubwa kwenye

uchunguzi huu, hasa katika kubaini jinsi *Bukuit Ne Tilil* ilivyotafsiriwa, na nani na kwa nini wakatafsiri kwa lugha ya Kikalenjin.

3.2 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni sehemu tu ya data inayotumika katika utafiti ili kuwakilisha hali ilivyo kijumla. Kulingana na Morse (1994), sampuli ya kimakusudi hutumika wakati wa kuteua sehemu ndogo ya data ili kuwakilisha sehemu nzima. Usampuli wa kimakusudi ulitumiwa na mtafiti katika kuchagua matini ya kuchanganua. Mtafiti alichagua kuchanganua matini ya kidini na vilevile kuchagua matini iliyotumia lugha ya Kiswahili kama M.A na iliyotafsiriwa hadi lugha ya Kikalenjin. Tuiteua kutafitia lugha hizi kwa sababu mtafiti ana umilisi katika lugha hizo; yaani Kikalenjin ikiwa ni lugha yake ya mama, huku Kiswahili kikiwa ni lugha ya kwanza na vilevile, lugha ya taifa na lugha rasmi nchini Kenya. Hivyo basi, mtafiti alikuwa na uwezo mkubwa wa kutekeleza utafiti wake kwa wepesi kwa kuwa alikuwa na umilisi katika lugha hizi mbili. Huu ulirahisisha uchanganuzi wa data katika utafiti wake.

Usampuli wa kimakusudi vilevile ulitumiwa kuteua Kitabu cha kuchunguzwa katika Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*). Ili kupata sampuli wakilishi ya matini iliyotafsiriwa ya Biblia ya Kikalenjin, tulitumia data kutoka kwa kitabu cha Mithali. Kitabu hiki kiliandikwa na mfalme Suleimani aliyeaminika kuwa na hekima kuliko wanadamu wote kwa wakati wake, maana alipewa hekima hiyo na Mungu (1 Wafalme 4:29-34). Kusudi la kukiteua kitabu hiki ni kutokana na kuwa na wingi wa methali, mifano na mafumbo. Uchambuzi huu ulituelekeza kubaini jinsi changamoto hizi za kutafsiri kitabu hiki zilizua uandishi upya katika *Bukuit Ne Tilil*; hasa katika kitabu hiki cha Mithali.

Kwa mujibu wa mtaalamu Kothari (2004), anapendekeza kuwa mtafiti anapochagua sampuli, anafaa kutilia maanani sababu hasa za kuteua sampuli yenyewe. Mtafiti hivyo, anapaswa kuteua sampuli itakayomwezesha kupata matokeo anayolenga. Kitabu hiki cha Mithali kilifaa zaidi katika kutupa matokeo yaliyotarajiwa kwa kuwa vifungu vyake vinakamilika kimaana pasipo kuhitaji msomaji kusoma vifungu kadhaa ili kuelewa mwandishi. Hili liliwezesha uchambuzi wa mstari baada ya nyingine. Hasa wakati wa kuchunguza mbinu za tafsiri zilizotumika.

Isitoshe, kitabu cha Mithali ni kimoja miongoni mwa vitabu sitini na sita katika Biblia. Ni kitabu chenye upekee wake kwa jinsi kilivyoandikwa; Mtiririko wake ni ule wa kiubeti; yaani kila kifungu kimeendelezwa kama ubeti. Kila ubeti; ambao huweza kuwa mstari mmoja au miwili, huwa umekamilika kimaana.

Umaarufu wa kitabu hiki miongoni mwa waumini ulichangia mtafiti kukitafitia. Kitabu cha Mithali kinapendwa sana na waumini na hata makasisi kwa kuwa kina mawaidha si haba. Kwa hivyo, kilifaa katika utafiti huu ili kuchunguza jinsi vifungu hivyo vilitafsiriwa. Sura zote zilisomwa na kisha vifungu vilivyoafiki malengo ya utafiti viliteuliwa ili kuchanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia tete maalum iliyochunguzwa katika utafiti. Kwa hivyo, ni kweli kuwa sura zote za kitabu hiki zilisomwa kwa undani ili kupata data iliyohitajika kwenye utafiti huu.

3.3 Utafiti Mwigo

Mtafiti kwanza alifanya utafiti mwigo kabla ya kuanza utafiti wenyewe. Ili kutekeleza utafiti huu, mtafiti alichagua baadhi ya vifungu vya Biblia huku akilinganisha na tafsiri yake. Katika kufanya hivi, mtafsiri aliweza kugundua mianya iliyopo kwenye tafsiri hiyo na kuona haja ya kugundua kile kilichosababisha kuwepo kwa upungufu huo.

Mtafiti alichagua vifungu kutoka agano la kale na agano jipya katika Biblia. Baada ya kufanya huo uteuzi, alilinganisha M.A na M.P ili kuchunguza iwapo kuna ulinganifu wa utamaduni, msamiati na pia sarufi baina ya lugha hizi mbili. Mtafiti aligundua kuwa tafsiri haikuwa ya moja kwa moja wala neno kwa neno. Maneno mengine yalitafsiriwa kwa namna ambayo ungedhani kuwa ni nenolenye maana tofauti kabisa. Kwa hivyo, mtafiti akawa na sababu ya kuendeleza uchunguzi huo kwa kutaka kujua mengi yanayojiri katika tafsiri ya Biblia.

Matini ya Biblia kwa Wakristo huaminika kuwa matini takatifu kutoka kwa Mungu mwenyewe. Mungu ndiye mwanzilishi wa matini hiyo na inapotafsiriwa inafaa kuhifadhiwa bila hata kupotosha ujumbe wenyewe. Mtafsiri alipokuwa anafanya utafiti mwigo, aligundua kuwa uandishi wa M.P ulitofautiana kwa kiasi fulani na M.A. Hasa, mambo yanayohusiana na vipengele alivyokusudia kutafitia. Hii ilimchochea mtafiti kuona haja ya kujikita kwenye matini hii kwenye utafiti wake.

Utafiti mwigo ulikuwa muhimu vilevile hasa wakati wa kuteua vifaa vya kukusanyia data. Mtafiti alipokumbana na changamoto katika utafiti mwigo, aliona uwezekano wa kupata data kwa kutumia vifaa vitakavyomwezesha kupata data kamilifu. Mtafiti pia alipata wazo la kuzuru ofisi inayojihusisha na kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha za kienyeji; hasa lugha ya Kikalenjin. Watafsiri hawa walihitajika ili kutoa mwanaga kuhusu changamoto zinazowakabili kwenye tafsiri na namna ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mbinu za kutumia kukusanya data ziliweza kuwa dhahiri kabisa baada ya kufanya utafiti mwigo. Mbinu zilizoonekana kuzalisha data muhimu katika utafiti zilitumika huku zingine zikitupiliwa mbali. Mtafiti kwa mfano alitupilia mbali matumizi ya

hojaji kwani aligundua kuwa usaili ungekuwa mwafaka na rahisi katika kukusanya data kamilifu zitakazokimu mahitaji ya utafiti.

Mtafiti aligundua kuwa angehitaji watu mbalimbali, hasa wazungumzaji lugha ya Kikalenjin na wenye mazoea ya kutumia *Bukuit Ne Tilil* katika ibada zao ili kumsaidia mtafiti endapo atakumbana na utata unaohusiana na lugha na Kikalenjin, msamiati wake, sarufi na utamaduni wa Wakalenjin. Watu hawa wanaweza pia kuwa si watu wanaotumia Biblia hii mara kwa mara lakini kwa kuwa wao ni wazungumzaji wa lugha ya Kikalenjin, wangeweza kutoa msaada wowote ule kwa mtafiti.

3.4 Ukusanyaji wa Data

Ili utafiti huu ufanikiwe, mtafiti alihitajika kukusanya data ambazo zilimsaidia katika uchanganuzi wake. Isitoshe, (Kombo na Tromp, 2006) wanasema kuwa data zinazokusanywa nyanjani ama huweza kudhibitisha au kupinga ukweli fulani na hivyo mtafiti anafaa kuwa makini katika kuteua vifaa vya kukusanya data yake. Kwa kuongozwa na mapendekezo yao Kombo na Tromp, mtafiti alitumia mbinu zifuatazo ili kupata data zilizohitajika kwenye utafiti huu.

3.4.1 Uchunguzi maktabani

Utafiti huu kwa jumla ulitekelezwa maktabani. Mtafiti alihitaji kuchukua muda kuketi maktabani ili asome matini asilia na matini pokezi. Kwa njia hii, aliweza kukusanya data mwafaka iliyohitajika kwa ajili ya utafiti huu. Nilipata data yangu kupitia kwa kusoma Biblia ya Kiswahili na *Bukuit Ne Tilil* ya Kikalenjin. Nilisoma sura zote thelethini na moja za kitabu cha Mithali. Sababu ya kukisoma kitabu kizima cha Mithali ni ili kodondoa sehemu mahsusi, hasa zilizoafikiana na nadharia tete za utafiti. Sehemu hizi zilinukuliwa kwenye daftari na kisha baadaye kuchanganuliwa,

huku sehemu ambazo hazikubeba umuhimu mkuu kulingana na nadharia tete hizo, zikiachwa katika uchanganuzi wangu.

3.4.2 Uchunguzi shirikishi

Mtafiti kwa kuwa anatoka katika jamii ya Wakalenjin na ana umilisi wa lugha ya Kikalenjin na Kiswahili, alitumia umilisi wake katika lugha hizi ili kupata na kuchanganua data iliyofaa utafiti huu. Umilisi huu ulikuwa wa manufaa katika kuchunguza kila kipengele kilichokuwa muhimu katika utafiti huu, kwa mujibu wa nadharia tete. Mtafiti alitumia umilisi wake katika kulinganisha data zilizohusu uteuzi wa msamiati mwafaka katika kutafsiri ili kuangalia iwapo ujumbe wa mwandishi wa M.A ulitafsiriwa kwa hali inayofikia H.P ipasavyo. Isitoshe, alichunguza vipengele vinavyohusu utamaduni wa Wakalenjin, ili kubaini iwapo vilitafsiriwa kwa njia inayoweza H.P kujumuika katika kuelewa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa M.A. Vilevile kubaini iwapo mbinu zilizotumika katika kutekeleza tafsiri hii zilifaulu katika kuwasiliana na H.P.

3.4.3 Usaili

Mtaalamu Orodho (2009) anadahili kuwa usaili ni njia ya kuuliza watafitiwa maswali kwa kuwapigia simu au kukutana nao ana kwa ana. Katika utafiti huu, nilizuru ofisi ya Tafsiri ya Biblia ya Kapsabet (Kapsabet Bible Translation and Literacy Office), ambapo nilikutana ana kwa ana na watafsiri katika ofisi hiyo. Niliwasaili ili kupata maelekezo kuhusu sababu za kutafsiri Biblia ya Kiswahili kwa lugha ya Kikalenjin. Wao walinieleza kuwa walitafsiri Biblia kwa lugha ya Kikalenjin ili kuwafikia Wakalenjin na Injili kupitia lugha wanayoifahamu vyema. Tafsiri hii pia ilichochea na kwamba katika miaka hiyo ya sitini, Wakalenjin wengi hawakuifahamu lugha ya Kiswahili.

Walinifahamisha kuwa waliohusika katika kutafsiri Biblia kwa lugha ya Kikalenjin ni Rev. Kipnyolei na Askofu Bryson. Aidha, wasailiwa hawa walichangia kwa kutoa maelezo hasa kuhusu changamoto zinazotokana na kutafsiri Biblia katika lugha za kienyeji, ikiwemo lugha ya Kikalenjin. Walisema kuwa tofauti za kitamaduni, kimazingira, itikadi na mila pamoja sarufi ya lugha hizi mbili hufanya kazi ya tafsiri kuwa ngumu.

Mbinu hii ya usaili katika kukusanya data ilinisaidia sana kupata habari muhimu na za ziada. Kama anavyoeleza Mugenda na Mugenda (2003), usaili humwezesha mtafiti kupata habari ya kina zaidi na zenye umuhimu kwa mtafiti. Kutokana na maelezo ya wasailiwa, nilipata kuchochewa zaidi katika kufanya utafiti huu. Nilipata ushahidi kuwa *Bukuit Ne Tilil* ni tafsiri kutoka kwa Biblia Takatifu ya lugha ya Kiswahili na hivyo kunipa uhuru wa kuchunguza kitabu hiki kitakatifu kiulinganifu.

3.5 Vifaa vya Kukusanya Data

Vifaa kadha wa kadha vilitumika katika kukusanya data ya utafiti huu. Vifaa vilivyotumika katika kukusanya data ni vifuatavyo:

3.5.1 Mwongozo wa usaili

Mwongozo wa usaili uliandaliwa kwa minajili ya kutumika katika kuwasaili wataalamu wa kutafsiri Biblia (Kiambatisho III). Nililenga wataalamu hasa wanaoshughulika katika kutafsiri Biblia kwa lugha ya Kikalenjin. Wataalamu hawa walipatikana katika ofisi ya kutekelezea tafsiri ya Biblia kule mjini Kapsabet. Hata hivyo, sikuweza kupata watafsiri wenyewe waliotafsiri Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*) katika miaka ya sitini; kwa kuwa walikuwa wameshafariki. Niliwapata watafsiri wengine ambao wamebaki katika shirika hilo na ambao bado wanaendeleza

kazi za tafsiri ya Biblia huku wakiendelea kufanya marekebisho na kutoa matoleo ya hivi majuzi. Wataalamu hawa walinisaidia kupata majibu ya maswali yangu.

Kwanza, walinieleza kuhusu sababu zilizowachochea kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Pili, walinisaidia kufahamu baadhi ya mikakati iliyotumika katika kutafsiri matini hii ya Kikalenjin. Wao pia waligusia changamoto zilizowapata watafsiri hadi kusababisha waandike upya matini tafsiri. Aidha nilifahamishwa baadhi ya mbinu zilizotumiwa na watafsiri hawa ili kufaulu katika kuandika M.P kwa namna inayoeleweka kwa H.P. Maoni na mapendekezo yao yalinifaa kwenye uchunguzi wangu na ndiyo yaliyoniwezesha kufikia hitimisho la utafiti huu.

3.5.2 Kinasa sauti

Nilipokuwa nikiwasaili wataalamu wa tafsiri ya Biblia kule Kapsabet, nilitumia kinasa sauti ili kurekodi yale tuliyokuwa tukizungumza. Sababu ya kutumia kinasa sauti ni kwa kusudi la kuhifadhi data muhimu itakayotumika baadaye kwenye uchanganuzi wa data.

Nilitumia kinasa sauti kwenye simu ya mkono. Wakati huu wote, tuliweza kujadiliana bila kuzua utata wowote unaotokana na kunasa sauti za wataalamu hawa. Baadaye, nilifungulia sauti hiyo na kunakili majibu kwa maswali niliyowauliza. Nilichanganua data hiyo kama ilivyoakisi malengo ya utafiti wangu..

Kama wanavyoeleza Kombo na Tromp (2006), nilinukuu vifungu vile vilivyobeba uzito wa utafiti kwenye karatasi. Baada ya kunukuu vifungu hivi, niliingia katika hatua iliyofuata ambayo ni kuchanganua data zilizokusanywa. Nilitekeleza uchanganuzi kwa kujiegemeza kwenye nadharia tete za utafiti huu.

3.6 Unukuzi wa Data

Kombo na Tromp (2006) wanadahili kuwa wakati wa kuzinukuu data, ni jukumu la mtafiti kuangazia data zilizoko muhimu kwenye utafiti wake. Kwa kufuatia mapendekezo haya, kitabu kizima cha Mithali kilisomwa. Baadaye, kikarudiwa kusomwa kwa mara nyingine huku vifungu vilivyoangazia suala la utafiti vikinukuliwa. Hivi vilikuwa vifungu vinavyoangazia utamaduni wa Wakalenjin ili kuelewa ni vipi mtafsiri alivyotafsiri zana za kitamaduni. Pia, vifungu mbalimbali vilisomwa kwa kina ili kutambua mikakati iliyotumika katika kutafsiri vifungu hivyo. Isitoshe, vifungu katika kitabu cha Mithali vilisomwa kwa makini ili kutambua mbinu ambazo zilitumiwa na mtafsiri ili kufanikisha tafsiri yake.

Vifungu vilivyonukuliwa katika kila kipengele vilipangwa na kisha kuchanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kwingineko, kipengele kimoja kilionekana kuwa na vifungu vingi mno. Kwa kuwa uchambuzi wa vifungu hivyo ungeonekana kujirudia, vifungu vichache vilichanganuliwa kwa hali hiyo, ili kuwakilisha vifungu vile vingine. Unukuzi huu ulisaidia kuhakikisha kuwa mtafiti anakamilisha malengo ya utafiti wake pasi na kujichanganya, au hata kusahau mambo mengine muhimu kwenye utafiti.

3.7 Uchanganuzi wa Data

Data iliyochanganuliwa ilitokana na matini ya Biblia ambapo kitabu cha Mithali kilisomwa kwa kina na kisha sura na vifungu mbalimbali kuchanganuliwa. Data ilichanganuliwa kiustahilifu. Hii inahusisha upimaji wa data kwa kutumia maelezo (Mugenda na Mugenda, 2003). Aghalabu, mihimili ya nadharia ya ulinganifu sambamba na ya tafsiri vitendo ilizingatiwa kwenye uchanganuzi huu. Nadharia hizi ziliwezeshakubaini uandishi upya katika matini tafsiri ya Mithali katika *Bukuit Ne Tilil*. Mtafiti alivichanganua vipengele vilivyoakisi uandishi upya katika kitabu hiki.

Vipengele vyenye ni utamaduni, mikakati ya kutafisiri na mbinu za kutafisiri. Ili kufanikiwa katika kuchanganua vipengele hivi, mtafiti alizingatia mambo kamamiundo ya lugha, uteuzi wa maneno na mpangilio wa sentensi kama inavyofafanuliwa katika nadharia ya ulinganifu na ile ya tafsiri vitendo. Baadaye mtafiti alitoa maoni yake kutokana na uchunguzi huu kuhusu iwapo tafsiri ni uandishi upya au la, aghalabu, kwa kutegemea matokeo ya utafiti uliohusu uchanganuzi wa data. Aidha mapendekezo yalitokana na yaliyojiri katika utafiti wenyewe.

Mtafiti katika kuchanganua data yake, alisoma kitabu cha Mithali kwa ujumla huku akichunguza vipengele vinavyohusika na utafiti wake huku akiviainisha. Baadaye, mtafiti alichunguza vifungu hivyo tena kwa mujibu wanadharia tete za utafiti wake huku akifafanua vile vipengele vilivyohusika na utafiti wake. Kwa kuwa mtafiti ni mzungumzaji lugha ya Kikalenjin na pia ninafahamu lugha ya Kiswahili, ilikuwa rahisi kwangu kubaini mambo muhimu yaliyoafiki malengo ya utafiti wangu.

3.8 Hitimisho

Sura hii imeangazia mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu. Mbinu zilizotumika ni pamoja na uchunguzi maktabani, uchunguzi shirikishi, pamoja na usaili. Mbinu hizi zilimfaa sana mtafiti katika kupata data iliyohitajika kwenye uchunguzi huu. Mbinu hizi zilimwezesha mtafiti kufaulu katika ukusanyaji wa data. Mtafiti alitumia vifaa kama vile mwongozo wa maswali ya usaili na pia kuandika data aliyoikusanya kwenye daftari lake. Sehemu hii imeelezea jinsi utafiti mwigo ulivyotekelezwa, jinsi data ilivyochanganuliwa ili kufikia malengo ya utafiti huu na hivyo kuibuka na matokeo maalum.

SURA YA NNE

VIPENGELE MUHIMU KATIKA KUTAFSIRI DHANA ZA KITAMADUNI

4.0 Utangulizi

Utamaduni unahusu hali ya maisha ya wanajamii, itikadi na imani yao. Wakati wa kutafsiri, ni muhimu kwa mtafsiri kumakinika katika kutafsiri vipengele vya utamaduni kwa kuwa hakuna tamaduni mbili zinazofanana. Sura hii inaangazia vipengele mbalimbali vya utamaduni vilivyoshughulikiwa na mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin ili kuhakikisha kuwa anawasiliana na H.P ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kikalenjin. Utafsiri wa vipengele hivi unahakikisha kuwa amewasillisha ujumbe wa mwandishi wa M.A hadi kwa H.P ambao ni Wakalenjin. Tulibaini jinsi ambavyo tofauti kati ya utamaduni wa Wakalenjin na ule wa Waswahili ulivyochangia katika uandishi upya wa Biblia ya Kikalenjin, ambayo ndiyo matini pokezi (M.P).

4.1 Utamaduni wa Wakalenjin

Mila na desturi ya jamii ya Wakalenjin huakisi maisha na imani yao ya kila siku. Wao hutumia lugha kama njia mojawapo ya kipitisha utamaduni wao kutoka kizazi hadi kingine. Katika utafiti huu, niligundua kuwa vipengele vya utamaduni wa wakalenjin vilibainika katika tafsiri ya Biblia ya Kikalenjin. Mtafsiri katika kuvishughulikia vipengele hivi, ama alifaulu au kupungukiwa katika kuzitafsiri dhana mbalimbali. Hii ilipelekea mtafiti kuchunguza vipengele hivyo, hasa vile vilivyoonekana kupelekea tafsiri isikamilike na hiyo kusababisha uandishi upya wa M.T. Vipengele vilivyobainika kutokana na utafiti huu ni kama vifuatavyo;

4.1.1 Tafsiri inayohusu vyakula

Wakalenjin ni jamii ya wafugaji wa mifugo kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo. Ng'ombe ni aina ya mifugo ambaye Mkalenjin halisi anaaminika kuwa lazima awe amewafuga. Ukweli huu unatokana na jinsi Wakalenjin hutumia mifugo hawa kwa kutolea mahari kwa wake zao. Vilevile, wakati wa sherehe zao mbalimbali, wao huchinja ng'ombe. Katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin, ukweli huu unabainika wakati mtafsiri anatafsiri nyama kwa kusisitiza kuwa ni nyama ya ng'ombe wala si nyama yoyote tu. Tazama tafsiri ifuatayo;

Mfano 1.

Mithali 9:2 **M.A** - Amechinja nyama zake, Umechanganya divai yake, Ameiandalia Meza yake pia.

M.P- *Kigoeny tukyik: kigoburuch divaikyik; kigichob amitwogik eng'mesennyi.*

Katika M.P, mtafsiri anapotumia neno **tukyik** (Ng'ombe wake), anatupilia mbali ile dhana ya **nyama** iliyowasilishwa na M.A, na badala yake, nyama yenyewe inafafanuliwa katika M.P kuwa ni ya ng'ombe wala si nyama yoyote tu. Mtafsiri anachagua tafsiri hii kimakusudi ili kuwezesha Wakalenjin kuelewa vyema na kuifanya M.P kuwa na athari sawa na ile ya M.A. Katika jamii ya Waswahili, dhana ya nyama inaeleweka kwa wanajamii, ila kwa Wakalenjin, dhana hiyo inalinganishwa moja kwa moja na nyama inayotokana na ng'ombe. Wao ni wafugaji na ni rahisi kumzungumzia mnyama anayeeleweka kwa wanajamii kwa jumla.

Mkate kwa Wakalenjin ni chakula kigeni. Wao kipindi cha kutafsiri Biblia ya Kikalenjin, mkate ulikuwa unajulikana kwa wachache mno. Hali hii ilipelekea mtafsiri akwepe kutafsiri dhana ya mkate kwa kuwa haingebainika wazi kwa wasomaji wa *BukuitNe Tilil*. Ukweli huu unatokana na tafsiri ya sehemu ifuatayo ya Biblia.

Mfano 2.

Mithali 9:5 **M.A-** Njoo ule mkate wangu, Ukanywe divai niliyoichanganya.

M.P- *Nyo, am amitwogikyuk, Ak iee divaik che kaaburuch.*

Tunavyoona katika tafsiri hii ni kuwa, neno **mkate**, limepewa tafsiri ya **amitwogikyuk**(chakula changu). Mtafsiri kwa kuzingatia L.P, hangeweza kupata kisawe cha neno, Mkate, kwa kuwa Wakalenjin hawakuwa na chakula hiki. Kwa hivyo alitumia neno la jumla la ‘chakula’ ili kuwasilisha dhana ya mkate.

Hali hii pia inapatikana katika;

Mfano 3.

Mithali 23:6 **M.A-** Usile mkate wa mtu mwenye husuda; Wala usivitamani vyakula Vyake vya anasa;

M.P- *Ameam amitwogikabinendet netinyei kong’ ne ya, Amemach amitwogikyik che anyiny:*

Neno **mkate** limefafiriwa kama **amitwogikab** (chakula cha). Kutokana na tafsiri hizi, tunaona kuwa Wakalenjin hawakutumia mkate kama aina ya chakula, hawakuwa na chakula aina ya mkate. Ili kukwepa kutofahamika kwa neno hili, alichagua kutumia neno la jumla ambalo ni ‘chakula’, na hivyo kuuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A kama alivyokusudia.

Tazama pia katika tafsiri ifuatayo:

Mfano 4.

Mithali 28:21 **M.A-**Kupendelea watu si kwema; wala mtu kuasi kwa ajili ya kipande cha Mkate.

M.P- *Ma mie keytii bik: Ana kobistoe chi kole si konyor kerutiet.*

Katika tafsiri hii, *kipande cha mkate* kimetafsiriwa kama *kerutiet* (kifungu au kipimo cha kitu fulani). Mtafsiri amekwepa kutafsiri mkate, kwa kuwa dhana hii haipo katika jamii ya Wakalenjin. Ili kuendeleza mawasiliano haya, amechagua kutumia maelezo yanayopelekea msomaji wa M.P kuelewa kuwa kinachozungumziwa ni kipande wala sio kitu kizima. Hata hivyo, dhana ya mkate imeachwa kabisa kwenye tafsiri hii. Ingawaje tafsiri hii haijazingatia neno ‘mkate’, ni kweli kwamba dhana ya ‘kipande’ imewasilishwa. Hii ni baada ya mtafsiri kubaini kuwa neno ‘mkate’ halikubeba uzito kama neno ‘kipande’ na kwamba kama angejaribu kutafsiri ‘mkate’ angepata ugumu wa msamiati mwafaka kwa maana Wakalenjin hawakutumia mkate kama aina ya chakula.

Ngano ni nafaka ambayo husagwa ili kutumika kuoka mikate. Wakalenjin, kwa kuwa ni wafugaji wa mifugo, hawakubobea sana katika ukulima hadi majuzi hasa baada ya ukoloni. Hali hii ilipelekea mtafsiri wa Biblia ya Kiswahili kutafuta namna nyingine ya kuwasilisha dhana ya ‘ngano’ kwa Wakalenjin ili waelewe kama aina ya chakula.

Tazama mfano ufuatao:

Mfano 5.

Mithali 27:22 **M.A-** Hata ukimtwanga mpumbavu kwa mchi kinuni pamoja na ngano, Upumbavu wake hautamtoka.

M.P- *Agot ngitui chito ne berber eng’ kenut koboto bek che kagitartaran, Ko maistoigei berberindanyi kora.*

Mtafsiri ametafsiri neno *ngano* kama *bek che kagitartaran* (wimbi iliyosagwa). Mtafsiri alichagua kutumia neno ‘wimbi’ badala ya ngano. Sababu ni kuwa, kando na kufuga mifugo, Wakalenjin walifanya ukulima wa wimbi, hasa kabla ya majilio ya wakoloni na hii ikawa ni nafaka mashuhuri sana miongoni mwa wanajamii hawa. Mtafsiri anapotumia dhana ya ‘wimbi’, inakuwa rahisi kwa H.P kuelewa ujumbe

kuliko kama angetumia neno 'ngano' ambalo halikuwa maarufu miongoni mwa Wakalenjin.

4.1.2 Tafsiri ya dhana zinazohusu jinsia

Wakalenjin katika mila na tamaduni zao, hutukuza jinsia ya kiume kuliko jinsia ya kike. Mwanamke huchukuliwa kama mtoto na kwa hivyo mwanamume hurejelewa katika hali mbalimbali kuliko ilivyo mwanamke. Wakati Waswahili wanatumia neno linalojumlisha jinsia zote mbili; yaani jinsia ya kiume na ya kike, hutumia neno 'mwana'. Lakini Wakalenjin wanaonekana kototambua jinsia ya kike na badala yake huashiria jinsia ya kiume.

Vifungu vinavyozingatia tafsiri hii ya 'mwana' kwa maana ya 'mtoto wa kiume' ni vingi katika kitabu hiki cha Mithali. Baadhi ya vifungu hivyo ni pamoja na:

Mfano 6.

Mithali 10:1 **M.A-** Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye
Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye.

M.P- *Iboiboi werit ne ng'om kwanda:
Ago inyalili werit ne berber kamet.
(Werit kwa maana ya mwana wa kiume)*

Mithali 13: 1 **M.A-** Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye;
Bali mwenye dharau hasikilizi maonyo.

M.P- *Epchin it werit ne ng'om kotigonetab kwandanyi:
Ago magasei keretab kong' chotindet.
(Werit kwa maana ya mwana wakiume)*

Mithali 15:20 **M.A-** mwana mwenye hekima humfurahisha babaye;
Bali mpumbavu humdharau mamaye.

M.P- *Iboiboi kwanda werit ne ng'om:
Ago sasei kamet chito ne berber.
(Werit kwa maana ya mwana wa kiume)*

Mithali 19:13 **M.A-** Mwana mpumbavu ni msiba kwa babaye;
Na ugomvi wa mke kama kutona-tona daima.

M.P- *Nyalildab kwandandanyi werit ne berber:
U beek che saitoi bolatetab osotiot.
(Werit kwa maana ya mwana wa kiume)*

Mithali 28:7 **M.A-** Yeye aishikayesheria ni mwana mwenye hekima;
Bali aliye rafiki wa walafi humwaibisha babaye.

M.P- *Werit ne ng'om age tugul ne ribei ng'atutik:
Ago itewri kwandanyi inendet ne choruetab kipkeinik.
(Werit kwa maana ya mwana wa kiume)*

Kwenye mifano iliyotolewa, ni dhahiri kuwa neno *werit* ni tafsiri ya neno mwana na ambaye katika muktadha huu wa Kikalenjin lina maana ya mwana wa jinsia ya kiume. Katika Kiswahili, neno hili halibagui jinsia bali linatumika kwa maana ya mtoto wa jinsia yoyote ile - awe wa kiume au wa kike. Lakini katika jamii ya Kikalenjin, utamaduni wao unamuenzi sana mtoto wa kiume. Hali hii inapelekea mtafsiri kulitafsiri neno hili kwa kugemea mkondo wa kiutamaduni ambapo anapendelea mtoto wa jinsia ya kiume. Iwapo angetafsiri tu bila kuzingatia utamaduni wa Kikalenjin, basi tafsiri ya neno hili lingekuwa *lakwet*, kwa maana ya mwana – yaani wa jinsia yoyote.

Mfano 7.

Mithali 8:32 **M.A-** Basi, wanangu, nisikilizeni sasa;
Maana heri hao wazishikao amri zangu.

M.P- *Ogasa anyun, werju:
Amu iberurotin ichek che ribei ortimwekyuk.
(Werju ina maana ya wana hawa wa kiume)*

Katika mfano wa hapa juu, tunaona jinsi neno wanangu linavyotafsiriwa kama *werju*. Tafsiri hii inazingatia jinsia ya kiume na kutupilia mbali jinsia ya kike. *Werju* ni neno linalotumika kama kivumishi kiashiria cha karibu lakini katika wingi, linaloonyesha

jinsia ya kiume wala si kike. Mwandishi wa Biblia ya Kiswahili alikusudia kuwasiliana na jinsia zote lakini mtafsiri anaegemea jinsia moja.

Mfano 8.

Mithali 5:1 **M.A-** Mwanangu, sikiliza hekima yangu;
Tega sikio lako, mzisikie akili Zangu;
M.P- *Werinnyu, kas ng'omnatennyu; epchi it naennyu:*

Mithali 6:1 **M.A-** Mwanangu, kama umekuwa mdhamini wa rafiki yako,
Ikiwa wewe na rafiki mme pana mikono,
M.P- *Werinnyu, ngot iegu ne itononjinichitab kokweng'ung,*
Ngot ko kooyosie onamge eunek ak kipsagarin,
(Werinnyu hapo ina maana ya mwana wangu wa kiume)

Mithali 23:15 **M.A-** Mwanangu, kama moyo wako una hekima,
Moyo wangu utafurahi, naam moyo wangu;
M.P- *Werinnyu, ngo ng'om muguleldang'ung',*
Kobaibai muguleldanyu, ee, baibai muguleldanyu:
(Werinnyu ina maana ya mwana wangu wa kiume)

Mithali 24:13 **M.A-** Mwanangu, ule asali, kwa maana ni njema,
Na sega la asali lililo tamu ulionjapo.
M.P- *Werinnyu, am kumik, amu miach;*
Koboto masamek, amu anyiny ye ichamjami:
(Werinnyu ina maana ya mwana wangu wa kiume)

Mithali 27:11 **M.A-** Mwanangu, uwe na hekima na kunifurahisha moyo wangu;
Ili nipate kumjibu anilaumuye.
M.P- *Werinnyu, ng'omitu, ak ibaibai muguleldanyu,*
Si amuch awolji inendet ne itewera.
(Werinnyu ina maana ya mwana wangu wa kiume)

Katika mifano hii, neno *mwanangu* limetafsiriwa kama *werinnyu* (mwangu wa kiume). Wakalenjin wanaonekana kusifu na kutilia maanani watoto wa jinsia ya kiume kuliko wale wa kike. Hali hii haina maana kuwa wanadharauliwa, lakini wanachukuliwa kuwa viumbe dhaifu na kwa sababu hii, hamna haja ya kuwazungumzia. Watoto wa kiume wanachukuliwa kuwa na umuhimu kwa kuwa wao wanaaminika kuendeleza jamii. La sivyo, neno 'mwanangu' lingetafsiriwa kama 'lakwenyu' kwa kuwa hili ni neno lisilobagua jinsia yoyote. Katika kitabu kizima cha

Mithali, neno ‘mwana’ limetafsiriwa kama ‘mwana wa kiume’. Kumaanisha mwanamke au mtoto wa kike hatambuliki kama mtoto ila yule wa kiume.

Mfano 9.

Mithali 19:18 **M.A-** Mrudi mwanao, kwa maana liko tumaini;
Wala usiikaze nafsi yako kwa kuangamia kwake.

M.P- *Itigon wering’ung’ kotagomi kamang’unet;
Amat itil eng’ muguleldang’ung’ ile mie ngo mee.
(Wering’ung’ ina maana ya mwana wako wa kiume)*

Mithali 29:17 **M.A-** Mrudi mwanao naye atakustarehesha.
Naam, atakufurahisha nafsi yako.

M.P- *Itigon wering’ung’, si kogonin kamuung’et;
Ee, si kobaibai sobondang’ung’.
(Wering’ung’ ina maana ya mwanao wa kiume)*

Mifano hii vilevile imeonyesha ubaguzi wa kinjinsia kwa sababu, neno *wering’ung’* limetafsiriwa kama mwana wako wa kiume. Labda mtafsiri angetafsiri hapa kama wanao, bila kuzingatia jinsia. Hata hivyo, uandishi huu upya umesababisha tafsiri hii kukubalika miongni mwa Wakalenjin ambao wanamtukuza mtoto wa jinsia ya kiume kuliko wa kike.

Mfano 10.

Mithali 13: 24 **M.A-** Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe;
Bali yeye ampendaye humrudi mapema.

M.P- *Wechei werinnyi ne mabirei:
Ago inendet ne chamei werinnyi kotigoni ko u ye nyalu.
(Werinnyi ina maana ya mwana wake wa kiume)*

Mfano huu vilevile unaonyesha namna neno mwanawe linavyopewa tafsiri ili kukidhi mahitaji ya jamii ya Wakalenjin. Hivyo, linatafsiriwa kama *werinnyi* kwa maana ya mtoto wake wa kiume. Kipengele cha ‘mwana’ kinachukuliwa kama ni yule wa kiume pekee, huku wa kike akipuuziliwa mbali.

Kutokana na tafsiri ya mifano yote hapo juu, mtafsiri ameonyesha jinsi mtoto wa kiume anavyopewa umuhimu zaidi kuliko mtoto wa kike. Kila mara, jinsia zote zinapostahili kuzungumziwa, tunaona mtoto wa kike akipuuzwa na badala yake wa kiume anatajwa. Hii ni kwa mujibu wa utamaduni wa Wakalenjin, ambapo mtoto anapotajwa, kwao huchululia kama ni wa kiume wala si wa kike. Mtafsiri alipaswa kuzingatia utamaduni huu ili kuwafikia walengwa wa M.T ambao ni Wakalenjin. Kutafsiri huku ndiko kulikosababisha kuwepo na uandishi upya wa dhana zinazohusiana na jinsia. Uandishi upya huu ni kwa makusudi ya kuifikia H.L na kuifanya kazi tafsiri ionekane kama kazi halisi wala si tafsiri.

4.1.3 Taasubi ya kiume katika tafsiri

Hii ni hali ambapo mwanamume anaonekana kupendelewa kuliko mwanamke, yaani, mwanamke anadunishwa. Hali kama hii huweza kutokea kwa mfano iwapo mambo mazuri yanahusishwa na wanaume ilhali mambo maovu yanahusishwa na wanawake. Katika Biblia ya Kikalenjin, mtafsiri ameonyesha hali hii kwa namna ya wazi kabisa katika tafsiri yake kwa kuwahusisha wanawake na mambo hasihuku wanaume wakihusishwa na mambo chanya. Tutazame mifano hii:

Mfano 11.

Mitahli 2:16 **M.A**- Ili kuokoa na malaya,
Naam,malaya mwenye kubembeleza kwa maneno yake.

M.P- *Si gosor eng' chepkugoniot,*
Ee, kwondo ne chemwai kut;

Katika tafsiri hii, neno *malaya* ambalo katika L.A (Kiswahili) linaashiria jinsia zote, yaani ya kike na kiume, limetafsiriwa kama *chepkugoniot* (mwanamke malaya). Kiambishi '*chep*' ikiwa ni kiambishi kiwakilishi cha jinsia ya kike. Jambo la wazi ni kuwa mwanamke amedunishwa kwa kuonekana kama ndiye malaya wala si mwanaume. Msisitizo huo pia upo katika sehemu ya pili ya kifungu. M.A katika

mstari unaofuata unazungumzia malaya kuwa anabembeleza, lakini M.P inazungumzia mwanamke (*kwondo*)mwenye kubembeleza kwa maneno matamu (*ne chemwai kut*). Kumaanisha kuwa wanaobembeleza si wanaume bali ni wanawake.

Tunapata hali kama hii vile vile katika tafsiri ifuatayo:

Mfano 12.

Mithali 5:3 **M.A-** Maana midomo ya malaya hudondoza asali,
Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta:

M.P- *Amu saune kumiat kutitab chepkugoniot,
Ago tangusen nag'alekyik kosiir mwaita:*

Katika tafsiri hii, neno *malaya* limetafsiriwa kama *chepkugoniot* (mwanamke ambaye ni malaya). Vile vile;

Mfano 13.

Mitahli 22:14 **M.A-** Kinywa cha malaya ni shimo refu;
Anayechukiwa na BWANA atatumbukia ndani yake.

M.P- *Keringet ne loo kutitab chepkugoniot:
Ibutyin yoto inendet ne nerekyin Jehovah*

Hapa tena, mtafsiri ametafsiri neon *malaya* kama *chepkugoniot* (mwanamke malaya) yaani '*chep*' ikiwa ni kiambishi awali kinachoashiria nafsi ya kike. Mifano ya tafsiri hizi inaonyesha kuwa katika utamaduni wa Wakalenjin, mwanamke pekee ndiye anayeweza kuhusishwa na umalaya wala si mwanamume. Na hii ni kwa sababu katika utamaduni wa Wakalenjin, mwanamume anaweza kuwa na uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa bila kushutumiwa. Isitoshe, ikiwa ana haja ya kuoia wanawake zaidi ya mmoja, huwa na uhuru huo, jambo ambalo halikubaliki kwa wanawake; ikiwa atakiuka kaida hii, atachukuliwa kama malaya. Kwa hiyo, katika jamii ya Wakalenjin malaya huwa ni wanawake wala haiwezekani kwa mwanamume kuwa malaya. Utamaduni huu huzua dhana ya taasubi ya kiume kwa kuwa wanaume tu ndio

wanaoonekana kuwa wema; hata wakihusika na matendo ya umalaya, wao huonekana kuwa kawaida na wanaruhusiwa. Lakini iwapo mwanamke ataolewa na zaidi ya mume mmoja, au awe na uhusiano nje ya ndoa, yeye hushutumiwa na kuonekana kama malaya. Mwanamke kama huyo hubaguliwa na jamii kwakuhusika na kitendo kama hicho.

Mfano 14.

Mithali 29:3 **M.A** Apendaye hekima humfurahisha babaye:
Bali ashikanaye na makahaba hutapanya mali yake.

M.P *Ibaibaikwanda age tugul ne chamei ng'omnatet:
Ago iseerseeri tuguk inendet ne namegei ak chepkugonik.*

Mtafsiri ametumia neno **chepkugonik** kwa tafsiri ya **makahaba**. Katika M.A, neno makahaba halina mpaka wowote wa kijinsia, kwani wanaweza kuwa wanawake au wanaume. Lakini mtafsiri anapotumia kiambishi '*chep*' ambacho ni kiwakilishi cha jinsia ya kike, anamaana kuwa katika utamaduni wa Wakalenjin, niwanawake tu ambao wanaweza kujihusisha na ukahaba bali sio wanaume. Hili linathibitisha taasubi ya kiume ya kiwango cha juu miongoni mwa Wakalenjin.

Mfano mwingine unaodhihirisha udunishaji wa wanawake miongoni mwa Wakalenjin unatokana na mfano huu hapa;

Mfano 15.

Mithali28:23 **M.A** Amkemeaye mwenzake hatimaye atapata kibali;
Zaidi ya mtu ajipendekezaye kwa ulimi wake.

M.P *Tun nyoru chamet inendet ne kere kong' chi
Kosiir inendet ne chemwai gut.*

Neno **mtu** katika L.A lina maana ya mwanadamu wa jinsia ya kiume au ya kike bila kubagua. Lakini katika L.P, neno hili limetafsiriwa kama **chemwai**, kwa maana ya, mwanamke mdanganyifu. Tafsiri hii inafanya M.P kuwa tofauti na M.A kwa sababu

kiambishi *'che'* kinarejelea jinsia ya kike wala si ya kiume. Dhana ambayo haijawasilishwa na M.A.*Chemwai gut* ina maana ya mwanamke adanganyaye kwa kutumia ushawishi mkubwa sana; akitumia maneno matamu kutoka kinywa chake. Jamii ya Wakalenjin huamini kuwa ni mwanamke tu anayeweza kudanganya kwa kutumia maneno matamu wala si mwanamume. Mwanamume hachukuliwi kuwa mdanganyifu. Hii ni sifa inayoaminika kupatikana miongoni mwa wanawake pekee. Katika misemo yao mara nyingi hukanya wanaume wasiwe kama wanawake ambao maneno yao hayaaminiki. Kwa hivyo tafsiri hii imepotosha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa M.A

Isitoshe, mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin anaendelea kuonyesha jinsi utamaduni wa Wakalenjin unavyomtukuza mwanaume. Tutazame hapa chini;

Mfano 16.

Mithali 7:19 **M.A** Maana mume wangu hayumo nyumbani,
Amekwenda safari ya mbali.

M.P *Amu mami ga chitab kobo got, Kawa banda ne loo:*

Katika tafsiri hii, maneno, *mume wangu* yametafsiriwa kama *chitab kobo got* (mtu mwenye kumiliki nyumba). Labda mtafsiri angetafsiri kama *manong'otiannyu* (mume wangu) kama ilivyowasilishwa katika M.A. Lakini kutokana na tafsiri hii, inadhihirika kuwa katika jamii ya Wakalenjin, mwanaume ndiye mwenye kumiliki nyumba wala si mwanamke. Licha ya kuwa wameoana, hawawezi kumiliki nyumba wote wawili kama jamii, ila nyumba ni mali ya mwanamume pekee. Badala ya mwanamke huyu kudai kuwa mume wake hayuko nyumbani, anasema kuhusu yule mwenye nyumba ambaye katika jamii ya Wakalenjin ni mwanaume. Mwanamke kamwe hawezi kumiliki nyumba au hata mali iliyoko katika boma ambapo ameolewa. Kazi yake ni kuzaa na kuchunga mali ya mumewe wala si kumiliki. Tafsiri hii

inaonyesha jinsi Wakalenjin wanavyowatukuza wanaume huku wakiwadunisha wanawake katika utamaduni wao.

4.1.4 Tafsiri Inayohusu hali za kimazingira

Wakati wa kutafsiri, mtafsiri huzingatia mazingira ya walengwa huku akilinganisha na mazingira ya hadhira asilia. Endapo mazingira yao ni tofauti, ina maana kwamba lazima atakuwa makini ili kwamba awasilishe ujumbe wa M.A kwa namna ambavyo haitaathiri ujumbe asilia kwa kuwa mara nyingi, kimazingira hutofautiana kutoka kwa jamii hadi nyingine. Katika kutafsiri Biblia ya Kiswahili hadi Kikalenjin, ni bayana kuwa mazingira ya Waswahili ni ya pwani huku ya Wakalenjin yakiwa ni ya bara. Mtafsiri hivyo basi hulazimika kuzingatia hali hii na hivyo kufanikisha mawasiliano ya mwandishi wa M.A kwa H.P. Katika Biblia ya Kikalenjin, tunaona namna mtafsiri alivyokabiliana na hali hizo kwa namna ya kipekee. Kwa mfano, katika tafsiri ifuatayo;

Mfano 17.

Mithali 20:17 **M.A** Chakula cha uongo ni kitamu kwa mtu;
Lakini halafu kinywa chake kitajaa changarawe.

M.P *Anyiny eng' chi amitwogikab lembeita;*
Ago ne matia konyi kutinnyi koik.

Changarawe ni aina ya mchanga unaopatikana kando kando mwa bahari, maziwa au hata mito. Ni aina ya mchanga uanotumika sana katika ujenzi wala si bora sana katika ukulima wa nafaka nyingi. Mchanga aina hii haupatikani sehemu nyingi za bara. Wakalenjin ni wafugaji na kwa hiyo walipendelea maeneo yenye malisho bora kwa mifugo yao ambapo, hasa ni sehemu za bara. Waswahili walijihusisha katika biashara na uvuvi na hivyo wao ni watu wanaopatikana katika pwani ya Kenya. Kutokana na kuwepo kwa Bahari ya Hindi, sehemu ya pwani basi ina wingi wa changarawe.

Katika tafsiri ya mfano wa 17, mtafsiri alitafsiri neno *changarawe* kama *koik* (mawe). Hii ni kwa sababu H.P ambao ni Wakalenjin hawangeelewa changarawe kwa sababu ya kuishi katika mazingira yasiyokuwa na mchanga aina hii. Ukulima wa mimea kama mahindi na mtama uliokuwa maarufu miongoni mwa Wakalenjin na hauwezi ukafanyika sehemu yenye mawe. Kwa hiyo ili kuleta picha ya ukavu unaotokana na changarawe, mtafsiri alitumia neno mawe ili kufanikisha mawasiliano yake na H.P.

4.1.5 Tafsiri ya mila na desturi

Wakalenjin wana mila na desturi zao ambazo ni tofauti na zile za Waswahili. Hali hii inafaa kuzingatiwa wakati wa kutafsiri matini moja kwenda kwa nyengine ili mwishowe, kuwe na welewa kwa wanaokusudiwa na kazi tafsiri. Katika kutafsiri Biblia ya Kiswahili kwenda kwa lugha ya Kikalenjin, tunaona mtafsiri akizingatia hoja hii.

Mfano 18.

Mithali 24:11 **M.A** Uwaokoe wanaochukuliwa ili wauawe;
Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe.

M.P *Soru ichek che kimuti koba meet,
Ak iet ichek che kimachei kebar.*

Katika kutafsiri sehemu hii, mtafsiri ametafsiri neno *kuchinjwa* kama *kebar* (kuuawa). Wakalenjin katika desturi na mila zao, mwanadamu hachinjwi (keeney) ila ni mnyama tu ambaye huchinjwa. Mwanadamu huuwana (*kebar*), kwa sababu mwanadamu ndiye anayeaminika kuwa na nafsi tofauti na aliyonayo mnyama. Kwa hiyo katika kutafsiri kwa namna ambavyo ujumbe wa mwandishi wa M.A ungeweza kuhifadhiwa, basi ilimpasa mtafsiri kuzingatia mila na desturi za Wakalenjin na kuwasiliana kwa urahisi. Katika mila ya Wakalenjin, mnyama huchinjwa kwa minajili ya kuliwa nyama. Hii ndiyo sababu, mtafsiri hangeweza kutafsiri vivyo hivyo kwa sababu mwanadamu katika jamii ya Wakalenjin haliwi kama alivyo mnyama. Iwapo

mtu atauliwa, ina maana kuwa hawezi akaliwa lakini kama atachinjwa, ina maana kuwa ataliwa; jambo ambalo si la kawaida katika mila na desturi za Wakalenjin.

Mfano mwingine unaoonyesha tafsiri inayozingatia mila na desturi za Wakalenjin ni hii;

Mfano 19.

Mithali 27:27 **M.A** Tena yatakuwapo maziwa ya mbuzi,
Ya kukutosha kwa chakula chako,
Na chakula cha watu wa nyumbani mwako,
Na posho la vijakazi vyako.

M.P *Ak mitei chegab ng,ororek che yamei koek amitwogiguk,
Ak che chebo bikab gong'ung;
Ak amitwogik che yamei tibiguk.*

Katika tafsiri hii neno **vijakazi** limetafsiriwa kama **tibiguk** (mabinti zako). Katika Kamusi ya Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004), neno mjakazi lina maana ya mtumwa ambaye ni mwanamke. Wakalenjin katika mila na desturi yao, hawakuwa na wajakazi kwa kuwa hawakuhusika na biashara ya kuuza na kununua watumwa. Waswahili waliishi kule pwani pamoja na wageni kama Waarabu waliojikusisha na biashara ya kununua watu na kuwauza. Kwa hivyo, Waswahili kwa sababu waliishi kwenye mazingira ya biashara ya aina hiyo, waliiga tabia hii ya kununua na kuuza watumwa na vijakazi, na dhana hii ikawa ni sehemu ya lugha yao. Kwa sababu ya umbali wa kimasafa ya bara kutoka pwani, Wakalenjin hawakushuhudia biashara ya watumwa. Kwa hivyo jambo la kununua na kuuza watumwa ni jipya sana miongoni mwao. Mtafsiri kwa kufahamu hali hii, hangeweza kutafsiri neno hili kwa namna nyingine yoyote ila kwa kutumia neno ambalo linaafikiana na mila na desturi ya H.P.

Jambo la kuuza na kununua wanadamu ni la unyama miongoni mwa Wakalenjin, ila tu mifugo na vitu vingine visivyo na uhai huweza kuuzwa na kununuliwa. Kwa sababu Biblia ni neno kutoka kwa Mungu, mtafsiri hangethubutu kutumia maneno

yasiyoambatana na mila na desturi za Wakalenjin kwa kuwa yangechangia katika kumfanya Mungu aonekane mbaya na labda neno hili (Biblia) likakosa kuaminika miongoni mwa Wakalenjin. Mtafsiri anapotumia neno *tibiguk*, anaonyesha utu unaoambatana na tabia za Wakalenjin, kwa sababu hata kama mtoto si wako kwa kuzaliwa, Mkalenjin ni lazima atamtambulisha kama wake kwa kuwa anaishi naye. Neno *tibiguk* (mabinti zako) linaashiria kuwa ni wake kwa sababu wanaishi naye, wala hawatambulishwi kama wageni wasio wake. Yaani hata kama Mkalenjin angeomba mtoto au kumwajiri, hangeonyesha kuwa huyo ni tofauti na watoto wake bali wote- pamoja na watoto wake- wangechukuliwa kama ni wa nyumba moja au baba mmoja.

Tunaipata tafsiri sawa na hii pia katika;

Mfano 20.

Mithali 31:15 **M.A** Tenahuamka, kabla haujaisha usiku;
 Huwapa watu wa nyumbani mwake chakula;
 Na wajakazi wake sehemu zao.

M.P Ng'eetei kogeny kota ko kemoi, ak kobai bikab gonnyi,
 Ak kogoch tibikyik boisienywa.

Neno wajakazi limetafsiriwa kama *tibikyik* (mabinti wake). Dhana ya mabinti wake inaonyesha ile hali ya kuhusiana kwa damu, yaani, kama ni mtoto wa kuzaa, kinyume na inavyowasilishwa na M.A inapoeleza kuhusu 'mabinti wako uliowanunua'. Mjakazi humilikiwa kutokana na kutoa malipo lakini binti ni wako wa kuzaa, unayehusiana naye kwa damu. Mtafsiri katika hali hii anaonekana kuchagua msamiati huu ili kukidhi mahitaji ya desturi na mila ya Wakalenjin.

Mfano 21.

Mithali 7:22 **M.A** Huyo akafuatana naye mara hiyo,
 Kama vile ng'ombe aendavyo machinjoni;
 Au mpumbavu kuadhibiwa katika pingu;

*M.P Isubi anyun inendet kwonyotok eng' yoto,
Ko u eito ne kikwerie kwo eng'set,
Anan kou mugurek che kitigone ne berber*

Mtafsiri ametafsiri neno **ng'ombe** kama **eito** (ng'ombe dume). Katika utafsiri huu, tunaona mtafsiri akitumia neno **eito** ambalo lina maana tofauti na ilivyo katika M.A. Labda kama angetaka kukuza msamiati uliotumika katika M.A, angetumia neno **teta** lenye maana ya ng'ombe. Tafsiri hii imeathiriwa na mila ya Wakalenjin ambapo kila mara wanapotaka kumchinja ng'ombe, huwa wanamchagua dume kwa sababu majukumu yake si mengi; kwa mfano hakamuliwi wala hazai. Kwa hivyo, mara nyingi, utampata Mkalenjin akitafuta ng'ombe dume wa kumchinja wala si wa kike.

Dhana hii vilevile inabainika katika kifungu kifuatacho;

Mfano 22.

Mithali 15:17 **M.A** Chakula cha mboga penye mapendano;
Ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.

*M.P Kaigai keam ngwek eng' ole mi chamnyet,
Kosir eito ne akwai koboto wechet.*

Mtafsiri hapa ameonyesha jinsi desturi ya Wakalenjin ilivyo. Anapotafsiri **ng'ombe** kama **eito** (ng'ombe dume), anatuonyesha bayana kwamba Mkalenjin hawezi kumchinja ng'ombe wa kike kwa ajili ya kuliwa kama chakula ila dume ndiye huchaguliwa. Wakati wa sherehe au kama kuna haja ya kutumia nyama kama chakula, Wakalenjin huchagua ng'ombe dume pekee kwa kazi hiyo. Hiyo ndiyo sababu hali hii inaonekana katika tafsiri hii.

4.2 Hitimisho

Katika sura hii tumeoana vipengele kadha wa kadha vinavyohusiana na utamaduni wa jamii ya Wakalenjin na jinsi vipengele hivyo vilivyozingatiwa katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit ne Tihil*) ili kukuza ujumbe wa mwandishi wa M.A, huku

ujumbe wa M.A ukiwasilishwa kwa namna ambayo H.P hufikiwa. Utamaduni ni jambo la muhimu sana katika jamii yoyote ikiwemo jamii ya Wakalenjin. Hii inapelekea mtafsiri kuwa makini sana anapotafsiri dhana za kitamaduni. Nadharia ya Tafsiri Vitendo imebainisha wazi kuwa tamaduni zote ulimwenguni hazifanani, na kwa hivyo mtafsiri anapaswa kuelewa utamaduni wa H.A na ule wa H.P, ili anapotafsiri, aweze kuchagua kwa makini msamiati mwafaka wa kutumia katika M.T, na hivyo kusababisha H.P kuelewa ujumbe uliokusudiwa na mwandishi wa M.A.

Kutokana na uchunguzi huu tumeona kuwa mtafsiri alibadilisha vipengele mbalimbali vilivyowasilishwa katika M.A, ili viweze kukimu mahitaji ya kitamaduni ya H.P. Haya yanaafiki maelezo ya nadharia ya ulinganifu sambamba ambayo inapendekeza vipengele vya kitamaduni vibadilishwe ili kuafiki matakwa ya utamaduni wa lugha pokezi, kwa sababu utamaduni wa Wakalenjin ni tofauti na ule wa Waswahili. Ili kuwafikia Wakalenjin, ilimpasa mtafsiri kuzingatia utamaduni wa Wakalenjin na hivyo kuwafanya waone kuwa M.P inawalenga wao wenyewe. Uandishi upya umetekelezwa hapa na mtafsiri ili kuhakikisha kuwa H.P inapokea ujumbe wa mwandishi wa M.A pamoja na athari sawa na za H.A, kwa mujibu wa nadharia ya tafsiri vitendo. Tofauti za kitamaduni pia zimechangia kwa mtafsiri kuandika upya M.L ili wasomaji ambao ni Wakalenjin, wanapoisoma, wataona kama ni kazi halisi wala haijatolewa kwingineko. Uandishi upya pia umesaidia M.L kueleweka vyema kwa H.P, kwani kama ingelitafsiriwa tu moja kwa moja bila kubadilisha dhana yoyote ili kukidhi mahitaji ya Wakalenjin, basi tafsiri hii haingeweza kuhifadhi ujumbe wa mwandishi wa M.A na hivyo kupotosha H.P. Kijumla, nadharia hizi mbili zilikuwa muhala katika kutafsiri vipengele vya kitamaduni katika *Bukuit Ne Tilit*.

SURA YA TANO

MIKAKATI ILIYOTUMIKA KATIKA KUTAFSIRI *BUKUIT NE TILIL*

5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua mikakati mbalimbali iliyotumika katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin (*Bukuit Ne Tilil*). Ili kufaulu katika utafsiri wowote, mtafsiri atalazimika kutumia ujuzi maalum ndipo afaulu katika kazi yake. Mtafsiri wa matini ya *Bukuit Ne Tilil*, alilazimika kujumuisha mikakati si haba ili kuifanya kazi hii ifanikiwe. Mikakati iliyotumika ni kama vile ukopeshaji wa msamiati wa lugha asilia, utohozi wa maneno yasiyo na visawe katika lugha ya Kikalenjin, upanuzi wa maana ya msamiati katika maelezo kwenye lugha pokezi, udondoshaji wa sehemu za M.A katika tafsiri, ufafanuzi wa ujumbe wa M.A katika tafsiri, urekebishaji wa maelezo katika tafsiri na ujumlishwaji wa msamiati husika katika tafsiri. Sehemu inayofuata imeshereheshea mikakati mbalimbali iliyotumika katika kutafsiri Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin.

5.1 Utohozi wa Maneno ya L.A katika L.P

Maneno mengine yalionekana kukosa kabisa visawe vyake katika L.P na hali hii ilisababisha mtafsiri kutohoa maneno yale ili kimofolojia yawe na umbo la maneno ya L.P. Mifano ya maneno yaliyotoholewa ni mingi sana katika *Bukuit Ne Tilil*. Jedwali lifuatalo limesheheni mifano:

Jedwali 1: Jedwali linaloonyesha maneno yaliyotafsiriwa kwa kutoholewa

KIFUNGU	MATINI ASILIA	MATINI POKEZI
Mithali 1:1	Sulemani, Israeli	Solomon, Israel
Mithali 6:23	Taa	Tait
Mithali 7:6	Dirisha	Tirisiet
Mithali 7:20	Fedha	Fedaisiek
Mithali 8:19	Dhahabu,fedha	Tahabu,feda
Mithali 9:2	Divai	Divaik
Mithali 11:2	Pete, meza,dhahabu	Peteit,mesa,tahabu
Mithali 14:11	Hema	Emait
Mithali 17: 3	Fedha,dhahabu	Feda, tahabu
Mithali 24:30	Zabibu	Sabibuk
Mithali 25:4	Fedha	Feda
Mithali 30: 1	Aguri, Yake, Ithieli, ukali	Agur,Jake,Itiel, Ukali
Mithali 31:1,4	Lemueli	Lemuel
Mithali 31:13	Kitani	Kitanit
Mithali 31:16	Mizabibu	Sabibuk
Mithali 31:21	Theluji	Teluchi

Kutokana na jedwali hili, ni wazi kuwa maneno kadha wa kadha yalitoholewa kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin wakati wa kutafsiri. Sababu ya kutohoa inatokana na hali kuwa maneno mengine katika L.A hayana visawe vyake katika L.P, na hivyo ili mtafsiri awasiliane na H.P, alitohoa maneno hayo ili kimofolojia na kifonolojia yakubalike. Kimofolojia, maneno mengi ya Kikalenjin huishia kwa sauti za konsonanti wala si za irabu, kama inavyobainika katika jedwali.1 hapo juu. Umbo hili hubadilishwa katika tafsiri ili kuhakikisha uhalisia wake kwa H.P, hasa wakati wanapotamka. Isitoshe, kifonolojia, sauti /j/ hubadilika na kuwa /ch/,/dh/ huwa /d/,/z/ huwa/s/, /d/ huwa /t/ na kadhalika. Mabadiliko haya yanatokana na sababu kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu, huku Kikalenjin ikiwa ni lugha ya Kinailoti na hivyo, sauti za lugha hizi haziafikiani kimofolojia. Ili kuleta uwiano na wepesi wa

kuyatamka, mtafsiri aliyaandika upya kwa mwendelezo wa kutohoa ili H.P iwe na wepesi wa kuyatamka hayo maneno. Utafsiri wa Biblia ya Kikalenjin hasa katika kitabu cha Mithali umesheheni utohozi wa msamiati wa Kiswahili. Mkakati huu wa utafsiri ulichangia pakubwa katika kufaulu kwa tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil*. Iihakikisha kuwa mawasiliano yanakamilika kwa kutumia maneno yenye mwendelezo wa sarufi ya lugha ya Kikalenjin.

Mkakati huu unaungwa mkono na nadharia ya ulinganifu sambamba kwa kuwa inapendekeza kuwa mtafsiri azalishe M.P inayolingana kimtindo na M.A. Katika jedwali tunaona kuwa maneno yanatoholewa ili kimtindo, yaafikiane na yale ya M.A. Ingawa maneno yameandikwa upya, lakini maana inalingana na ile ya M.A.

5.2 Upanuzi wa Maana ya Maneno

Mkakati huu unahusu hali ambapo mtafsiri hutafsiri neno bila kutumia kisawe bali hutumia maelezo mengi ili kutafsiri neno moja au sehemu fupi ya sentensi. Mkakati huu humsaidia msomaji wa M.P kuelewa zaidi kwa kuwa tafsiri imetekelezwa kwaundani huku msamiati mmoja ukifafanuliwa kwa maneno mengi yanayomwezesha msomaji kupata maelezo yanayomfanya kuelewa ujumbe zaidi. Mfano wa sehemu zilizotafsiriwa kwa kutumia mkakati huu ni kama;

Mfano 23.

Mithali 16:5 **M.A** Kila mwenye moyo wa kiburi ni chukizo kwa BWANA;
Hakika, hatakosa adhabu.

*M.P kit ne wechei Jehovah ko muguleldo age tugul ne menei:
Agot ngo namgei eunek, ko magimeto ama kibar*

Mtafsiri amepanua tafsiri hii anaposema '*Agot ngo namgei eunek*' yaani, 'hata kama wataelewana'. Mtafsiri hapa anataka kusisitiza hali ya kukubaliana au kuelewana, kwamba hata kama watu wataelewana kutenda maovu, ni lazima watapata adhabu

kwa kuwa wamekosa. Upanuzi huu umesaidia msomaji wa M.A kuelewa zaidi muktadha wa usemi huu, na hivyo kuelewa zaidi.

Mfano 24.

Mithali 16:10 **M.A** Kukata maneno huwa katika midomo ya mfalme;
Kinywa chake hakitakosa katika hukumu.

M.P *Bunu kutitab laitoriat tiletab kiruoget ne bo kamuktaindet:
Malelei kutinnyi eng' kiruoget.*

Mtafsiri anaonekana kuongeza maelezo zaidi katika tafsiri yake anaposema, '**ne boKamuktaindet**' kwa maana, 'ya Bwana Mungu'. Labda katika kuongeza maelezo hayo, mtafsiri alikusudia kusisitiza kwamba ingawa ni mfalme anayeweza 'kukata maneno' lakini Mungu ndiye anayetoa maamuzi. Maelezo haya hayapatikani katika M.A lakini mtafsiri anapotumia inakuwa kwamba anapanua msamiati wa M.P

Mfano 25.

Mithali 18:22 **M.A** Apataye mke apata kitu chema;
Naye ajiapatia kibali kwa BWANA.

M.P *Nyuru kit ne mie age tugul ne nyuru osotiot ne ituni;
Ak nyuru chamet eng' taitab Jehovah.*

Tafsiri hii imepanuliwa kwa kuwa maneno '**ne ituni**' yaani 'wa kumwoa' ni maneno yasiyokuwemo kwenye M.A lakini yanaongezwa kwenye M.P. Nyongeza hii inaonekana kuwekwa na mtafsiri ili kuleta msisitizo kwamba si mke tu bali ni yule wa kumwoa. Msisitizo huu unafaa ingawa inaonekana kuipanua M.P.

Mfano 26.

Mithali 19:10 **M.A** Maisha ya anasa hayampasi mpumbavu;
Sembuse awatawale wakuu.

M.P *Manyoljin tugukab talbisto ne berber;
Kotam nee anyun ngele bou otwogindet werikab laitoriat.*

Katika mfano huu, sehemu, *‘ngele bou otwagindet weritab’* yaani ‘ikiwa mtumwa atatawala mwana wa’. Maneno haya hayakuweko kwenye M.A lakini yakaongezwa kwenye M.P ili kutoa maelezo zaidi. Maelezo haya yanasaidia wasomaji wa M.P kuelewa vyema ujumbe uliokusudiwa katika M.A

5.3 Udondoshaji wa Sehemu za M.A katika Tafsiri

Mkakati wa udondoshaji ni pale ambapo mtafsiri anaacha neno au maneno pasipo kutafsiri. Uamuzi huu hutekelezwa na mtafsiri mwenyewe baada ya kuona haja hiyo katika harakati yake ya kuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A katika lugha ya H.P. Mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil*, alitumia mkakati huu katika sehemu mbalimbali za M.P hii.

Mfano 27.

Mithali 1:17 **M.A** kwa kuwa mtego hutegwa bure,
Mbele ya macho ya ndege yeyote.

M.P *Kigirich mestet buch,
Kogeerei taritiet age tugul;*

Katika tafsiri hii, maneno ‘kwa kuwa’, yamedondolewa kwenye M.P

Mfano 28.

Mithali 1:19 **M.A** Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tamaa ya mali;
Huuondoa uhai wao walio nayo.

M.P *U noto ortinwekab age tugul ne kipkeiyat agobo kelunet;
Rebei sobonwekab bik.*

Katika tafsiri hii, maneno ‘walio nayo’ yameondolewa kwenye M.P na mtafsiri. Maneno haya yametumika kusesitiza kuwa wale wanaonyang’anywa uhai ni walio nayo, lakini msisitizo huu haujaonyeshwa kwenye M.P

Mfano 29.

Mithali 6:14 **M.A** Mna upotofu moyoni mwake, hutunga uovu daima,
Hupanda mbegu zamagomvi.

M.P *Mi mastaet muguleldannyi, chobei yaitiet ko tugul;
Kole toiyet.*

Sehemu iliyodondoshwa kwenye tafsiri ni ‘mbegu za’. M.A imetoa maelezo ya kina kuwa kila kinachopandwa ni mbegu, ndipo maana inazungumzia ‘mbegu za’. Lakini mtafsiri anaonekana kupuuza dhana ya ‘mbegu’ na hivyo kudondoa katika tafsiri yake.

Mfano 30.

Mithali 7:3 **M.A** Zifunge katika vidole vyako;
Ziandike juu ya kibao cha moyo wako.

M.P *Ratyi moriguk; Sirji muguleldong’ung’.*

Mtafsiri amedondosha maneno ‘juu ya kibao cha’ katika tafsiri yake. Labda kwa kuwa neno “kibao” ni geni katika lugha ya Kikalenjin na ingekuwa vigumu kuelewa msemu huu wa kuwa na ubao kwenye moyo wa mtu. Mtafsiri alidondosha msamiati huu ili kukwepa utata wowote usitokee.

Mfano 31.

Mithali 10:6 **M.A** Baraka humkalia mwenye haki kichwani;
Bali jeuri hufunika kinywa chake mtu mwovu.

M.P *Tebe kaberoik ne bo iman:
Ago tuhei koromnatet kutitab kiptengekyot.*

Katika M.P, neno ‘kichwani’ limesondolewa. Labda kwa sababu kitendo cha kukalia hufanyika ‘kitini’ wala si ‘kichwani’, ndiyo maana mtafsiri akaamua kukitupilia mbali kwa kutolitafsiri hili neno.

Mfano 32.

Mithali 16:27 **M.A** Mtu asiye faa kitu huchimba shimo la madhara;
Katika midomo yake mna moto uteketezao.

M.P *Chobei yaitiet chito ne matilei kiy;*
Ak mitei kutinnyi kit ne u mat ne beelesei.

Kwenye tafsiri hii, neno ‘shimo’ halijatafsiriwa, kwa kuwa tafsiri ‘*chobei yaitiet chito ne matilei kiy*’ kwa maana ya ‘mtuasiyefaa kitu hutengeneza madhara’. Neno ‘*chobei*’ limetumika kwa maana ya ‘huchimba’. Kwa hivyo ni dhahiri kuwa mtafsiri ameacha sehemu nyingine ya sentensi hii bila kutafsiri, na kuondoa uzito uliobebwa na sentensi. Udondoshaji huu umepotosha ujumbe wa mwandishi wa M.A.

Mfano 33.

Mithali 24:30 **M.A** Nilipita karibu na shamba la mvivu
Na shamba la mzabibu la mtu asiye akili.

M.P *Kiabun mbaretab chito ne choriren,*
Ak olenegite mbaretab sabibuk ne bo chichoto matinyei naet;

Katika M.P mtafsiri anaonekana kudondosha neno ‘karibu’ yaani ‘*ole negitee*’ katika tafsiri yake. Hata hivyo, matini hii haijapoteza ujumbe ulioko kwenye M.A kwa kuwa cha muhimu ni uwezo wa kuona. Kwa hivyo alichooona ni muhimu, wala si mahali anapoonea kwa kupita karibu na shamba au kwa kupita shambani. Kwa hali hizi zote, la muhimu ni kwamba kwa kupitia pale, alimwona mwenye njaa.

Mfano 34.

Mithali 25:21 **M.A** Adui wako akiwa ana njaa, mpe chakula;
Tena akiwa na kiu, mpe maji ya kunywa.

M.P *Ngo am rubet bunyondeng’ung’, ibai;*
Ak ngo am melel, inage koe.

M.A imebainisha dhahiri kuwa cha kumpa anywe ni maji, lakini mtafsiri anakosa kulitafsiri hili neno. Sababu ya kulidondosha hili neno ni kwa kuwa katika jamii ya

Wakalenjin, kuna maneno yanayotumiwa kubainisha ni kinywaji gani kinachozungumziwa. Hivi kwamba wanaposema *'koe'* ina maana ya kuteremsha maji kupitia kooni, hasa kwa minajili ya kukata kiu. Neno hili halitumiki kwa kutajia unywaji wa vinywaji vingine isipokuwamaji. Hii inasababisha mtafsiri kutotafsiri neno 'maji' kwa kuwa atakuwa kama anajirudia, maana akisema *'koe'*, atakuwa amewasilisha dhana ya 'kunywa maji'.

Mfano 35.

Mithali 27:2 **M.A** Mwingine akusifu wala si kinywa chako mwenyewe.
Mtu mgeni wala si midomo yako wewe.

M.P *Ingolosun age, amelasuge*
Ingolosun toondet, amelasuge

Mtafsiri wa M.P ameonekana kudondosha sehemu za sentensi hizi. Kwa mfano, katika sehemu ya kwanza; *ingolosun age, amelasuge*, kwa maana 'wacha mtu mwingine akusifu wala usijisifu', *'ingolosun toondet, amelasuge'*, kwa maana, 'usijisifu ila mgeni akusifu'. Katika sentensi ya kwanza, maneno haya: 'kinywa chako mwenyewe' yameondolewa na kisha neno 'usijisifu' likatumika. Katika sentensi ya pili, maneno; 'midomo yako mwenyewe' yamedondoshwa na badala yake, neno 'amelasuge', yaani 'usijisifu' likatumika. Udondoshi huu umenuiwa kukwepa kujirudia katika M.A. Maanake kule kujisifu kunatokana na matumizi ya kinywa au midomo. Ili kukwepa kujirudia, mtafsiri akaonelea kutumia neno *'amelasuge'* kwa maana ya 'usijisifu'.

Mfano 36.

Mithali 30:7 **M.A** Mambo haya mawili nimekuomba; usininyime (matatu) kabla sijafa.

M.P *Kasomin tuguk aeng'; Amat ietena kotom amee:*

Katika kutafsiri kifungu hiki, mtafsiri ameacha sehemu ya '(matatu)' na hivyo kufutilia mbali sehemu hii kabisa. Mtafsiri anaonekana kukusudia katika kuidondoa sehemu labda kwa kuwa imetiwa kwenye mabano. Lakini katika kifungu kinachofuata ndipo inabainika kuwa ni mambo matatu wala si mawili aliyotaka asinyimwe.

Mfano 37.

Mithali 30:8 **M.A** Uniondolee ubatili na uongo; Usinipe umasikini walautajiri; Unilishe chakula kilicho kadiri yangu.

M.P *Iste koloogitu eng' ane, tangoita ak lembechek: Amegona bananda anan magornatosiek; Baena amitwogik che yama:*

Katika orodha ya mambo haya, mtafsiri anataja mambo matatu kama alivyotaja mwandishi wa M.A, ilhali ametangulia kwa kusema ni mambo mawili ambayo angetaka yaondolewe kutoka kwake, ila kwenye mabano tunaona kuwa ameashiria kuwa ni mambo matatu. Mtafsiri naye amendondoa neno lililotiwa katika mabano na hivyo kusababisha shaka kwa msomaji wa M.P kwa kuwa ameorodhesha mambo matatu kinyume na anavyosema kuwa ni mambo mawili.

Mfano 38.

Mithali 30:9 **M.A** Nisije nikakusahau, Nikasema BWANA ni nani?
Wala nisiwe maskini sana nikaiba,
Na kulitaja bure jina la Mungu wangu.

M.P *Si mabiye ak aesien, ak ale, Ng'o Jehovah
Anan si maegu kibanania, ak achorse,
Si mamwa kainetab Kamuktaindennyu eng' tangoi.*

Katika tafsiri hii, neno 'sana' halijatafsiriwa. Mwanandishi wa M.A ametumia hili neno kwa minajili ya kuleta msisitizo wa hali ya umasikini, lakini mtafsiri amelidondosha. Udondoshaji huu umefanya tafsiri kutokuwa na uzito kama ilivyo
M.A

Mfano 39.

Mithali 31:27 **M.A** Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake
Wala hali chakula cha uvivu.

M.P *Ribei komie atebosiekab bikab gonnyi,
Ama amei che bo charirnatet.*

Katika matini hii, mtafsiri amedondosha neno ‘chakula’ katika tafsiri yake. Udondoshaji huu unapelekea kuwe na upungufu wa welewaji wa M.P kama alivyokusudia mwandishi wa M.A. Hali hii inatokana na kutolewa kwa sehemu muhimu katika kifungu hiki. Neno ‘chakula’ ndilo kiini katika sentensi hii. Linapodondoshwa, ujumbe katika M.P unadhoofika. Neno ‘*amei*’ yaani ‘kula’ katika jamii ya Wakalenjin huweza kuchukuana na maneno tofautitofauti ili kuleta maana mbalimbali. Kwa mfano, ‘*amei amitwogiki*’ ina maana ya ‘kula chakula’, ‘*amei emoo*’ ina maana ya ‘kubarizi’, ‘*amei metit*’ ina maana ya ‘anaumwa na kichwa’ na kadhalika. Kutokana na mifano hii, ni wazi kuwa neno ‘chakula’ halingeondolewa kwenye tafsiri kwa kuwa linabeba uzito katika kuwasilisha ujumba kama alivyokusudia mwandishi wa M.A.

5.4 Ufafanuzi wa Ujumbe wa M.A katika Tafsiri

Mkakati huu unahusu hali ambapo mtafsiri katika kutafsiri matini, hufafanua dhana fulani hasa kutokana na hali kwamba amekosa kisawe chake L.P. Ufafanuzi huu huhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi wa M.A unamfikia msomaji wa M.P bila kupotosha maana iliyokusudiwa. Mkakati huu kwa hivyo, haulengi kutafsiri neno baada ya jengine ilakutafsiri ujumbe wa M.A. Mifano ifuatayo inatuonyesha jinsi mtafsiri alivofanikiwa kwa kutumia mkakati huu.

Mfano 40.

Mithali 1: 20 **M.A** Hekima hupaza sauti yake katika njia kuu.
Hutoa sauti yake katika viwanja;

M.P *Waachei mising' ng'omnatet eng' oret;
Ng'alali eng' komoswek che baraen.*

Katika tafsiri hii, neno 'viwanja' limetafsiriwa kama '***komoswek che baraen***', yaani, 'sehemu zilizo pana'. Mtafsiri anapotumia sentensi kutafsiri neno hili, ananua kufafanua maana ya neno hili ambalo labda amekosa neno kisawe chake. Ili kueleweka kwa H.P, imemlazimu basi kulifafanua neno hili na hivyo kulifanya kueleweka vyema. Tunaona mkakati huu wa ufafanuzi ukitumika pia katika kifungu kifuatacho:

Mfano 41.

Mithali 7:12 **M.A** Mara yu katika njia kuu, mara viwanjani,
Naye huotea kwenye pembe za kila njia.

M.P *Mi oret ra, komi tun komaswek che baraen,
Ak soptai eng' ole besiechin ortinwek.*

Neno 'viwanjani' limetafsiriwa hapa pia kama '***komaswek che baraen***', kwa maana ya 'sehemu zilizo pana'. Katika vifungu vinavyofuata, tunaendelea kuona mifano mingine ya maneno yaliyotafsiriwa kwa kutumia mkakati huu.

Mfano 42.

Mithali 5:5 **M.A** Miguu yake inatelemkia mauti;
Hatua zake zinashikamana na kuzimu;

M.P *Chorjingei kelyekik meet;
Namegei kakwautikyik ak oldab che kigobek.*

Neno 'kuzimu' halina kisawe chake katika lugha ya Kikalenjin na hivyo, likatafsiriwa kwa kulifafanua kama '***oldab che kigobek***' yaani;

Oldab – mahala pa

Che – kiwakilishi cha nafsi ya tatu wingi

Kigobek – walioisha (waliokufa)

Mfano 43.

Mithali 7:19 **M.A** Maana mume wangu hayumo nyumbani,
Amekwenda safari ya mbali.

M.P *Amu mami ga chitoab kobo got,
Kawa banda ne loo:*

Maneno ‘mume wangu’ yametafsiriwa kama ‘*chitab kobo got*’; ikiwa na maana ya ‘mtu mwenye nyumba’. Dhana hii ya kummiliki mume haipo miongoni mwa Wakalenjin. Mume huchukuliwa kama anayemiliki ‘nyumba’ ikiwa na maana kuwa mke, watoto na mali yote ni ya mume. Hii inapelekea jamii kumwita mume; hasa aliyeoa, kuwa ni ‘mwenye nyumba’. Katika sehemu hii, ni mke anayesema kuwa mume wake hayuko nyumbani. Mtafsiri ametafsiri hivi ili kuleta welewa miongoni mwa Wakalenjin, hasa kuonyesha nafasi ya mwanamume kama anavyochukuliwa na mke.

Mfano 44.

Mithali 8:25 **M.A** Kabla ya milima haijawekwa imara,
Kabla ya vilima nalizaliwa.

M.P *Ye kitomo kelumnda tulonok,
Kigisicha ye kitomo kobiit tulonok che mengechen.*

Kisawe cha neno ‘vilima’ hakipo katika lugha ya Kikalenjin. Hii ndio sababu mtafsiri aliamua kulifafanua hili neno kwa kutumia maneno yenye kuhifadhi ujumbe wa mwandishi wa M.A. Anatafsiri kama, ‘*Tulonokche mengechen*’ yenye maana ya, ‘milima midogo’. Ufafanuzi huu unaafiki maana ya ‘vilima’ kwa kuwasilisha dhana hiyo ya udogo.

Mfano 45.

Mithali 17:8 **M.A** Kipawa ni kama kito cha thamani machoni pake yeye aliye nacho;
Kila kigeukapo hufanikiwa.

M.P *U koita ne bo kamnutiet ne o,
kitab kagaigaet, eng’ taitab inendet ne tinyei;
Borei eng’ ui tugul ole tokyingei.*

Neno ‘kipawa’ limetafsiriwa kama ‘*kitab kagaigaet*’ yaani, ‘*kitu kinachofariji*’. Neno hili limekosa kisawe katika lugha ya Kikalenjin na kumfanya mtafsiri kulifafanua kwa maneno mengi. Anaposema ‘kitu chenye kufariji’, anaonekana kuonyesha hali ya jinsi anavyohisi mtu anapokuwa na kitu cha thamani; kuwa yeye hufarijika. Kwa kiwango fulani, mtafsiri anajaribu kuhifadhi ujumbe wa M.A anapolifafanua neno hilo, na kusababisha athari iliyo sawa na ile ya M.A.

Mfano 46.

Mithali 26:3 **M.A** Mjeledi kwa farasi, lijamu kwa punda,
Na fimbo kwa mgongo wa mpumbavu.

M.P *Ko u ye bo kipcharitit mbartanyit, ak ko u ye bo karnetab
kutit sigiriet, Ko u noto, bo kirokto chito ne berber.*

Mtafsiri anapokosa kisawe cha neno ‘lijamu’ katika lugha ya Kikalenjin, anaamua kulifafanua maana ya neno lenyewe. Anaposema ‘*karnetab kutit sigiriet*’ ana maana ya ‘*chuma kinachotiwa mdomoni mwa punda*’. Taswira inayojitokeza katika akili ya msomaji wa M.P, inamfanya afahamu hicho kichuma kinachoashiriwa na kwa hivyo hupata ujumbe uliokusudiwa kwenye matini.

Mfano 47.

Mithali 26:14 **M.A** Kama vile mlango ugeukavyo katika bawaba zake;
Kadhalika mtu mvivu katika kitanda chake.

M.P *Ko u ye weegegei kereiywotab kurget karikyik che namei;
Ko u noto weechegei chito ne choriren eng’ itogunnyi.*

Katika kifungo hiki tunaendelea kuona namna mtafsiri alivyotafsiri kwa kutumia mkakati huu wa kufafanua matini kama njia moja ya kutafsiri. Kwenye kifungu hiki, neno bawaba linakosa kisawe chake katika lugha ya Kikalenjin na mtafsiri analifafanua anaposema, ‘*karikyik che namei*’, kwa maana ya ‘*vyuma vyake vinavyovishikilia*’. Tafsiri hii ni ufafanuzi wa jinsi bawaba hufanya kazi; kwamba huwa na kazi ya kushikilia mlango katika sehemu yake. Maelezo haya hata hivyo japo

ni marefu, lakini msomaji wa M.P bila shaka atakuwa ameelewa mawasiliano hayo, kwa mujibu wa mtafsiri.

Mfano 48.

Mithali 28:15 **M.A** Kama simba angurumaye, na dubu mwenye njaa;
Ndivyo alivyo mtu mbaya awatawalaye maskini.

M.P *U ng'etundo ne boriseni ak tiondo ne u keerit ne ombenoti,
Bounindet ne ya ne bou kibananok.*

Mtafsiri ametafsiri neno 'dubu' kama '*tiondo ne u keerit*' kwa maana ya '*mnyama kamambweha*'. Tunaona kuwa neno hili halijatafsiriwa kwa kutumia neno lenye kisawe chake lakini badala yake, mtafsiri amelifafanua. Aidha hii inatokana na kuwa Wakalenjin hawakuishi mahali ambapo mnyama huyu hupatikana lakini wanamfahamu mbweha. Kwa hivyo ili kupelekea H.P kuelewa ujumbe huu, amemfananisha dubu na mbweha na hivyo kusaidia H.P kulielewa.

Mfano 49.

Mithali 30:23 **M.A** Mwanamke mwenye kuchukiza aolewapo;
Na mjakazi aliye mrithi wa bibi yake.

M.P *Ak kwondo ne kiwechei ye kagitun;
Ak chepto ne otwagindet ne tun bunjin tugukab kwondo
ne bou inendet.*

Maneno yaliyofafanuliwa hapa ni kama, 'mjakazi' ambalo limefafanuliwa kama '*chepto ne otwagindet*' yaani 'mtumishi ambaye ni msichana'. Tafsiri hii ni kutokana na kwamba, hadhira pokezi haingepata maana ya neno mjakazi kwa kuwa neno hili halipatikani katika jamii ya Wakalenjin kwa sababu hawakufanya biashara ya kuuza na kununua wanadamu. Na hivyo mtafsiri anaonelea kutumia neno mtumishi kwa kuwa halikuwa neno geni kwao. Vilevile, 'mrithi' limefafanuliwa kama '*ne tun bunjin*' yaani, 'atakayeachiwa'. Ufafanuzi huu unaafiki tamaduni za Wakalenjin kwamba mtoto wa kike hawezi kurithi ila hapa anaonyesha kuwa anaweza kuachiwa

vitu hivyo wakati bibi yake atakapoondoka ulimwenguni, wala si kama urithi bali ni kwa sababu ya kukosa mtu wa kurithi.

Mfano 50.

Mithali 31: 8 **M.A** Fumbua kinywa chako kwa ajili yake aliye bubu;
Uwatetee watu wote walioachwa peke yao.

M.P *Ng'alal agobo ne namat kut,
Agobo tugul che kagilakta kotebi ichegei.*

Katika sehemu hii, mtafsiri amefafanua neno 'bubu' kwa kusema, '**ne namat kut**', yaani 'yeye aliyefumbika kinywa'. Hii ni kwa sababu hakukipata kisawe cha neno hili katika lugha ya Kikalenjin na hivyo kutumia maelezo ili kufafanua kuwa bubu ni hali ya kutozungumza; yaani kufumbika kinywa. Maelezo haya hata hivyo yanafaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi wa M.A.

5.5 Urekebishaji wa Maelezo katika Tafsiri

Mkakati wa kurekebisha muundo wa vishazi hutokana na haja ya mtafsiri kuwasilisha dhana ileile ya mwandishi wa M.A lakini kwa namna ambavyo hatasababisha utata katika uelewekaji wa M.P. Hivyo huweza kubadilisha kishazi katika sentensi ili kukubaliana na lugha pokezi. Mkakati huu huhakikisha kuwepo kwa mtiririko wa matini katika lugha pokezi. Mifano ya sehemu zilizotafsiriwa kwa kutumia urekebishaji wa maelezo ni kama ifuatayo:

Mfano 51.

Mithali 1:15 **M.A** Uzuie mguu wako usiende katika mapito yao.

M.P *Iste keldong'ung' eng' orenywa.*

Tafsiri hii imerekebisha ujumbe wa M.A ambapo, kishazi 'uzuie mguu wako usienende' kimetafsiriwa kama, '**iste keldang'ung'** yaani, 'ondoa mguu wako'. Katika tafsiri, ujumbe wa mwandishi wa M.A umerekebishwa na kuzua dhana ya kuondoa mguu ilhali alimaanisha mguu kuzuiwa kabla ya kufika mahali fulani.

Kuondoa mguu ina maana kuwa mguu tayari upo mahali maalum na hivyo kuna haja ya kuuondoa. Urekebishaji huu unasababisha kuzaliwa kwa ujumbe tofauti na ule wa mwandishi wa matini asilia.

Mfano 52.

Mithali 5:15 **M.A** Unywe maji ya birika lako mwenyewe,
Na maji yenye kububujika katika kisima chako.

M.P *Ee beek che mi tereng'ung',
Ak iee beek cherootai eng' keringeng'ung'.*

Badala ya mtafsiri kulitafsiri neno birika, amerekebisha kwa kulitafsiri kama '*tereng'ung*' yaani 'chungu chako'. Neno birika halina mshiko miongoni mwa Wakalenjin ila chungu. Wao walitumia chungu kuhifadhi maji wala si birika. Hii ndio sababu ya mtafsiri kulichagua neno hili ili kuwafikia wasomaji wa M.P

Mfano 53.

Mithali 6:4 **M.A** Usiache macho yako kupata usingizi,
Wala kope za macho yako kusinzia.

M.P *Ameru,
Anan inuuch.*

Mtafsiri katika tafsiri yake, anaonekana kufanyia marekebisha utafsiri huu. Anaposema '**Ameru**' kwa maana ya 'usilale' na anaposema '**Anan inuuch**', ana maana ya 'wala kusinzia'. Hapa, ameacha maelezo mengine yanayopatikana katika M.A na hivyo kufupisha M.P. Ingawaje maneno mengine hayakutafsiriwa, tunaona kuwa ujumbe umekuzwa na hivyo msomaji wa M.P atapata ujumbe wa mwandishi wa M.A, japo kwa muhtasari.

Mfano 54.

Mithali 6:26 **M.A** Maana kwa malaya mtu hutiwa katika hali ya kuhitaji kipande cha Mkate; Na kahaba humwinda mtu anase nafsi yake iliyo ya thamani.

M.P Amu ibeeti chepkugoniot chito agoi kong'etyi kererutiet
Ak cheng'oti chepkugoniot koriich sobondo ne kararan.

Katika tafsiri hii, kishazi ‘yake iliyo na thamani’ kimetafsiriwa kama *‘ne kararan’* yaani, ‘iliyo ya kumpendeza au nzuri’. Mtafsiri hapa anaonekana kubadilisha kishazi hiki na kuleta dhana nyingine isiyodhihirisha hali yoyote ya ‘uthamani’ kama alivyodokeza mwandishi wa M.A. Lakini cha mno ni kwamba kitu cha thamani ni lazima kiwe kizuri. Hii ndiyo sababu urekebishwaji huu wa maelezo hauonekani kuleta utata wa ujumbe ingawa maneno yaliyoteuliwa na mtafsiri yanaonekana kutotafsiriwa neno kwa neno.

Mfano 55.

Mithali 7:11 **M.A** Ana kelele na ukaidi:
Miguu yake haikai nyumbani mwake.

M.P *Bolin ago ngelelio; Matononi eng’ gonnyi.*

‘Miguu yake haikai’ imetafsiriwa kama *‘matononi’* yaani ‘hatulii’. Katika tafsiri hii, dhana ya kutulia imelinganishwa na miguu kutokaa mahali pamoja. Inaonekana kana kwamba mtafsiri amelea dhana nyingine tofauti katika maelezo yake, lakini Mkalenjin atakuwa ameelewa ule ujumbe vilivyo.

Mfano 56.

Mithali 9:3 **M.A** Amewatuma wajakazi wake, analia,
Mahali pa mjini palipo inuka sana,

M.P *Kigoyokto tibikyik, waachei
Eng’ komoswek che tororen mising che bo nganaset,*

Mtafsiri amerekebisha neno ‘wajakazi’ kwa kulitafsiri kama *‘tibikyik’* lenye maana ya ‘binti zake’. Urekebishaji huu unatokana na kwamba katika jamii hii ya Wakalenjin, neno hili halina kisawe wala halina mshiko wowote kwa sababu hawakuwaajiri wafanyikazi. Wao waliamini katika kufanya kazi kwa pamoja na iwapo mtu angehitaji usaidizi, basi jamaa wake wangetoa usaidizi unaohitajika. Ili Wakalenjin wapate kuelewa dhana hii, mtafsiri aliitafsiri kwa kutumia kisawe kinachoeleweka kwa H.P. Anaporekebisha sehemu hii na kutumia ‘binti zake’, anafanya hivyo kwa nia ya

kuwasilisha ujumbe ulio sawa na ule wa M.A. Hii ni kwa sababu, watoto wa kike hufanya kazi ambayo wajakazi hufanya katika jamii ya Waswahili.

Mfano 57.

Mithali 12:4 **M.A** Mwanamke mwema ni taji kwa mumewe;
Bali aaibishaye ni kama kuoza mishipani mwake.

M.P *Egu kwondo ne mie konditab manong'otiondenyi:
Ago kwondo ne ibu kalilinet ko u nunatet eng' kowekab
chichoto.*

Kishazi 'mwanamke mwema ni taji' kimetafsiriwa kama '*egu kwondo ne mie kondit*' kwa maanaya 'mwanamke mwema atakuwa heshima'. Urekebishaji huu umetokana na hali kwamba mtu hupewa taji kama ishara ya kuheshimiwa. Mtafsiri ametafsiri matokeo ya mtu kupata taji kuwa ni kwa sababu ya kuheshimiwa kwa kitendo fulani. Kwa hiyo, mwanamke katika jamii ya Wakalenjin anapoheshimu mumewe, humfanya akaheshimike na hivyo akapewa sifa nzuri ambayo ni sawa na kupokea taji. Mtafsiri hapa anaonekana kutafsiri kwa kujiegemeza katika undani wa maelezo hayo kama inavyoeleweka katika jamii ya M.P.

Mfano 58.

Mithali 27:4 **M.A** Ghadhabu ni kali, hasira gharika:
Lakini ni nani awezaye kusimama mbele ya wivu.

M.P *Korom nereknatet, koromen mising' neregek;
Ago ng'o ne imuchi kotonon eng' taitab ng'etkonda?*

Katika tafsiri hii, mtafsiri anaposema, '*koromen mising' neregek*' yaani, ghadhabu ni kali sana, ni kwamba amerekebisha tafsiri hiyo kwa kurudia kishazi cha kwanza katika sentensi hii na kusisitiza tu kwa kutumia neno 'sana'. Urekebishwaji huu unafaa kwa sababu neno 'gharika' kama lingetafsiriwa halingewasilisha maana kamili kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa M.A.

Kwa ujumla, tumeona kuwa katika kutafsiri Biblia ya Kikalenjin, mtafsiri alitumia mikakati tuliyojadili kwa haja ya kupitisha ujumbe wa mwandishi wa M.A kwa hadhira pokezi ambao ni Wakalenjin. Urekebishaji huu umewezesha maneno yaliyo magumu kutafsiri katika lugha ya Kikalenjin kuelezwa kwa jinsi ilivyo rahisi kueleweka kwa H.P. Kama mikakati hii haingetumika, ingekuwa vigumu kwa tafsiri kupitisha ujumbe kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa matini asilia.

5.6 Ujumlishwaji wa Msamiati Husika katika Tafsiri

Ujumlishwaji huhusu hali ambapo mtafsiri katika kufanya tafsiri, hutumia neno moja lenye kujumlisha maelezo yaliyotolewa kwa marefu. Zifuatazo ni mifano ya sehemu zilizotafsiriwa kwa kutumia mkakati huu:

Mfano 59.

Mithali 6:25 **M.A** Usiutamani uzuriwake moyoni mwako;
Wala usikubali ukunase kwa kope za macho yake.

M.P *Amegase miat eng' muguleldang'ung' kororonindannyi;
Amengoriigenen konyekik.*

Mtafsiri ametumia neno jumuishi katika kutafsiri maneno 'kope za macho yake' anapotafsiri kama '*konyekyik*' kwa maana ya 'macho yake'. Tunaelewa kuwa kope ni nywele zinazozunguka macho. Lakini hapa, mtafsiri ameacha dhana hii na kutaja macho. Hata hivyo, hamna upungufu wowote katika tafsiri hii kwa kuwa ujumbe wa mwandishi asilia umebaki kwa sababu mtu hunaswa kwa kutazamwa, na kinachotumika kutazama ni macho. Kwa hali hii tafsiri hii ni sahihi.

Mfano 60.

Mithali 6:28 **M.A** Je! Mtu anaweza kukanyaga makaa ya moto,
Na nyayo zake zisiungue?

M.P *Imuch chi kotiegat ng'eteti, Ama lalyo kelyekyik?*

Nyayo ni sehemu ya chini ya kukanyaga wakati wakutembea. Lakini katika tafsiri, neno *'kelyekyik'* kwa maana ya, miguu yake, lililotafsiriwa kwa kutumia neno lenye maana jumuishi kwa kuwa linarejelea mguu, kuanzia magoti kwenda chini. Hili ni neno jumuishi wala sio bainifu kama ilivyo neno lililotumika katika M.A. Hata hivyo, kwa kutumia neno jumuishi, hamna athari yoyote kwa kuwa linawasilisha ujumbe uleule wa M.A.

Mfano 61.

Mithali 9:17 **M.A** Maji yaliyoibiwa ni matamu,
Na mkate ulioliwa kwa siri hupendeza.

M.P *Anyiny beek che kechorei,
Ak kororon amitwogik che keamei eng' ung'ot.*

Katika tafsiri hii neno 'mkate' halina kisawe chake katika lugha ya Kikalenjin. Hii ndiyo sababu mtafsiri ametumia neno *'amitwogik'* lenye maana ya 'chakula', neno ambalo ni jumlishi kwa kuwa halibaini ni chakula cha aina gani kama inavyobainika katika M.A. Hata hivyo, maana ya ujumbe haijapotoshwa kwa namna yoyote kwa kuwa ujumbe umewafikia walengwa kwa njia inayoeleweka.

5.7 Hitimisho

Sura hii imechunguza mikakati iliyotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Kutokana na uchanganuzi huu, imebainika kuwa ili kufanikiwa kwa tafsiri ya Biblia hii, mikakati zaidi ya moja ilitumika. Mikakati hii ilimwezesha mtafsiri kuhifadhi ujumbe wa mwandishi wa M.A na kuhakikisha kuwa H.P inaathirika kwa namna sawa na wasomaji wa M.A. Nadharia ya tafsiri vitendo imefaa katika uteuzi wa mikakati hiikwani nadharia yenyewe inasisitiza athari ya ujumbe uliotafsiriwa iwe sawa na ile ya M.A kwa hadhira yake.

Katika sura hii tumeona kuwa kuna uandishi upya wa M.P kama alivyodahili mtaalamu Justa Holz-Monttari katika nadharia yake ya tafsiri vitendo. Anaposema kuwa lengo la mtafsiri si kuwasilisha maneno tu yaliyo sawa na yale yaliyoko kwenye M.A. Mtafsiri ana jukumu kuu la kuhakikisha kuwa H.P inapokea ujumbe wa mwandishi wa M.A. Isitoshe, mtaalamu huyo amependekeza kuwa mtafsiri awe anaelewa utamaduni wa H.P ili awafikie katika utafsiri wake. Jambo hili limedhihirishwa katika matumizi ya mikakati mbalimbali aliyochagua kutumia. Mikakati hii ilichangia katika kumfikia msomaji wa M.P kwa namna ambayo matini itaeleweka na kuzua athari sawa na ilivyo M.A kwa H.A.

Justa Holz-Montarri katika nadharia yake alisisitiza umuhimu wa tafsiri kuwa ni kuwasiliana kati ya watu wenye tamaduni tofauti. Kwa hivyo, mtafsiri anafaa kuwa ni daraja la kuwaunganisha wanajamii hawa. Hali hii inaonekana dhahiri katika uchanganuzi uliopo katika sura hii. Mtafsiri ametumia mikakati tofauti tofauti ili kuhakikisha kuwa anasababisha mawasiliano yakamilike. Kando na hayo, ni kuhakikisha kuwa M.P inatekeleza dhima na makusudi iliyokuwa katika M.A na iliyokusudiwa na mwandishi wa M.A. Haya yote yamewezekana kupitia kwa kuandika upya M.P

SURA YA SITA

MBINU ZILIZOTUMIKA KATIKA KUTAFSIRI *BUKUIT NE TILIL*

KUTOKA KWA BIBILIA TAKATIFU YA KISWAHILI

6.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia matokeo ya uchunguzi kuhusiana na mbinu zilizotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Mbinu za kutafsiri ni njia zinazotumiwa na mtafsiri kubadilisha ujumbe uliomo katika Biblia Takatifu ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A bila kupotosha ujumbe. Hii inapelekea mtafsiri kumakinika sana anapoteuwa mbinu ya kutumia ili kuhakikisha kuwa ujumbe unahifadhiwa na kumfikia msomaji wa M.P kwa namna iliyo rahisi kueleweka. Katika utafiti huu, mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil* alitumia baadhi ya mbinu za kutafsiri ambazo ni pamoja na tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Uchanganuzi huu umeonyesha mifano mbalimbali ya matini pamoja na mbinu za kutafsiri zilizotumika katika kutafsiri sehemu hizo.

6.1 Mbinu Zilizotumika Kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*

Kutokana na uchunguzi huu, ilibainika kwamba mtafsiri alitumia mbinu zaidi ya moja katika kutafsiri Biblia Takatifu ya Kiswahili hadi *Bukuit Ne Tilil* ya Kikalejin. Mbinu hizi kwa kweli ni njia mwafaka zilizohakikisha kuwa M.A inahawilishwa hadi kuwa katika lugha ya pili pasipo kuwa na upungufu unaoweza kuonyesha kuwa kazi ile si asilia. Pamoja na kuifanya M.A iweze kusomeka katika lugha pokezi, ni muhimu pia kuboresha uhawilishaji huo kwa namna ambavyo itaweza kuvutia H.P kwa kuwafanya wajumuike katika uelewekaji. Ili kufaulu basi, mtafsiri atalazimika kutafuta njia mwafaka za kutekeleza kazi hiyo; nayo ni kuchagua mbinu za kutafsiri

zitakazokimu mahitaji ya tafsiri. Biblia ya Kikalenjin ilitafsiriwa kwa kutumia mbinu tatu kuu, kama zilivyochanganuliwa katika sehemu ifuatayo.

6.1.1 Tafsiri ya Neno kwa Neno

Hii ni tafsiriambayo kwayo, mofimu na maneno hufasiriwa yakiwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za msingi bila kujali muktadha. Mpangilio wa mofimu na maneno ya lugha asilia hubaki vilevile, yaani haubadiliki. Maneno yanayofungamana na utamaduni hufasiriwa kisisisi. Matini ya tafsiri, yaani M.P, huandikwa chini ya matini ya lugha asilia, yaani M.A. Kwa mfano;


Mfano 1 **Kiswahili:** Alilala hadi asubuhi.
English: He/she slept until morning

Mfano 2 **Kiswahili:** Walikwenda kupiga maji wakarudi hoi
English: They went to beat water they return helpless

Kutokana na mifano hii, ni bayana kuwa mtafsiri hutafsiri neno baada ya neno pasi na kuzingatia muktadha wa neno. Hali hii wakati mwingine, hasa kama maana ya neno inaathiriwa na mazingira, huchangia katika kupotosha ujumbe wa mwandishi wa M.A. Katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*, mtafsiri ametumia mbinu hii kwa asilimia kubwa hasa kwa kutafsiri zile sehemu ambazo welewa wake ni wazi na hauhitaji kuzingatia muktadha maalum ili kukamilisha maana yake. Katika sehemu inayofuata, nimechanganua vifungu mbalimbali vya Biblia, yaani kifungu kimoja katika kila sura ya kitabu cha Mithali. Sura nyingine zilibainika kwa kutotumia tafsiri hii na hivyo sura kama hizo hazikuchanganuliwa. Uchanganuzi huu ulibaini kuwa maneno yaliweza kutafsiriwa neno moja baada ya jengine. Katika mifano ifuatayo, mishale imetumika kuonyesha jinsi kila neno lilitafsiriwa chini yake:

Mfano 62.

Mithali 1:1M.A Mithali za Suleimani, mwana wa Daudi, mfalme wa sraeli.




M.P *Kalewenaikab Solomon weritab Daudi, laitoriatab Israel.*

Mfano huu hapa unaonyesha kila neno la L.A lilivyotafsiriwa chini yake kwa L.P. Hii inaonyesha kuwa mpangilio wa sentensi za L.P wakati mwingine huweza kuwa sawa na ule wa L.A hasa wakati wa kutafsiri neno baada ya neno. Ila tunachoona katika mfano huu, ni kwamba kuna maneno mengine ya M.A yanayoweza kutafsiriwa kwa kutumia neno moja tu katika L.P. Kwa mfano ‘Mthali za’ ni maneno mawili yaliyotafsiriwa kama, ‘*Kalewenaikab*’ ambalo ni neno moja tu. Mwendelezo huu huandikwa kama neno moja ila ndani ya hili neno kuna maneno mawili yaliyokutanishwa; *kalewenoik-Mithali*, na *ab-za*.


Mifano 63.

Mithali 3:2M.A Maana zitakuongezea wingi wa siku.




M.P *Amu tesun choto chang'indab betusiek,*

Na miaka ya uzima, na amani.




Ak kenyikiekab sobet, ak kalyet.

Mithali 4.2 M.A Kwa kuwa nawapa mafundisho mazuri;



M.P *Amu agonok konetisiet ne mie;*



Mifano hii hapa juu inaonyesha hali ambayo neno moja la L.A limetafsiriwa kwa maneno mawili katika L.P yaani, neno ‘mazuri’ limetafsiriwa kama ‘*ne mie*’. Maneno ‘sheria yangu’ yametafsiriwa kwa kutumia neno moja, *ng'atutiennyu*. Tunachukulia hii kuwa ni tafsiri ya neno kwa neno kwa kuwa hali ilivyo katika sintaksia ya L.P ni kwamba sharti maneno hayo mawili yatenganishwe na wakati mwingine yaunganishwe kuwa neno moja ili kutoa maana ileile ya neno la L.A.

Katika mifano ifuatayo, nimeendelea kuonyesha baadhi ya vifungu vilivyotafsiriwa kwa kutumia mbinu hii. Itabainika katika mifano hii kuwa kila neno limetafsiriwa chini yake kwa kutumia kisawe chake katika lugha pokezi. Wakati mwingine maneno mawili hutumika kupitisha dhana ile iliyoko katika neno moja kwenye lugha husika. Tazama mifano hii hapa chini:

Mfano 64.

Mithali 5.31 M.A Lakini akipatikana, atalipa mara saba;


↓	↓	↓	↓	↓
M.P Ago	<i>ngot kenyor,</i>	<i>kogeeri</i>	<i>konyil</i>	<i>tisab;</i>

M.A Atatoa mali yote ya nyumba yake.

↓	↓	↓	↓	↓
M.P Igoitoi	<i>tuguk tugul</i>	<u><i>che bo</i></u>		<i>gonnyi.</i>


Katika mfano wa 64, tunaona neno ‘akipatikana’ limetafsiriwa kwa kutumia maneno mawili ya L.P, yaani, *ngot kenyor*. Neno la Kiswahili ‘ya’ limetafsiriwa kwa kutumia maneno mawili ya L.P, *che bo*. Vilevile, maneno mawili ya Kiswahili, yaani, ‘nyumba yake’ yametafsiriwa kwa kutumia neno moja katika M.P yaani, *gonnyi*.

Mfano 65.



Neno la Kiswahili, 'nikaona' limetafsiriwa kwa kutumia maneno mawili ya Kikalenjin, *ak kiager*. Vilevile, neno 'wajinga' limetafsiriwa kwa kutumia maneno mawili, *che abusanik*. Neno la Kiswahili, 'nikamtambua' limetafsiriwa kama, *ak kianyit*, na maneno 'asiyekuwa na' yakatafsiriwa kama, *matinyei*.

Mfano 66.



Katika mfano huu hapa juu ni kuwa neno la Kiswahili ‘kama’ limetafsiriwa kwa manenomawili ya Kikalenjin, *ngot ko*. Huku neno ‘una’ limetafsiriwa kama *ko i*. Hali kadhalika manenomawili ya L.A yalitafsiriwa chini yake kwa neno moja la L.P, yaani, ‘nafsi yako’ ilitafsiriwa kama *neng’ung*, ‘una dharau’ ikawa *ichotisiei*, huku ‘peke yako’ ikawa *inyege*.

Mfano 67.

Mithali 10:15 M.A Mali ya tajiri ni mji wake wa nguvu;
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
 M.P *Magornatetab mogoriot ko nganasennyi ne kim:*

M.A Uangamivu wa maskini ni umaskini wao.
 ↓ ↓ ↓ ↓
 M.P *Ng’emisietab kibananok ko banandanywa.*

Mithali 12:1 M.A Kila apendaye mafundisho hupenda maarifa;
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
 M.P *Age tugul ne chamei kotigonet kochamei naet*

M.A Bali yeye achukiaye kulaumiwa ni kama mnyama.
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
 M.P *Ago inendet ne esioi keretab kong’ko u tiondo.*

Mithali 14:24 M.A Taji ya wenye hekima ni mali zao;
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
 M.P *Chepkuletak che ng’omen ko magornatosiekwak:*

M.A Bali upumbavu wa wajinga ni upumbavu tu.
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
M.P Ago berberindab che berber ko berberindo kityo

Mithali 16: 8 M.A Afadhali mali kidogo pamoja na haki,
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
M.P Kaigai tuguk che matia koboto imanda

M.A Kuliko mapato mengi pamoja na udhalimu.
 ↓ ↓ ↓ ↓ ↓
M.P Kosiir kelunaik che chang' koboto kertaetab kong'.

Mfano 67 ni kundi la vifungu zaidi vya kitabu cha Mithali vinavyodhihirisha matumizi ya mbinu hii ya kutafsiri neno kwa neno katika kuhawilisha ujumbe wa L.A hadi L.P.Aidha, kutokana na uchanganuzi huu, ilibainika kuwa maneno mawili ya Kiswahili huweza kuunganishwa na kuwa neno moja la Kikalenjin, na kwingineko, neno moja la Kiswahili huweza kutafsiriwa kwa maneno mawili ya Kikalenjin. Maneno kama hayo yametiliwa mstari ili kuonyesha kuwa yanaunganishwa ili kutoa maana ya neno moja ambalo limeonyeshwa na ishara ya mshale. Ingawaje maneno mawili yametumika kuhawilisha maana ya neno moja, ni kweli kuwa ni tafsiri ya neno kwa neno kwa kuwa tafsiri yake ipo chini ya hilo neno.

Aina hii ya tafsiri imetumika kwa wingi katika kutafsiri sehemu nyingine za kitabu cha Mithali ingawaje kuna baadhi ya sura ambazo hazikutumia mbinu hii, hasa katika kutafsiri kifungu kizima. Sura ambazo hazikutumia mbinu hii kutafsiri kifungu kizima ni pamoja na sura ya 2,5,8,11,13,15,19,22,27 na 28. Hizi ni sura kumi kati ya jumla ya sura 31 katika kitabu cha Mithali. Idadi hii ni takribanthuluthi moja ya kitabu kizima

cha Mithali. Hata hivyo, haina maana kuwa vifungu hivi havikutumia kabisa mbinu hii, ila mbinu hii imechanganywa na mbinu nyingine. Mbinu hii ya kutafsiri ilionekana kuhifadhi ujumbe wa mwandishi wa M.A kwa kuwa haikuathiriwa na miktadha yoyote. Kwa hivyo, mbinu ya neno kwa neno imeonekana kuungwa mkono na nadharia ya ulinganifu sambamba. Nadharia hii imeelezea kuwa umbo la neno linaweza kubadilika lakini ujumbe utasalia kuwa ule ule. Maneno yanapobadili umbo kama tulivyoshuhudia katika uchanganuzi wa mifano ya hapo juu, maana ya ujumbe imehifadhiwa. Ujumbe unapohifadhiwa, basi na athari zake zinakuwa sawa na za M.A.

6.1.2 Tafsiri ya Kisemantiki

Katika mbinu hii, mfasiri hutafsiri kila neno katika sentensi jinsi lilivyo lakini kwa kufuata sarufi ya L.P. Katika mbinu hii, mkazo huwekwa kwenye maana ya matini kama ilivyokusudiwa na mwandishi. Haisahihishi au uboreshwajihaupo. Tafsiri hii basi huwa ngumu kidogo kueleweka, haina maonjo, ina mshindilio wa taarifa na inamfikirisha sana msomaji badala ya kumpatia ukweli wa taarifa papo hapo.

Faida ya tafsiri hii ni uwezo wake mkubwa wa kuendeleza lugha pokezi kwa kuingiza miundo ya misemo kutoka kwenye lugha asilia. Kwa mfano:

<i>Good day</i>	–	Siku njema
<i>Ladies and gentleman</i>	–	mabibi na mabwana
<i>Yours loving</i>	–	mimi nikupendaye
<i>Honourable speaker</i>	–	mheshimiwa spika
<i>It was reported that</i>	–	ilielezwa kuwa

Upungufu wa tafsiri hii ni kwamba haitilii maanani nahau na misemo maalum inayohusiana na utamaduni na misimamo ya lugha inayolengwa katika tafsiri. Katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*, mtafsiri alitumia mbinu hii katika sura zote za Mithali. Uchanganuzi huu, umetumia vifungu kumi tu vilivyotafsiriwa kwa kutumia mbinu hii ilikuwakilisha sura zote, yaani kuanzia sura ya kumi hadi kumi na tisa. Mifano

ifuatayo inaonyesha namna ilivyo mipangilio ya maneno katika sentensi za L.A na jinsi mipangilio hiyo ilivyo katika M.P . Nambari imetumika kuonyesha ilivyo katika M.A na nambari hizi zinaonekana jinsi zinavyobadili nafasi katika M.P.

Mfano 68.

1 2 3 4 5
Mithali 10:10 M. A Akonyezaye kwa jicho huleta masikitiko;

6 7 8 9 10 11
 Bali mpumbavu mwenye maneno mengi ataanguka.

4 5 1-2 3
M.P *Ibu arogenet ne ng'wegisie konda:*

6 11 7 8 10 9
Ago ibuti ne berber ne chang' ng'alek.

Katika tafsiri hii, maneno yamechanganywa katika M.P na mpangilio uliomo katika M.A haupo tena kwa kuwa kisemantiki, mpangilio wa maneno katika lugha hizi haufanani. Katika M.A 1 ni neno moja huku ikiwa ni maneno mawili katika M.P. Vilevile, katika M.P sehemu ya neno 1 ya M.A hugawanywa kuwa maneno mawili kisha sehemu ya mwisho ikakutanishwa na neno 2 ili kuwasilisha neno moja. Hiyo ndiyo sababu neno 1 na 2 katika M.A huwa neno mojakatika tafsiri yake kwenye M.P. Katika mfano huu na zile za 69 hapo chini, inaonyesha kuwa katika tafsiri ya kisemantiki, maneno yalivyopangwa katika M.A huwa hayaambatani katika mfululizo huo huo kwenye M.P.

Mfano 69.

1 2 3 4 5
Mithali 11:3 M.A Ukamilifu wao wenye haki utawaongoza

6 7 8 9 10 11
 Bali ukaidi wao wenye fitina utawaangamiza.

5 3 4 1 2
M.P *Indochin* che bo iman kagesunatenywa bo ge:

6 11 8 9 10 7
 Ago ng'emei che yaei kabersiet, kamaasenywa.

1 2 3 4 5 6
Mithali 12:3 M.A Mtu hatathibitika kwa njia ya uovu;

7 8 9 10 11 12
 Shina la mwenye haki halitaondolewa kamwe.

2 1 3 4-6 12 11 7-8 9 10
M.P *Magimitu* chi eng' yaitio: Amagoi kitut tigitotab che bo iman.

1 2 3 4 5 6
Mithali 13:4 M.A Nafsi ya mvivu hutamani asipate kitu;

7 8 9 10 11 12
 Bali nafsi ya mwenye bidii itanenepeshwa.

4 1-2 3 5 6
M.P *Tinyei maget* sobondab ne choriren ,ak manyoru kiy:

7 12 8-9 10 11
 Ago nereii sobondab ne igiilegei.

1 2 3 4
Mithali 14:5 M.A Shahidi mwaminifu hatasema uongo;

56 7 8 9 10 11 12
 Bali shahidi wa uongo, pumzi zake niuongo.

3 4 1 2
M.P Mamwaei lembech baoriat ne kiyani:

5 9-12 6 7 8
 Ago mwaiei lembech baoriat ne ma bo iman.

1 2 3 4 5 6
 Mithali 15:10 **M.A** Adhabu kali ina yeye aiachaye njia;

7 8 9 10
 Naye achukiaye kukemewa atakufa.

3 1 2 4 5 6
M.P Mi kotigonet ne ng'wan eng' inendetne metoi oret:

7 10 8 9
 Ak meei inendet ne wechei keretab kong'.

1 2 3 4
 Mithali 16:20 **M.A** Atakayelitafakari neno atapata mema:

5 6 7 8 9 10
 Na kila amwaminiye BWANA ana heri.

3 4 1 2
M.P Nyoru mieindo ne epchin it ng'olyot:

5 9-10 6 7 8
 Ak baibai age tugul ne imang'u Jehovah.

1 2 3 4 5 6 7
 Mithali 17:20 **M.A** Mtu mwenye moyo wa ukaidi hatapata mema;

8 9 10 11 12 13 14 15
 Na mwenye ulimi wa upotofu huanguka katika misiba.

6 7 1 2 5 10
M.P Manyoru kiy ne mie inendet ne imaasat muguleldo:

8 13-14 15 9 10 11 12
 Ak *ibutyin yaitiet* ne tinyei *ngelyepta ne imaasat.*

1 2 3 4
 Mithali 18:2 **M.A** Mpumbavu hapendezwi na ufahamu;

5 6 7 8 9
 Ila moyo wake udhihirike tu.

2-3 1 4
M.P *Maboiboitune* ne berber *kaguiyet,*

5 8 9 6-7
 Ago *ibortogei kityo muguleldonyi.*

1 2 3 4 5 6
 Mithali 19:24 **M.A** Mtu mvivu hutia mkono wake sahanini;

7 8 9 10 11 12
 Ila hataki hata kuupeleka kinywani pake.

3 4 6 1 2
M.P *Unyei eunnyi* eng' tabet *chito* ne choriren,

7 8 10 11-12 9
 Ama *chamei konde kutinnyi kogeny.*

Katika mfano 69 hapo juu, vifungu kumi vilivyochaguliwa kutoka kitabu cha Mithali vilichanganuliwa. Kutokana na uchanganuzi huu, ni dhahiri kuwa mtiririko wa maneno katika L.A ni tofauti wakati mwingine na ulivyo katika L.P. Hali hii hupelekea tafsiri ya kisemantiki kuwa inayofaa kuliko ile tafsiri ya neno kwa neno. Sarufi ya L.P lazima itiliwe maanani na mtafsiri ili matini iliyotafsiriwa iweze kueleweka kwa H.P. La sivyo, ujumbe wa mwandishi wa M.A utapotoshwa kabisa

kwenye tafsiri. Vilevile, katika mfano 69 iliyochanganuliwa hapa juu, tuliona kuwa nambari zilizotiwa juu ya maneno ya M.A zilibadili mpangilio wake katika M.P. Hii ina maana kuwa mpangilio mpya unafaa kutumika katika tafsiri ili kuhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi wa M.A unahifadhiwa na kuifikia hadhira inayolengwa.

Mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilit* alitumia mbinu hii kutafsiri sura zote za kitabu cha Mithali, sura zote zilitumia mbinu hii katika vifungu vyake mbalimbali. Mbinu hii ilichangia kuhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi wa M.A unawafikia walengwa. Hii ilitokana na kwamba M.P iliweza kuwasilishwa kwa njia ambayo kisarufi, ilikubaliana na lugha pokezi, na kufanya H.P kuielewa matini hii kama lugha yao.

6.1.3 Tafsiri ya kimawasiliano /huru/sabilia

Tafsiri hii humlenga msomaji wa M.P ambaye hatarajii ugumu wowote katika matini atakayosoma, bali hutarajia tafsiri nyepesi ya dhana za kigeni katika utamaduni na lugha yake kila inapolazimu na kwa kadiri inavyowezekana. Mtafsiri ana uhuru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, utamaduni na mazingira ya L.P. Hufuata sarufi ya L.P, mwelekeo wake wa jamii, historia, kiutamaduni na kimazingira. Kwa mfano:

Betty married John – John alimwuo Betty
He drinks like hell – anakunywa kupindukia
No need to cry over spilt milk – maji yakimwagika hayazoleki

Tafsiri hii hutoa athari ileile iliyokuwa katika M.A kwa hadhira pokezi. Tafsiri hii hutumika kutafsiri mambo au mawazo ya kigeni katika lugha na mazingira mapya. Mawazo ambayo huelezwa katika misingi ya lugha, utamaduni na mazingira yanayoeleweka kwa wasomaji wa L.P

Upungufu hutokea iwapo mfasiri hataegemea kwenye mawazo, historia, utamaduni, mazingira na itikadi ya L.P. Endapo mtafsiri atatumia mbinu hii kwa wingi, ina maana

kuwa wasomaji wa M.P wana uwezo wa kuelewa vizuri M.P kwa sababu maelezo yanatambua miktadha wa hadhira pokezi. Mbinu hii ilitumika sana katika Biblia ya Kikalenjini. Sura zote zilitumia mbinu hii kutafsiri takriban nusu ya kitabu hiki cha Mithali. Mifano kumi imetolewa hapa kubainisha matumizi ya mbinu hii.

Mfano 70.

Mithali 21:27 M.A Sadaka ya wasio haki ni chukizo;
Si zaidi sana ailetapo mwenye nia mbaya!

M.P *Kit ne kiwechei korosiotab kiptengeginik:
Kotam nee anyun ye ibu korosiondonoto,
Kotinyei kabwatutik che yaach!*

Katika mfano huu, mtafsiri ametumia maneno *kotinyei kabwatutik che yaach?* (akiwa na mambo mabaya), ili kutoa maelezo kuhusu mtumwenye nia mbaya kuwa yeye huwa na ‘mafikira maovu’ na kumpelekea kuwa na ‘nia mbaya’. Haya ni maelezo yanayotolewa kwa H.P ili wapate kuelewa ujumbe wa mwandishi wa M.A kwa njia rahisi kuliko kutumia tafsiri ya neno kwa neno ambayo labda ingemkanganya msomaji kwa kutozingatia muktadha.

Mfano 71.

Mithali 22:27 M.A Kama huna kitu cha kulipa;
Kwani ukaondolee kitanda chako chini yako.

M.P *Ngot ko metinye che iyaaktoe,
ko amu nee anyun si koibenen itogung’?*

Maneno ‘kitanda chako chini yako’ yametafsiriwa kwa kutozingatia maneno ‘chini yako’. Haya yamesababishwa na mtafsiri kulenga kuwasiliana na H.P na hivyo hamna haja ya kunukuu kila neno; kwani akishatumia neno moja ‘*itogung*’, kwa maana ya ‘kitanda chako’, basi atakuwa amewasiliana na H.P.

Mfano 72.

Mithali 23:16 M.A Naam,viuno vyangu vitafurahi,
midomo yako inenapo maneno mema.

M.P *Ee, boiboitu muguleldanyu,
ye kemwa tuguk che bo iman.*

Boiboitu muguleldonnyu ni maneno yaliyotumika kutoa dhana ya ‘viuno vyangu vitafurahi’. Kwa kweli, neno ‘viuno’ likitafsiriwa lilivyo hadi lugha ya Kikalenjin, basi maana itakuwa imepotoka na isiyofaa kwa muktadha wa kufurahi. Basi ili kuonyesha hali ya kufurahi, mtafsiri ametumia neno ‘**muguleldonnyu**’ kwa maana ya ‘moyo wangu’. Tafsiri hii inakuwa fasaha zaidi kwa H.P kwa kuwa inawawezesha waelewe zaidi makusudi ya mwandishi wa matini hii.

Mfano 73.

Mithali 24:24 M.A Amwambiaye mtu mvivu, wewe una haki;
Kabila za watu watamlaani, taifa watamchukia.

M.P *Inendet ne mwachin kiptengekyot, kolenjin, i bo iman;
Kochubei bik inendet, wechei bororiosiok inendet.*

Katika mfano huu, tafsiri hii imeelekea kuwasiliana na H.P kwa namna ambavyo sehemu ya ‘mtu mvivu’ imetafsiriwa kwa neno *kiptengekyot* (mtenda dhambi). Hapa inaonekana kuwa neno tofauti kabisa na lile la M.A. Lengo la mtafsiri hapa ni kuhakikisha kuwa amewasiliana na H.P kwa kuwa mtu wa ‘kulaaniwa’ au ‘kuchukiwa’, ni yule atendaye jambo baya ambalo katika muktadha wa neno la Mungu, basi huyo mtu ni ‘mtenda dhambi’. Hiyo ndiyo sababu sehemu hii inapotafsiriwa hivi, ina lengo la kuifikia hadhira na kuiathiri kwa jinsi sawa na ilivyo katika M.A.

Mfano 74.

Mithali 25:28 M.A Asiyetawala roho yake ni mfano wamji uliobomolewa,
usio na kuta.

M.P *U nganaset ne kigebut amatinyei irimet,
chito ne maribegei.*

Maneno ‘asiyetawala roho yake’ yametafsiriwa kwa kutumia neno moja **maribegei**, kwa maana ya ‘asiyejilinda’. Mtafsiri hapa ameacha maneno mengine na kutumia hili

neni tu akiamini kuwa H.P itaelewa ujumbe huu; Kwamba mtu asiyejitunza ni sawa na mtu asiyetunza roho yake. Hata hivyo, anapoacha maneno mengine analenga kuwasiliana na H.P.

Mfano 75.

Mitahli 26:10 M.A Fundi stadi hufanyiza vitu vyote;
Bali amwajiriye mpumbavu ni kama awajiriye watu wapitao.

M.P *U mwogindet ne iguoteni tugul;*
Inendet ne sirei ne berber anan che siirtoi, koboisiechi.

Katika mfano huu sehemu ya kifungu, yaani ‘fundi stadi hufanyiza vitu vyote’, kimetafsiriwa kwa namna tofauti kabisa katika M.P. Kwani maneno *U mwogindet neiguoteni tugul* yana maana ya ‘Ni kama msasi anayewajeruhi wote’. Labda kwa sababu Wakalenjin ni watu waliojijhusisha sana na usasi, basi aliona ni bora kulinganisha mfano huu na msasi ambaye ni hodari na huweza kusaka mawindo na kuwajeruhi wote kwa sababu ana ustadi. Badala ya kutumia ‘fundi’ ambalo ni geni katika jamii ya Wakalenjin ambao hawakujishughulisha sana ufundi kama ilivyo usasi.

Mfano 76.

Mithali 27:2 M.A Mwingine na akusifu wala si kinywa chako mwenyewe;
Mtu mgeni wala si midomo yako wewe.

M.P *Ingolosun age, amelosuge; Ingolosun toondet, amelosuge.*

Mtafsiri katika kutafsiri sehemu ya ‘kinywa chako mwenyewe’ ametumia maneno *amelosuge*, kumaanisha ‘usijisifu’. Hakutafsiri ‘midomo’ kwa kuwa alichukulia kuwa mtu anayejisifu hufanya hivyo kwa kutumia midomo. Kwa hivyo anapotumia hili neno moja, anaamini kuwa amewasiliana na H.P bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa M.A.

Mfano 77.

Mithali 28:15 **M.A** Kama simba angurumaye, na dubu mwenye njaa;
Ndivyo alivyo mtu mbaya awatawalaye maskini.

M.P *U ng'etundo ne boriseni ak tiondo ne u keerit ne ombenati,
bounindet ne ya ne bou kibananok.*

Katika tafsiri hii, mtafsiri ametoa maelezo ya 'dubu mwenye njaa' kama mnyama anayefanana na mbweha anayetangatanga, yaani *tiondo ne u keerit ne ombenati*. Maelezo haya ya kumfananisha dubu na mbweha ni kwa makusudi ya kuieleweshwa H.P kwa kuwa mbweha ni mnyama anayefahamika kwa H.P kuliko dubu. Dhana ya kutangatanga imesaidia ili kuleta taswira ya mnyama aliye na njaa ambaye hatulii ila hujishughulisha kutafuta chakula; yaani hutangatanga huku na kule ili kujitafutia riziki. Maelezo haya ya kina ni kwa minajili ya kukamilisha mawasiliano katika M.P.

Mfano 78.

Mithali 29:14 **M.A** Mfalme awahukumuye maskini kwa uaminifu;
Kiti chake cha enzi kitathibitika milele.

M.P *Kigimiti agoi koigeny laitornatetab laitoriat
Ne iruokyin kibananok eng' imanda.*

'Kiti chake cha enzi' kimetafsiriwa kama 'utawala wa mfalme', yaani '*laitornatetab laitoriat*'. Tafsiri hii imewakilisha ujumbe wa M.A kwa kuwa mfalme anayetawala ndiye aketiye katika kiti cha utawala. Hivyo katika tafsiri, neno 'kiti' halikuzingatiwa na kutafsiriwa kwa namna hiyo kwani utawala utakuwa umewasilisha maana ya neno hilo.

Mfano 79.

Mithali 30:23 **M.A** Mwanamke mwenye kuchukiza aolewapo;
Na mjakazi aliye mrithi wa bibi yake.

M.P *Ak kwondo ne kiwechei ye kagitun;
Ak chepto ne otwogindet ne tun bunjin tugukab kwondo
ne bou inendet.*

Sehemu ya pili ya kifungu hiki imetafsiriwa kwa kutumia maelezo marefu ili kutoa picha hasa ya maana ya neno ‘mjakazi’ kwamba ni ‘msichana’ yaani *chepto*. Kwamba atarithi kutoka kwa ‘bibi anayemtawala’, yaani, *kwondo ne bou inendet*. Maelezo haya yanasaidia msomaji wa M.P kuelewa vyema kama alivyoelewa hadhira wa M.A. hivyo kufanikisha mawasiliano.

6.2 Hitimisho

Katika sura hii, tumechunguza mbinu zilizotumiwa na mtafsiri wa Biblia ya Kikalenjin katika tafsiri yake. Tulibaini kuwa mtafsiri alitumia mbinu za neno kwa neno, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Kitabu cha Mithali kilidhihirisha matumizi ya tafsiri ya kisemantiki na ya kimawasiliano kwa kiwango cha juu kwa kuwa kila sura ilitumia aina hizi mbili za tafsiri kwa wingi zaidi. Hata hivyo, tafsiri ya neno kwa neno haikutumika katika sura zote za kitabu hiki. Ingawaje, vifungu vingine katika kitabu hiki vilitafsiriwa kwa kuchanganya mbinu zaidi ya moja. Lakini kijumla ni kwamba mbinu tatu pekee ndizo zilizotumika katika kutafsiri kitabu cha Mithali kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin.

Mbinu hizi zilichangia katika kuwasilisha ujumbe wa M.A kwenda kwa H.P. Kama wanavyopendekeza Holz- Manttari na Nida katika nadharia zao. Kwamba, mtafsiri ana jukumu la kupitisha ujumbe wa mwandishi wa matini asilia kwa hadhira pokezi bila ya kupoteza maana. Kwa kutumia nadharia hizi, mtafsiri wa *Bukut Ne Tilit* aliwajibika katika kuhakikisha kuwa anahifadhi ujumbe wa M.A. Makusudi ikiwa ni kuhakikisha kuwa M.P inatekeleza dhima na jukumu lililokusudiwa na mwandishi wa matini asilia.

SURA YA SABA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Utangulizi

Kuanzia sura ya nne hadi ya sita, nimechanganua vifungu vinavyobainisha uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil* ambayo ni Biblia ya lugha ya Kikalenjin, iliyotafsiriwa kutoka kwa 'Biblia Takatifu' iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Masuala yaliyopelekea Biblia hii ya Kikalenjin kutafsiriwa kwa namna ambayo inakuwa uandishi upya, yameangaziwa katika sura hizo tatu. Sura hii ya saba inalenga kutoa hitimisho la utafiti huu na kutoa mapendekezo ya mtafiti.

Utafiti ulilenga kuchunguza namna tofauti za kitamaduni baina ya Waswahili na Wakalenjin zilivyosababisha tafsiri kuandikwa upya. Vilevile ilikusudia kutathmini jinsi mikakati mbalimbali iliyotumiwa na mtafsiri wa *Bukuit ne Tilil* ilivyosababisha kuwepo kwa uandishi upya kwenye matini tafsiri. Isitoshe, mtafiti katika utafiti wake alikusudia kuchunguza mbinu mbalimbali zilizotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Mwisho, utafiti huu ulichunguza iwapo mbinu hizi zililetea kazi tafsiri hii ionekane kama uandishi upya wa matini asilia.

Utafiti ulikusudia kuchanganua matini ya *Bukuit Ne Tilil* huku ikilinganisha na yale yaliyomo kwenye M.A, ambayo ni Biblia Takatifu, na hivyo kuweza kueleza mambomuhimu ya kitamaduni yaliyobainika kwenye kazi tafsiri. Mikakati iliyotumika vilevile ilianguziwa na mtafiti ili kubaini jinsi ilitumika katika kila kifungu kwenye kitabu cha Mithali. Katika kuchunguza huku, aliweza kubaini mikakati mbalimbali iliyotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Utafiti huu hususan, ulitambua aina kadha za mbinu zilizotumika wakati wa kuhawilisha matini na ujumbe uliomo kwenye M.A kwenda kwenye M.P

7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Sura ya kwanza ya tasnifu hii imeangazia misingi ya utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti na nadharia tete za utafiti. Isitoshe, sura hii imetuonyesha sababu za mtafiti kuichagua mada hii na kuitafiti. Vilevile, mtafiti ameonyesha katika sehemu hii umuhimu wa kutekeleza utafiti huu, kisha akakamilisha kwa kuonyesha upeo wa utafiti.

Mapitio ya maandishi pamoja na misingi ya kinadharia yameangaziwa kwenye sura ya pili. Sura ya tatu nayo imeangazia mbinu zilizotumika kutekeleza utafiti huu, namna data ilikusanywa na kuchanganuliwa, na baadaye kueleza changamoto zilizokabili utafiti huu. Sura ya nne imeangazia jinsi vipengele vinvavyohusiana na utamaduni vilivyotafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kikalenjin. Vipengele hivi vya kitamaduni vilichunguzwa ili kubaini jinsi mtafsiri alivyokabiliana navyo katika harakati ya kutafsiri.

Mikakati mbalimbali ilitumika na mtafsiri ili kuhakikisha kuwa anafikia malengo yake ya kupitisha ujumbe wa mwandishi asilia kwa hadhira pokezi. Sura ya tano ndiyo iliyoonyesha mikakati hii kwa kina. Nayo sura ya sita imeshughulikia mbinu zilizotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil* kutoka kwa Biblia Takatifu ya lugha ya Kiswahili. Tumetamatisha kwa sura hii ambayo imejadili matokeo ya utafiti huu na kutoa mapendekezo ya utafiti. Aidha, sura hii imekamilika kwa mtafiti kutoa mapendekezo yake kuhusu tafiti za baadaye.

7.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa kile mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil* alichokuwa akifanya katika kutafsiri hii Biblia kilikuwa kuiandika upya Biblia hii. Uandishi upya haukuweza kuepukika kwa kuwa lugha hizi zilikuwa ni tofauti kwa namna

mbalimbali. Mtafiti angalidumisha kutafsiri moja kwa moja yale maelezo ya lugha ya Kiswahili hadi kwa lugha ya Kikalenjin, labda ujumbe ungebadilika au kupotea kabisa.

Matokeo ya utafiti huu yamegawanywa kulingana na malengo ya utafiti kama yanavyobainika katika sehemu inayofuata:

7.2.1 *Bukuit Ne Tilil* kama uandishi upya wa Biblia Takatifu kutokana na tofauti za kitamaduni

Lengo la kwanza katika utafiti huu lilikuwa kuchunguza jinsi tofauti za kitamaduni kati ya Waswahili na Wakalenjin zilivyochangia katika uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*. Vifungu katika kitabu cha Mithali vilichanganuliwa ili kubaini jinsi dhana za kitamaduni zilivyotafsiriwa. Vipengele mbalimbali vya kitamaduni vilibainika katika matini tafsiri hii. Kwa mfano, utafsiri wa vyakula, jinsia, taasubi ya kiume, mazingira na hata mila na desturi.

Katika kutafsiri aina ya vyakula, ilibainika kuwa katika utamaduni wa Wakalenjin, nyama ya ng'ombe ilichukuliwa kuwa ni aina ya chakula cha thamani. Wakalenjin wanapokuwa na shereheyoyote muhimu, wao humchinja ng'ombe. Isitoshe, ng'ombe hutumika kutolea mahari. Utamaduni huu ulichangia kuathiri tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil*. Pale ambapo neno nyama lilipohitaji kutafsiriwa, walitumia neno *teta* (ng'ombe) kama tafsiri yake. Katika kufanya hivi, mtafsiri alikuwa analiandika upya hili neno na kuufanya utafsiri huu kuwa uandishi upya.

Dhana ya mkate imetafsiriwa kama *amitwogik* (chakula). Neno chakula ni la jumla katika lugha ya Kiswahili. Mtafsiri, alitafsiri kwa kutumia neno hili linalojumlisha aina zote za vyakula kwa kuwa katika utamaduni wa Wakalenjin, hawakuwa wanaoka

mikate. Chakula hiki kilikuwakigeni na hivyo kutafsiri kwake kulipelekea mtafsiri kutumia dhana hii ya jumla ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A.

Isitoshe, Wakalenjin hawakulima nafaka aina ya ngano katika ukulima wao, badala yake, wao aghalabu walipanda wimbi na kujishughulisha na ufugaji. Katika Biblia Takatifu, neno ngano limetajwa lakini mtafsiri katika kulitafsiri neno hili, alitumia neno *bek* (wimbi), ili Wakalenjin wapate kuelewa ujumbe kama ulivyokusudiwa na mwandishi wa M.A. Kueleweka huku kunakamilika lakini mtafsiri atakuwa ameandika upya matini hiyo, hasa kwa kuingiza neno tofauti na lile linalotumiwa na Waswahili.

Kuhusiana na jinsia, mtafsiri alijikita katika utamaduni wa Wakalenjin katika kutoa tafsiri ya neno, 'mwana'. Kulingana na lugha ya Kiswahili, mwana ni mtoto wa jinsia ama ya kike au kiume. Katika kulitafsirineno hili kwa lugha ya Kikalenjin, neno *werit* (mwana wa kiume) lilitumika katika vifungu vyote vya kitabu cha Mithali. Utamaduni wa Wakalenjin unampa hadhi mtoto wa kiume zaidi kuliko wa kike. Hali hii inapelekea mtafsiri kupuuza maana ya neno hili kama linavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili na kisha akalitafsiri kama linavyokubalika katika utamaduni wa Wakalenjin. Yaani, badala ya kutumia neno *lakwet* (mtoto), ametumia *werit* (mtoto wa kiume). Uandishi upya huu, ulitumiwa na mtafsiri kwa makusudi ya kuleta ukubalifu miongoni mwa H.P. Ukubalifu huu pia unawezesha H.P kupata ujumbe wa mwandishi wa M.A kama alivyokusudia.

Taasubi ya kiume ni jambo jengine lililojitokeza katika uchunguzi huu. Utamaduni wa Wakalenjin unatukuza jinsia ya kiume kuliko ya kike. Mambo mengi mema na makuu yanahusishwa na jinsia ya kiume huku wanawake mara nyingi wakihusishwa na mambo hasi na ya kudhalilisha. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha ukweli huu.

Mfano mzuri ni matumizi ya neno ‘malaya’. Katika lugha ya Kiswahili, neno hili linaashiria jinsia zote, yaani, anaweza kuwa wa kiume au wa kike. Katika utafiti huu, tulipata kuwa malaya huchukuliwa kuwa ni mwanamke pekee wala si mwanamume miongoni mwa Wakalenjin. Ndipo neno *chepkugoniot* (malaya ambaye ni mwanamke) lilitumika. Mtafsiri alilazimika kutafsiri hivi ili kukubalika miongoni mwa Wakalenjin wanaochukulia kuwa mwanaume anapofanya mapenzi popote na jinsi apendavyo, hashutumwiwi, lakini jambo hili halikubaliki miongoni wa wanawake. Hivyo, mwanamke pekee ndiye anaweza kuchukuliwa kama malaya wala si mwanamume.

Mtafsiri vilevile, alijiegemeza katika utamaduni wa Wakalenjin katika kuonyesha jinsi mwanamke anadunishwa na utamaduni. Wakati Biblia Takatifu ya Kiswahili inazungumzia ‘mtu ajipendekezaye’, mtafsiri naye anatafsiri kama *chemwai gut* (mwanamke ajipendekezaye). Tendo la kujipendekeza linahusishwa moja kwa moja na mwanamke wala si mwanamume katika jamii ya Wakalenjin. Mtafsiri amehifadhi taasubi ya kiume katika tafsiri yake ili matini haya yakubalike miongoni mwa Wakalenjin ambao katika utamaduni wao, wanawake mara nyingi hubeba sifa hasi, wala si wanaume.

Utamaduni wa Wakalenjin pia umebainisha kuwa rasilimali yote ya jamii ni ya mwanamume wala si mwanamke, na hata wanawake wanalifahamu hilo. Kwa mfano, mwanamume anaelezwa kama mwenye kumiliki nyumba wala si mwanamke. Mtafsiri anapoyatafsiri maneno ‘mume wangu’, anaandika kama *chitab kobo got* (Mtu mwenye nyumba). Hii inaashiria kuwa utamaduni wa Wakalenjin unamtambua mume kama mwenye kumiliki mali katika familia ikiwemo nyumba. Mwanamke hana cha kumiliki kwa kuwa hata yeye anamilikiwa na mumewe. Mtafsiri alipaswa kuandika

upya kazi yake ili iambatane na utamaduni wa H.P ambayo ni Wakalenjin. Uandishi upya huu, unasababisha wasomaji ambao ni Wakalenjin, kukubali maandishi haya na kuchukulia kama ni yao, kwa kuwa yamehifadhi utamaduni wao.

Wakalenjin ni watu wanaopatikana katika maeneo ya bara, huku Waswahili wakipatikana katika maeneo ya pwani. Tofauti hii ya kimazingira iliathiri tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil*. Mtafsiri kwa kuwa alitaka kuwafikia Wakalenjin, ilimbidi atafsiri kwa kuandika upya matini tafsiri, ili kuhakikisha inaafiki mazingira ya Wakalenjin. Tunaona haya anapotafsiri neno ‘changarawe’, ambapo anatunia neno *koik* (mawe). Ingawaje ametumia neno tofauti na lile la Kiswahili, lakini la muhimu ni kuwa amewafikia Wakalenjin ambao kutokana na mazingira yao, wanafahamu mawe kuliko changarawe. Mazingira haya yalipozingatiwa na mtafsiri, akaishia kuandika upya matini tafsiri ili kufaulu katika kupitisha ujumbe wa mwandishi wa M.A.

Mila na desturi pia zilizingatiwa katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Mtafsiri anaonyesha haya katika kutafsiri neno ‘kuchinjwa’. Kulingana na mila na desturi ya Wakalenjin, binadamu hachinjwi ila mnyama. Neno hili linapotumika kuashiria kuuawa kwa mwanadamu kwa njia ya kikatili, mtafsiri anaandika upya kwa kutumia neno *kebar* (kuua) ili kuondoa ukali uliopo katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na jamii ya Wakalenjin, kinachochinjwa kinaweza kulika kwa mfano mnyama. Lakini mwanadamu hawezi kuchinjwa kwa kuwa haliwi. Vilevile, neno ‘kijakazi’ lilitafsiriwa upya kwa kuandika neno tofauti na la M.A. Mtafsiri alitumia neno *tibiguk* (binti zako) kwa kuwa mila ya Wakalenjin hawakuruhusu hali ya ujakazi. Mtu angeweza kuishi na binti asiye wake kana kwamba ni mtoto wake. Hali ya utumwa haikuwepo miongoni mwa Wakalenjin. Mtafsiri kwa kuelewa hali hii, ilibidi atafute neno lingine mbadala litakaloafiki utamaduni wa Wakalenjin.

Wakalenjin, katika mila na desturi yao, walipendelea kumchinja ng'ombe dume katika sherehe zao mbalimbali. Katika kutafsiri Biblia kwa Wakalenjin, mtafsiri alikuza desturi hii. Tunaona kuwa badala ya mtafsiri kutafsiri neno 'ng'ombe' kama *teta*, alitumia neno *eito* (ng'ombe dume), kwa kuwa si kawaida wao kumchinja ng'ombe wa kumkamua kwa maana ya kuwa huyo ndiye hulisha familia kutokana na maziwa. Ilikuwa ni kawaida kwa Mkalenjin kumchinja ng'ombe dume na utamaduni huu unakuzwa katika tafsiri hii. Hali hizi za kitamaduni ndizo zilizosababisha mtafsiri kuandika upya M.P.

7.2.2 Mikakati ya kutafsiri na uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*

Lengo la pili katika utafiti huu lilikuwa ni kutathmini namna mikakati iliyotumiwa na mtafsiri ilivyopelekea kuwe na uandishi upya katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil*. Iidhihirika kuwa wakati mtafsiri anatafsiri, hutumia mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa anafaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi wa M.A kwa H.P kama inavyohitajika. Mikakati hii hata hivyo ilibainika kuwa ilipelekea uandishi upya kwa namna zifuatazo:

Mkakati wa kwanza ni utohozi, aghalabu wa nomino. Mtafsiri alipojaribu kutafutia kisawe cha neno la Kiswahili kwa lugha ya Kikalenjin, na kukosa kabisa, basi alitumia mkakati huu. Ambapo alitohoa baadhi ya maneno ya Kiswahili kwa kuzingatia fonolojia ya Kikalenjin na kisha kuiandika kwa kutumia mofolojia ya Kikalenjin. Mfano, maneno 'taa' linatafisiriwa kama *tait*, 'theluji' inakuwa *teluchi*, 'Israeli' inakuwa *Israel* na mengine mengi. Utohozi huu ni bayana kwamba maneno mapya yanaingizwa katika msamiati wa lugha ya Kikalenjin na hivyo kupelekea uandishi upya wa matini pokezi. Lengo la mtafsiri ni kufikisha ujumbe wa mwandishi asilia kwa hadhira pokezi kwa namna ambayo M.P itaonekana kama ndiyo M.A.

Mtafsiri alitumia pia mkakati wa upanuzi wa msamiati katika kutoa maana ya maneno. Mtafsiri alionekana kutumia mkakati huu kwa kutafsiri maneno ya Kiswahili hadi kwa lugha ya Kikalenjin. Mtafsiri alitafsiri neno moja kwa kutolea maelezo kwa mapana akitumia maneno zaidi ya moja. Vilevile, alitumia idadi ya maneno zaidi ya yale yaliyomo kwenye M.A ili kuleta welewa zaidi kwa H.P. Mfanokatika neno; ‘hakika’ limetafsiriwa kama *agot ngo namgei eunek*. Maneno haya yalitumika ili kutoa msisitizo ulioko kwenye hilo neno la Kiswahili. Kwa kukosa neno moja lililo kisawe cha hili neno, mtafsiri alitumia mkakati huu wa kupanua maelezo yanayohusiana nayo ili kuleta mawazo yaleyale ya M.A.

Udondoshaji wa sehemu za M.A katika M.P ulitumika katika kutafsiri *Bukuit ne Tilil*. Mkakati huu ulitumika pale mtafsiri alipoona hamna haja ya kulitafsiri neno au maneno fulani. Kwa mfano, tafsiri ya maneno, ‘ziandike juu ya kibao cha moyo wako’ yalitafsiriwa kama, *sirji muguleldong’ng* (ziandikie moyoni mwako). Maneno ‘juu ya kibao cha’ yalidondoshwa wakati wa kutafsiri. Ingawaje maneno haya yalidondolewa katika M.T, ni kwamba maana haijaondolewa kwa namna yoyote. Mfano mwingine ni katika maneno; ‘tena akiwa na kiu, mpe maji ya kunywa’ yalitafsiriwa kama *ak ngo am melel, inage koe* (tena akiwa na kiu, mpe anywe). Katika tafsiri hii maneno, ‘maji ya’ yalidondoshwa, lakini maana ya kifungu hiki ilihifadhiwa. Kwa hivyo mkakati huu ulitumika pale ambapo mtafsiri aliona kuwa hata baada ya kuyadondosha maneno mengine, maana haingeathirika kwa namna yoyote.

Aidha, mtafsiri katika kutafsiri *Bukuit ne Tilil*, alitumia mkakati wa kufafanua ujumbe wa M.A katika tafsiri yake. Mtafsiri alichagua kutumia mkakati huu ili kukabiliana na hali ya kukosa kisawe mwafaka cha maneno yaliyotumika katika M.A.

Hivyo, alipotumia maelezo yenye kufafanua kile kilichotajwa katika M.A. Alihakikisha kuwa H.P inapata ujumbe wa mwandishi wa matini asilia kwa kufafanua huku. Mfano, maneno, ‘kabla ya vilima nalizawa’ tafsiri yake ikawa, *kigisicha ye kitomo kobiit tulong chemengechen* (nalizaliwa kabla ya kuwepo kwa vilima vidogo). Lugha ya Kikalenjin haina neno ‘vilima’ kwa kuashiria hali ya udogo. Mtafsiri katika kushughulikia tafsiri hii, alifafanua kwa kutumia ‘milima midogo’ ili kuonyesha udogo kwa sababu neno hili katika lugha ya Kikalenjin halina msamiati wa kuonyesha udogo. Mfano mwingine ulitokana na tafsiri ya, ‘mjeledi kwa farasi’, ‘lijamu kwa punda’ kuwa *ko u ye bo kipcharitit mbartanyit, ak ko u ye bo karnetab kutit sigiriet* (kama vile mjeledi ni kwa farasi, na kama ilivyo chumacha mdomo wa punda). Katika tafsiri hii, neno ‘lijamu’ halipatikani katika msamiati wa lugha ya Kikalenjin. Mtafsiri hivyo aliamua kufafanua maana yake: *karnetab kutit sigiriet* (Chuma cha mdomo wa punda). Kwa kutoa ufafanuzi huu, aliandika upya M.P ingawa ujumbe unawafikia walengwa ambao ni hadhira pokezi.

Mkakati mwingine uliobainika katika utafiti huu ni ule wa urekebishaji wa maneno na vishazi katika matini tafsiri. Ili kuhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi wa M.A unahifadhiwa, mtafsiri alitumia mkakati huu. Urekebishaji huu ulitokana na kwamba lugha ya Kikalenjin ilikosa kisawe cha neno linalopatikana katika lugha ya Kiswahili, kwa hivyo urekebishaji ulihusu kutafuta msamiati mwingine ambao ni tofauti na ule wa M.A lakini unawasilishajumbe ipasavyo. Mfano maneno, ‘unywe maji ya birika lako mwenyewe’ yalitafsiriwa kama, *Ee beek che mi tereng’ung* (unywe maji yaliyo chungu chako). Neno ‘birika’ limerekebishwa na kuwa ‘chungu’. Hata hivyo, uandishi upya huu haukuathiri ujumbe kwa namna yoyote ila tu neno lililotumika ni tofauti na lile la M.A. Mfano mwingine ni kama, ‘amewatuma wajakazi wake’ iliyotafsiriwa kama, *kigoyoktotibikyik* (amewatuma binti zake). Neno ‘wajakazi’

limerekebishwa kuwa *tibik* (binti). Ingawaje neno hili ni tofauti na lile la M.A, lakini limefaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi asilia.

Mwisho, ni mkakati wa kutumia msamiati jumuishi. Katika kutafsiri kutoka M.A kwenda M.P, mtafsiri alitumia msamiati jumuishi pale ambapo maneno yaliyotumika katika matini asilia yalitumika kuashiria kipande au sehemu ya dhana nzima. Maneno haya yaliandikwa upya kwa kutumia msamiati wenye maana tofauti ila maana hiyo huweza kusimamia maana ya mwandishi asilia. Kwa mfano maneno, ‘Na nyayo zake zisiungue’ yalitafsiriwa kama, *ama lalyo kelyekyik* (Miguu yake isiungue). Katika mfano huu, neno ‘nyayo’ limeandikwa upya kwa kutumia neno la kijumla *kelyek* (miguu), na kupuuza ukweli kwamba hii ni sehemu ya chini ya mguu. Mfano mwingine ni pale ambapo maneno, ‘na mkate ulioliwa kwa siri hupendeza’ yalitafsiriwa kama *ak kororon amitwogik chekeamei eng’ ung’ot* (na chakula kinacholiwa kwa siri hupendeza). Tulibaini kuwa neno ‘mkate’ linatafsiriwa kwa kutumia msamiati wa kijumla, yaani ‘chakula’. Ingawaje mtafsiri ameandika upya neno hili, tunakubali kuwa limefaulu katika kuhifadhi maana ya M.A bila kusababisha utata kwa H.P

7.2.3 Mbinu za kutafsiri na uandishi upya wa *Bukuit Ne Tilil*

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa la kuchunguza jinsi mbinu zilizotumiwa na mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil* zilivyosababisha M.P kuandikwa upya. Mtafsiri wa *Bukuit Ne Tilil* alitumia mbinu tofauti tofauti katika kutekeleza kazi yake. Mbinu hizi hata hivyo zilichaguliwa kukimu mahitaji ya kutafsiri vifungu katika kitabu cha Mithali na kuhakikisha kuwa ujumbe wa mwandishi wa M.A haupotoshwi. Mbinu za tafsiri zilizotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil* ni pamoja na; tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano.

Mbinu ya kutafsiri neno kwa neno ilibanika katika tafsiri ya *Bukuit Ne Tilil*. Mtafsiri alitumia mbinu hii kulitafsiri kila neno pekee pasipo kuathiriwa na vipengele vingine kama vile muktadha wa neno husika. Tafsiri aina hii ilisaidia katika uelewekaji wa neno kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa matini asilia, kwa kuwa kila neno lilitafsiriwa moja baada ya jingine. Mfano maneno, ‘Mithali za Suleimani mwana wa daudi, mfalme wa Israeli’ yalitafsiriwa kama, *kalewenaikab Solomon weritab daudi, laitoriatib Israel*. Pia, ‘afadhali mali kidogo pamoja na haki’ ikatafsiriwa kama, *kaigai tuguk cha matia koboto imanda*. Hii ni mifano tu ya tafsiri ya neno kwa neno katika kitabu cha Mithali. Mtafsiri alitumia mbinu hii katika kutafsiri baadhi ya vifungu kwa lugha ya Kikalenjin. Uandishi upya ulionekana katika mbinu hii ya kutafsiri kwa kuwa maneno mengine ya Kikalenjin hayaandikwi kwa mofolojia sawa na ya Kiswahili. Ililazimu kuwa maneno mengine yalikutanishwa ili kuwasilisha maana ya neno moja katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano maneno, ‘mithali za’ yalitafsiriwa kwa kutumia neno moja, yaani, *kalewenaikab* kwa sababu maneno hayo hukutanishwa kuwa moja kulingana na mofolojia ya Kikalenjin. Mwendelezo huu wa kufanya maneno mawili kuwa moja ndio uandishi upya wa M.P

Mbinu nyingine iliyotumika katika kutafsiri *Bukuit Ne Tilil* ni ile ya kisemantiki. Mbinu hii ni kinyume na ile ya neno kwa neno kwa kuwa maneno hayapangwi katika M.T kwa mpangilio sawa na ule wa M.A. Hii ni kutokana na tofauti za kisarufi baina ya Kiswahili na Kikalenjin. Tafsiri hii hata hivyo, ilizingatia maana inayowasilishwa katika kila sentensi, kisha tafsiri yake ikaandikwa kulingana na muundo wa sentensi wa lugha pokezi. Hii inasababisha maneno yapangwe katika M.P sambamba na semantiki yake. Kwa mfano mpangilio wa maneno yafuatayo, Adhabu (1) kali (2) ina (3) yeye (4) aiachaye (5) njia (6): Naye (7) achukiaye (8) kukemewa (9) atakufa (10). Tafsiri yake katika M.P ilipangwa kwa namna ifuatayo: Mi (3) kotigonet (1) ne g’wan

(2) eng' inendet (4) ne metoi (5) oret (6): Ak (7) meei (10) inendet (4) ne wechei (8) keretab kong'(9). Katika mfano huu, mpangilio wa maneno katika M.A ni 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10 lakini katika M.P, mpangilio huu unabadilika na kuwa 3, 1, 2, 4, 5, 6, 7, 10, 4, 8, 9. Ingawaje M.P imeandikwa upya kwa kuzingatia semantiki ya lugha pokezi, ilifaulu kupitisha ujumbe wa mwandishi wa M.A. Wakati mwingine, maneno kadha kama vile neno namba 4 limerudiwa mara mbili katika M.P. Hii ilisababisha uandishi upya katika matini tafsiri, kwa kuwa lugha hizi mbili ni tofauti kisemantiki. Mbinu hii ya tafsiri kama ilivyobainika ilipelekea kuwepo kwa uandishi upya katika matini tafsiri.

Tafsiri ya kimawasiliano au huru ni mbinu nyingine iliyotumiwa na mtafiri wa *Bukuit Ne Tilil*. Mtafsiri akitumia mbinu hii, alilazimika kutafsiri vifungu vya Biblia kwa kujiegemeza kwenye utamaduni, mazingira na hata tamathali za usemi za lugha pokezi. Mbinu hii ilijiegemeza hasa katika kuwasiliana na H.P kwa namna ya kipekee inayoafikiana na malengo ya mtafsiri kuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa M.A. Katika mbinu hii ya kutafsiri, mtafsiri alikuwa na uhuru wa kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na dhana za lugha asilia ili kuwasilisha ujumbe wa M.A. Mtafsiri alifuata mwelekeo wa jamii ya Wakalenjin, historia yao, utamaduni wao na sarufi ya lugha ya Kikalenjin katika kutafsiri. Kutokana na hali hii, mtafsiri aliishia kuandika upya M.P kwa sababu ya haja ya kuifikia H.P bila kuzua utata kwenye mawasiliano yake.

7.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatoa mchango wa kitaalamu kwa namna zifuatazo: Kwanza kabisa ni kuwa utafiti huu ulihusu tafsiri ya matini ya kimaandishi, hii ina maana kwamba

wataalamu mbalimbali ambao wanahusika na tafsiri za matini wanaweza kutumia matokeo ya utafiti huu ili kujipa mwelekeo zaidi hususan, wa kutekeleza tafsiri zao.

Aidha, kutokana na matokeo ya utafiti huu, tulibaini sababu za kuwa tafsiri ni uandishi upya wa matini asilia kwenye matini pokezi. Watafiti watakaotumia matokeo ya utafiti huu watanufaika katika tafiti zao kwa kuweza kutoa tathmini kuhusiana na ubora wa kazi tafsiri wanazoziangazia.

Matokeo ya utafiti huu yatawanufaisha watafsiri wa sasa na siku za usoni hasa wanaotafsiri Biblia katika lugha mbalimbali za kienyeji. Wataweza kuona umuhimu wa kutafsiri Biblia kwa makusudi ya kupitisha ujumbe wa mwandishi wa matini asilia kwa njia rahisi na yenye kukubalika kwa hadhira lengwa. Wanapofanya hivyo, H.P huweza kuipokea matini ilioandikwa kwa lugha yao na kufanya waiamini kwa kuwa wanaiona kama ni sehemu yao.

Jambo jengine ni kuwa, mashirika mengi humu nchini yanayotafsiri matini mbalimbali yatanufaika kutokana na kazi hii. Yataumia matokeo ya utafiti huu ili kupata mwelekeo wa jinsi ya kutumia mikakati mbalimbali ya kutafsiri ili kupata matokeo mema katika kazi zao. Aidha wataongozwa na baadhi ya mbinu zilizojadiliwa katika utafiti huu katika kuchangia ubora wa kazi zao.

Kwa kuwa utafiti huu ulihusu tafsiri ya matini takatifu, watafsiri wengine wa matini takatifu watanufaika kutokana na matokeo ya kazi hii. Watapata mwongozo utakaochangia katika kazi zao za kutafsiri. Ikizingatiwa kuwa Biblia ni matini takatifu, basi watafsiri hawa, watanufaika kutokana na matokeo kuhusu mwelekeo uliotumiwa na watafsiri wa *Bukuit Ne Tilit*. Watafanikisha azma yao ya kuhawilisha ujumbe wa matini asilia hadi kwa matini pokezi, bila kudhoofisha maana ya ujumbe uliokusudiwa.

Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwanufaisha wanafunzi katika vyuo mbalimbali, hasa wanaozamia somo la tafsiri. Wanaweza kutumia mapendekezo ya utafiti huu kuendeleza tafiti zao au hata kuzua mada zaidi za kutafiti. Hivyo, kuendelea kupanua taaluma hii ya tafsiri.

Mwisho ni kuwa, kutokana na Kiswahili kufanywa lugha rasmi nchini, kunahitajika watafsiri wengi watakaotafsiri makala mbalimbali zilizokuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Ili kufanikisha kazi zao, watafsiri hawa wanaweza kutumia matokeo ya utafiti huu ili kupata mwongozo wa kuzitekelezea kazi zao kwa wepesi, hasa kwa kuzingatia mikakati inayotumika katika kutafsiri na mbinu mbalimbali za utafiti. Hii itachangia katika kufanikiwa kwa kazi zao za tafsiri.

7.4 Mapendekezo ya Utafiti

Mapendekezo yanayowasilishwa hapa yanatokana na matokeo ya utafiti huu na yanalenga kuchangia katika kuimarisha taaluma ya tafsiri kwa lugha za kienyeji.

Mapendekezo ni yafuatayo:

- i) Sera za elimu kuhusiana na lugha za kienyeji zinafaa kutiliwa maanani ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata kuzielewa lugha zao za kienyeji. Jambo hili litahakikisha kuwa kazi zinazotafsiriwa hadi lugha za kienyeji zinapata wasomaji, la sivyo, ujumbe wa matini hizi hazitapata wasomaji wengi.
- ii) Mashirika yanayojishughulisha na tafsiriyanafaa kupanuliwa zaidi, kwa mfano katika kupewa uthamini, ili kuyawezesha kuzitafsiri matini nyingikatika lugha za humu nchini. Hii itawezesha wakenya kuzisoma makala hizi kwa lugha wanayoielewa vyema. Hili linapotendeka, inakuwa rahisi kuwafikia watu wengi zaidi.

- iii) Waandishi wa matini mbalimbali wanafaa kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuzitafsiri kazi zao ili kupanua hadhira yao. Kazi zinazotafsiriwa hupata wasomaji wengi watakaosoma kupitia lugha wanayoielewa na kuwa na umilisi kwayo.
- iv) Shirika la kutafsiri Biblia humu nchini linastahili kujikakamua zaidi kwa kuitafsiri Biblia hadi kwa lugha yenye wazungumzaji wachache humu nchini. Kwa kufanya hivi, wataweza kuwafikia watu wengi na injili ya Kristo. Huku kutimiza wito kwa Wakristo kutoka Mesiha Yesu kuwa: Enendeni kote ulimwenguni mkalihubiri injili (Mathayo 28:19)
- v) Vyuho vikuu humu nchini vitoe mafunzo ya tasfiri kwa wanafunzi ili waweze kuzitafsiri hata kazi watakazozipata katika taaluma mbalimbali. Na kwa kuwa Kiswahili kimefanywa kuwa lugha rasmi sawa na Katiba ya Kenya (2010), basi wanafunzi hawa baadaye wakifuzu watakuwa na kazi hasa ya kuzitafsiri matini mbalimbali katika lugha za kienyeji na kitaifa, bila matatizo.
- vi) Vitabu vilivyopendekezwa katika silibasi mpya vitafsiriwe hasa kwa wanafunzi wa darasa la chini. Hii itawawezesha kukuza na kuendeleza lugha zao za kienyeji. Hali kama hii itaokoa lugha za kienyeji zisije zikafa kutokana na kusakamwa na lugha zinazotumika shuleni, yaani Kiswahili na Kiingereza.
- vii) Kama njia mojawapo ya kukuza lugha za kienyeji, serikali ya kitaifa na za kaunti zinafaa kuunga mkono tafsiri za makala mbalimbali zinazotumiwa shuleni na hata katika ofisi za kiserikali ili wananchi wengi wajihusishe zaidi katika shughuli za ujenzi wa taifa kwa kufikiwa kwa lugha wanazozielewa vyema.

7.5 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulilenga kuchunguza uandishi upya unavyojitokeza katika tafsiri. Utafiti uliangazia maandishi matakatifu ya Biblia, ambapo ulichunguza jinsi uandishi upya ulivyobainika katika tafsiri ya Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kikalenjin. Kutokana na utafiti huu, tunaweza kutoa mapendekezo yafuatayo kuhusu tafiti za baadaye:

1. Kwa kuwa utafiti huu ulijikita katika tafsiri ya Biblia kutoka lugha ya Kiswahili hadi Kikalenjin, utafiti mwingine unaweza kufanywa unaochunguza tafsiri kutoka lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kihebrania na kadhalika, hadi lugha ya Kikalenjin au lugha nyingine ya kienyeji.
2. Utafiti mwingine unaweza kufanywa ili kubaini jinsi matumizi ya alama za uakifishaji zinavyoweza kusababisha kuwepo kwa uandishi upya wa matini tafsiri.
3. Utafiti kama huu pia unaweza kufanywa kwa kutumia matini zisizo za kidini, kama vile Katiba, ili kukadiria kiwango cha uandishi upya ikilinganishwa na ilivyo katika matini za kidini.
4. Kando na kuchunguza kitabu kimoja katika Biblia, labda utafiti mwingine unaweza kufanywa wa kuchanganua uandishi upya katika vitabu zaidi vya Biblia. Hili litatambua iwapo kitabu cha Mithali kilitafsiriwa tofauti na vitabu vingine vya Biblia, hasa kwa kuzingatia uandishi upya unavyodhihirika.
5. Aidha, utafiti unaweza kufanywa ili kuchunguza mchango wa kazi tafsiri kwa ukuaji wa maendeleo na uchumi humu nchini, na hata Afrika Mashariki.
6. Utafiti mwingine unaweza kufanyiwa katika tafsiri ya Katiba ya Kenya kuona kama uandishi upya uliathiri ujumbe asilia kwa kuwa katiba ni chombo muhimu katika utawala na utangamano wa nchi.

MAREJELEO

- Agar, M. (1994). *Language Shock: Understanding the Culture of Conversation*. Cambridge: Cambridge University press.
- Al-Hassan, A. (2013). The Importance of Culture in Translation: Should Culture be Translated? Katika *International Journal of Applied Linguistics & English Literature*. Vol 2 No.2. ISSN 2200-3452 (Online)
- Alvarez, R. R., & Vidal, M. C. A. (1996). "Translating: A Political Act". *Translation Power Subversion*. Clevedon: Multilingual Matters Ltd.
- Askoy, B. (2001). "Translation As Rewriting: The Concept and It's Implications on the Emergency of a National Literature". Katika *Translation Journal* 5(3)
- Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation*. London: Routledge.
- Bal, M (2002). *Travelling Concepts in the Humanities. A Rough Guide*. Toronto: University of Toronto Press
- Bassnett, S. (1980). *Translation Studies*. London: Routledge.
- Biamah, J. (2012). *Methods and Trends of Interpretation*. Deutschland: Lambert Academic Publishing.
- Bitugi, E. M. (2007). "Taaluma ya Tafsiri katika Vyombo vya Habari Nchini Kenya: Matatizo, Changamoto na Mustakabali wake" katika Njogu (Mhr) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Limuru. Kolbe Press.
- Bryson, S. M. (1959). *The History of the Nandi People; Light in Darkness*. England: Parry Jackman.
- Buliba, A. F. (2001). "Lugha, Utamaduni na Jamii, katika Maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa" katika Shitemi N.L na wenzake (2001). *Kiswahili A Tool for Development the Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University press.
- Catford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. New York: Oxford University Press.
- Eco, U. (2001). *Experiences in Translation*. Toronto: University of Toronto Press.
- Fawcett, P. (1997). *Translation and Language*. Manchester: St. Jerome Publishing.
- Graedler, A. L. (2010). "Cultural Shock." *Oslo Studies in English on the Net – Translation Course*. Oslo: Oslo University. Web. 19 Nov 2015
- Gromova, N. V. (2004). Tafsiri Mpya ya Fasihi ya Kirusi. *Katika Kiswahili. Swahili Forum* 2004 (11) Uk. 121-125.
- Guerra, A. F. (2012). Translating Culture: Problem Strategies and Practical. *A Journal of Literature, Culture and Literary Translation*. No. 1 Year 3
- Gumperz, C. (1971). *Language in Social Groups*. Stanford: Stanford University.

- Harvey, M. (2012). A beginner's course in Legal Translation: The case of Culture-bound Terms. Katika A.F. Guerra (2012). "Translating Culture Problems, Strategies and Practical realities". *Juzuu la Literature, Culture and Literary Translation*.
- Hatim, B., & Mason, I. (1994). *Discourse and the Translator*. New York: Longman.
- Hermans, T. (2004). *Translation in Systems: Descriptive and System Oriented Approaches Explained*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Education Press.
- Hongwei, C. (1999). *Cultural Difference and Translation*. Wuhan: Central China Normal University.
- House, J. (2009). *Translation*. Oxford: Oxford University Press.
- Inaba, I. (2001). *Is Translation a Rewriting of an Original Text?* <http://www.translaciondirectory.com/articles/article2003>.
- Inaba, T. (2009). Is Translation a Rewriting of the Original Text? *Katika Translation Journal* Vol.13:2.
- Jakobson, R. (1959). On Linguistic Aspects of Translation katika R.A Brower (Mhr) *On Translation*. Cambridge: Harvard University Press. Uk 232-239.
- Katan, D. (1999). *Translating Culture: An Introduction for Translators, Interpreters and Mediators*. Manchester: St. Jerome.
- Kelly, L. (1979). *The True Interpreter: A History of Translation Theory and Practice in the West*. Oxford: Basil Blackwell.
- Kerlinger, F. N. (1973). *Foundation of Behavioural Research*. New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Kombo, D. K., & Tromp, L. A. (2006). *Proposal and Thesis writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques*. 2nd Edition. New Delhi: Wiley Eastern Limited.
- Kramersch, C. (1998). *Language and Culture*. New York: Oxford University Press.
- Krings, H. P. (1986). "Translation Problems and Translation Strategies of Advance German Learners of French". Katika J, House na S. Blum-Kulka (Whr), *Interlingual an Intercultural Communication*. Uk 263-265. Tübingen: Gunterman.
- Larson, M. (1984). *Meaning-Based Translation. A Guide to Cross-Language Equivalence*. (2nd Ed) New York: University Press of America.
- Lefevere, A. (1992). *Translation, Rewriting and the Manipulation of Literary Fame*. London/ New York: Routledge.
- Lefevere, A. (1999). "Mother Courage's Cucumber: A Text, System and Refraction in a Theory of Literature." Katika Venuti, L. (mhr). *The Translation Studies Reader*. London: Routledge.

- Lefevere, A. (2004). *Translation, Rewriting and the Manipulation of Literary Fame*. Shanghai: Shanghai Foreign Language Education Press.
- Leppihalme, R. (1997). *Culture Bumps: An Empirical Approach to the Translation of Allusions*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Malangwa, P. S. (2010). "Handling Technical Translations: The Case of Computer Programs from English into Kiswahili." Tasnifu. Ph.D. Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mbiti, J. S. (12-5-2015). "Bible Translation into Vernacular" makala katika gazeti la *The Daily Nation*.
- McGuire, B. S. (1980). *Translation Studies*. London: Methuen.
- Mish, J. L. (1988). "The World as language." Katika Newmark. *Approaches to Translation*. Upper Saddle River: Prentice Hall.
- Morse, J. (1994). *Critical Issues in Quantitative Research Methods*. Thousand Oaks, CA: Sage.
- Mugenda, O. M., & Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods, Qualitative & Quantitative Approaches*. Nairobi: ACTS Press.
- Mukuthuria, M. (2007). Mchango wa Kiswahili katika Tazunguzi za Kitaaluma za Kiswahili katika Njogu (Mhr) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Limuru. Kolbe Press.
- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies, Theories and Application*. London na New York: Routledge.
- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitambulizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Newmark, P. (1988). *Approaches to Translation*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Nida, A. E. (1988). *Translation as Communication*. Katika Newmark. *Approaches to Translation*. Upper Saddle Rive: Prentice Hall.
- Nida, E. A (1964). *Towards a Science of Translating with Special Reference to Principles & Procedures involved in Bible Translating*. Leiden: Brill
- Nida, E. A., & De Waard. (1986). *From One Language to Another: Functional Equivalence in Bible Translating*. Nashville: Thomas Nelson Publishers.
- Nida, E. A., & Taber. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: Brill.
- Nord, C. (2007). *Translating as Purposeful Activity: Functionalists Approaches Explained*. Manchester: St.Jerome Publishers.
- Odeo, I. I., na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimu Jamii Kwa Shule Ya Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

- Oduori, R. (2008). Uchanganuzi wa Nadharia za Tafsiri: Mwelekeo wa Kiusemezano. Katika N.O Ogechi, N.L Shitemi na K.Simala (whr) 2008: *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili Na Lugha Nyingine za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Ogechi, N. O. (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.
- Ordudari, M. (2007). Translation procedure, Strategies and Methods. Katika *Translations Journal*. [URL: http://translationaljournal.net/journal/41culture.htm](http://translationaljournal.net/journal/41culture.htm) (6/12/2015).
- Orodho, J. A. (2009). *Elements of Education and Social Sciences Research Methods*. Maseno: Kanezja Publishers.
- Picken, C. (1983). *The Translators Handbook*. London: Aslib Publishing.
- Picken, C. (1989). *The Translator's Handbook*. (2nd Edition) Aslib: The Association for Information Management.
- Pym, A. (1995). *Translation as Transaction Cost*. Frankfurt: Peter Lang.
- Pym, A. (2000). *Exploring Translation Theories*. New York: Routledge.
- Republic of Kenya.(2010). *The Constitution of Kenya, 2010*. Nairobi: The Government Printer.
- Salehi, M. (2012). Reflections on Culture, Language and Translation Katika *The Journal of Academic and Applied Studies*. Juzuu.2(5). Uk 76-85.
- Sapir, E. (1949). *Culture, Language and Personality*. London: University of California Press.
- Shitemi, N. L. (1997).“Uaminifu katika Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili. Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka.” Tasnifu: Dphil. Eldoret, Moi University. (Haijachapishwa).
- Shitemi, N. L. (2001). Language as a Tool for development: Issues to Ponder. katika, Shitemi N.L na wenzake (2001) *Kiswahili A Tool for Development the Multidisciplinary Approach*. Eldoret: Moi University press.
- Shuping, R. (2013). Translation as Rewriting. Katika *International Journal of Humanities and Social Sciences*. Juzuu 3: 18 (Uk. 55-59).
- Snell-Hornby M. (1988). *Translation Studies: An Integrated Approach*. America: John Publishing Company.
- Sun, H. (2011). On Cultural Differences and Translation Methods. Katika *Jarida la Language Teaching and Research*. Juzuu 2 uk. 160-163. Finland: Academy Publishers.
- Toury, G. (1995). *Descriptive Translation Studies and Beyond*. John Benjamin Publishing.

- Traore, A.F. (2005). Translating Kiswahili Novel into 'Kizungu': Sepazione, The Italian Edition of Said Ahmed Mohamed's *Utengano*. *Swahili Forum* 12 (2005) uk. 99-107.
- TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Venuti, L. (1995). *The Transator's Invisibility: A History of translation*. New York: Routledge.
- Venuti, L.(1998). Strategies of Translation Katika M. Baker (Mhr) *Encyclopedia of Translation Studies* (Uk. 240-244).London and New York: Routledge.
- Wardaugh, R. (2004). *An Introduction to Sociolinguistics*. London: Blackwell Publishing.
- Wikipedia. (12/01/2015). en.wikipedia.org/wiki/Johann-Ludwig-Krapf.
- Wolfgang, L. (1991). *Translation Performance, Translation Process and Translation Strategies. A Psycholinguistic Investigation*. Tübingen: Narr Print.
- Zakhir, M. (2010). *The History of Translation*. Moulay: University of Soultan Moulay Slimane.

MATINI TEULE

United Bible Societies (1969). *Bukuit Ne Tilil*. Nairobi: The Bible Society of Kenya.

United Bible Society (1957). *Biblia Takatifu*. Nairobi: The Bible Society of Kenya.

VIAMBATISHO

Kiambatisho I: Data Iliyochanganuliwa Kutoka Kitabu Cha Mithali

- Mithali 1:1 **M.A** Mithali ya Suleimani, mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli.
M.P *Kalawenaikab Solomon weritab Daudi, laitoriatat Israel:*
- Mithali 1:10 **M.A** Mwanangu, wenye dhambi wakikushawishi,
Wewe usikubali.
M.P Werinnyu, ngogaigain kiptengeginik,
Ko mecham.
- Mithali 1:15 **M.A** Mwanangu, usiende njiani pamoja nao;
Uzuie mguu wako usiende katika mapito yao.
M.P *Werinnyu, amobe oret agenge koboto ichek;
Iste keldang'ung' eng' orenywa:*
- Mithali 1:17 **M.A** Kwa kuwa mtego hutegwa bure,
Mbele ya macho ya ndege yeyote.
M.P *Kigiriich mestet buch,
Kogeer ei taritiet age tugul:*
- Mithali 1:20 **M.A** Hekima hupaza sauti yake katika njia kuu,
Hutoa sauti yake katika viwanja;
M.P *Waachei mising' ng'omnatet eng' oret;
Ng'alali eng' komoswek che baroen;*
- Mithali 2:16 **M.A** Ili kuokoka na malaya,
Naam, na malaya mwenye kubembeleza kwa maneno.
M.P *Si kosoruen eng' chepkugoniot'
Ee, kwondo ne chemwai kut;*
- Mithali 3:9 **M.A** Mheshimu BWANA kwa mali yako,
Na kwa malimbuko ya mazao yako yote.
M.P *Konyite Jehovah tuguguk, Ak eng' tongoanikab rurateng'ung
tugul.*
- Mithali 4:2 **M.A** Kwa kuwa nawapa mafundisho mazuri; Msiiache sheria yangu.
M.P *Amu agonok konetisiet ne mie; Amobagakte ng'atutiennyu.*
- Mithali 5:1 **M.A** Mwanangu, sikiliza hekima yangu;
Tega sikio lako, mzisikie akili zangu;
M.P *Werinnyu, kas ng'omnatennyu;
Epchi it naennyu:*
- Mithali 5:3 **M.A** Maana midomo ya malaya hodondoza asali,
Na kinywa chake ni laini kuliko mafuta;
M.P *Amu saune kumnyat kutiab chepkugoniot,
Ak tangusen ng'alekyik kosiir mwaita:*

- Mithali 5:5 **M.A** Miguu yake italelemkia mauti
Hatua zake zinashikamana na kuzimu.
M.P *Chorjingei kelyekyik meet;*
Namegei kakwautikyik ak oldab che kigobek.
- Mithali 5:15 **M.A** Unywe maji ya birika lako mwenyewe,
Na maji yenye kububujika katika kisima chako.
M.P *Ee beek che mi tereng'ung',*
Ak iee beek che rootei eng' keringeng'ung'.
- Mithali 5:31 **M.A** Lakini akipatikana, atalipa mara saba;
Atatoa mali yote ya nyumba yake.
M.P *Ago ngot kenyor , kogeeri konyil tisab;*
Igoitoi tuguk tugul che bo gonnyi.
- Mithali 6:1 **M.A** Mwanangu, kama umekuwa mdhamini wa rafiki yako,
Ikiwa wewe na rafiki mme pana mikono,
M.P *Werinnyu, ngot iegu ne itononjini chitab kokweng'ung'*
Ngot ko kooyosie onamge eunek ak kipsagarin,
- Mithali 6:4 **M.A** Usiache macho yako kupata usingizi,
Wala kope za macho yako kupata usinzia.
M.P *Ameru, Anan inuuch.*
- Mithali 6:14 **M.A** Mna upotofu moyoni mwake, hutunga uovu daima,
Hupanda mbegu za magomvi.
M.P *Mi mastael muguleldannyi, chobei yaitiet ko tugul;*
Kolei toiyet.
- Mithali 6:23 **M.A** Maana maagizo hayo ni taa, na sheria hiyo ni nuru,
Na maonya ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima.
M.P *Amu kayamisutiet ko tait; ak e ko lapkeiyet;*
Ak keretab kong' ne bo kotigonet ko oretab sobondo:
- Mithali 6:25 **M.A** Usiutamani uzuri wake moyoni mwako;
Wala usikubali akunase kwa kope za macho yake.
M.P *Amegase miat eng' muguleldang'ung' kororonindannyi;*
Amengoriigenen konyekyik.
- Mithali 6:26 **M.A** Maana kwa malaya mtu hutiwa katika hali
ya kuhitaji kipande cha mkate;
M.P *Amu ibeeti chepkugoniot chito agoi kong'etyi kereruti:*
Ak cheng'oti chepkugoniot koriich sobondo ne kararan.
- Mithali 6:28 **M.A** Je! Mtu aweza kukanyaga makaa ya moto,
Na nyayo zake zisiungue?
M.P *Imuch chi kotiegat ng'etietot,*
Ama lalyo kelyekyik?

- Mithali 7:3 **M.A** Zifunge katika vidole vyako;
Ziandike juu ya kibao cha moyo wako.
M.P *Ratyi moriguk; Sirji muguleldang'ung'*
- Mithali 7:6 **M.A** Maana katika dirisha la nyumba yangu
Nalichungulia katika shubaka yake.
M.P *Amu kiaiitite eng' tirisietab gonny
Eng' tirsiennyu ne bo segengeisiek*
- Mithali 7:7 **M.A** Nikaona katikati ya wajinga;
Nikamtambua miongoni mwa vijana, Kijana mmoja siyekuwa
na akili,
M.P *Ak kiager eng' kwenutab che abusanik, Ak kianyit eng' kwenutab
Neranik, neran ne matinyei naet.*
- Mithali 7:11 **M.A** Ana kelele na ukaidi:
Miguu yake haikai nyumbani mwake.
M.P *Bolin ago ngelelio; Matononi eng' gonnyi:*
- Mithali 7:12 **M.A** Mara yu katika njia kuu, mara viwanjani,
Naye huotea kwenye pembe za kila njia.
M.P *Mi oret ra, komi tun komoswek che baraen,
Ak soptai eng' ole besiechin ortinwek.*
- Mithali 7:19 **M.A** Maana mume wangu hayumo nyumbani,
Amekwenda safari ya mbali,
M.P *Amu mami ga chitab kobo got,
Kawa banda ne loo:*
- Mithali 7:22 **M.A** Huyo akafuatana naye mara hiyo,
Kama vile ng'ombe aendavyo machinjoni;
Au mpumbavu kuadhibiwa katika pingu;
M.P *Isubi anyun inendet kwonyotok eng' yoto,
Ko u eito ne kikwerie kwo eng'set,
Anan kou mugurek che kitigone ne berber*
- Mithali 8:19 **M.A** Matunda yangu hupita dhahabu, naam dhahabu safi,
Na faida yangu hupita fedha iliyo teule.
M.P *Kororon logoekyuk kosiir tahabu, ee, tahabu che tililen;
Ak siirei kelunetab tugukyuk feda che kororon.*
- Mithali 8:25 **M.A** Kabla milima haijawekwa imara,
Kabla ya vilima nalizaliwa.
M.P *Ye kitomo kelumnda tulongok,
Kigisicha ye kitomo kobiit tulongok che mengechen;*
- Mithali 8:32 **M.A** Basi, wanangu, nisikilizeni sasa;
Maana heri hao wazishikao amri zangu.
M.P *Ogas anyun, werju:
Amu iberurotin ichek che ribei ortinwekyuk.*

- Mithali 9:2 **M.A** Amechinja nyama zake,
Umechanganya divai yake,
Ameiandalia meza yake pia.
M.P *kigoeny tukyik; kigoburuch divaikyik;
Kigochob amitwogik eng' mesennyi.*
- Mithali 9:3 **M.A** Amewatuma wajakazi wake, analia,
Mahali pa mjini palipoinuka sana,
M.P *Kigoyokto tibikyik, waachei eng komoswek che tororen mising
Che bo nganaset,*
- Mithali 9:5 **M.A** Njoo ule mkate wangu,
Ukanywe divai niliyoichanganya.
M.P *Nyo, am amitwogikyuk'
Ak iee divaik che kaaburuch.*
- Mithali 9:12 **M.A** Kama una hekima, una hekima kwa nafsi yako;
Na kama una dharau, Utaichukua peke yako.
M.P *Ngot ko i ng'om, ko i ng'om ne neng'ung:
Ak ngot ichotisie i geseni inyege.*
- Mithali 9:17 **M.A** Maji yaliyoibiwa ni matamu,
Na mkate ulioliwa kwa siri ni hupendeza.
M.P *Anyiny beek che kechorei,
Ak kororon amitwogik che keamei eng' ung'ot.*
- Mithali 10:1 **M.A** Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye;
Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye.
M.P *Iboiboi werit ne ng'om kwanda:
Ago inyalili werit ne berber kamet.*
- Mithali 10:6 **M.A** Baraka humkalia mwenye haki kichwani;
Bali jeuri hufunika kinywa chake mtu mwovu.
M.P *Tebe kaberoik ne bo iman:
Ago tuche koromnatet kutitab kiptengekyot.*
- Mithali 10:10 **M.A** Akonyezaye kwa jicho huleta masikitiko;
Bali mpumbavu mwenye maneno mengi ataanguka.
M.P *Ibu arogenet ne ng'wegisie konda:
Ago ibuti ne berber ne chang' ng'alek.*
- Mithali 10:15 **M.A** Mali ya tajiri ni mji wake wa nguvu;
Uangamivu wa maskini ni umaskini wao.
M.P *Magornatetab mogoriot ko nganasennyi ne kim:
Ng'emisietab kibananok ko banandanywa.*
- Mithali 11:2 **M.A** Kijapo kiburi ndipo ijapo aibu;
Bali hekima hukaa na wanyenyekavu.
M.P *Ye nyo menotet, konyo agine kalilinet:
Ago mi ng'omnatet ak che iming'inegei.*

- Mithali 11:3 **M.A** Ukamilifu wao wenye haki utawaongoza
Bali uakidi wao wenye fitina utawaangamiza.
M.P *Indochin che bo iman kagesunatenywa bo ge:
Ago ng'emei che yaei kabersiet, kamaasenywa.*
- Mithali 12:3 **M.A** Mtu hatathibitika kwa njia ya uovu;
Shina la mwenye haki halitaondolewa kamwe.
M.P *Magimitu chi eng' yaitio: Amagoi kitut tigitotab che bo iman.*
- Mithali 12:4 **M.A** Mwanamke mwema ni taji ya mumewe;
Bali aaibishaye ni kama kuoza mishipani mwake.
M.P *Egu kwondo ne ng'om konditab manong'otiondennyi:
Ago kwondo ne ibu kalilinet ko u nunatet eng' kowekab
chichoto.*
- Mithali 12:1 **M.A** Kila apendaye mafundisho hupenda maarifa;
Bali yeye achukiaye kulaumiwa ni kama mnyama.
M.P *Age tugul ne chamei kotigonet kochamei naet:
Ago inendet ne esioi keretab kong' ko u tiondo.*
- Mithali 13:1 **M.A** Mwana mwenye hekima husikiliza mausia ya babaye;
Bali mwenye dharau hasikilizi maonyo.
M.P *Epchin it werit ne ng'om kotigonetab kwandanyi:
Ago magasei keretab kong' chotindet.*
- Mithali 13:4 **M.A** Nafsi ya mvivu hutamani asipate kitu;
Bali nafsi ya mwenye bidii itanenepeshwa.
M.P *Tinyei maget sobondab ne choriren, ak manyoru kiy:
Ago nereu sobondab ne igiilegei.*
- Mithali 13: 9 **M.A** Nuru ya mwenye haki hung'aa sana;
Bali taa ya mtu mbaya itazimika.
M.P *Iluu mising' lapkeiyetab che bo iman:
Ago kimisi taitab kiptengeginik.*
- Mithali 13:24 **M.A** Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe;
Bali yeye ampendaye humrudi mapema.
M.P *Wechei werinnyi ne mabirei:
Ago inendet ne chamei werinnyi kotigoni ko u ye nyolu.*
- Mithali 14:5 **M.A** Shahidi mwaminifu hatasema uongo;
Bali shahidi wa uongo, pumzi zake ni uongo.
M.P *Mamwaei lembech baoriat ne kiyani:
Ago mwaei lembech baoriat ne ma bo iman.*
- Mithali 14:11 **M.A** Nyumba ya mtu mbaya itabomolewa;
Bali hema ya wenye haki itafanikiwa.
M.P *Kigabui gotab kiptengeginik:
Ago kiberuri emaitab ne bo iman.*

- Mithali 14:24 **M.A** Taji wa wenye hekima ni mali zao;
Bali upumbavu wa wajinga ni upumbavu tu.
M.P *Chepkuletab che ng'omen ko magornatosiekwak:
Ago berberindab che berber ko berberindo kityo.*
- Mithali 15: 10 **M.A** Adhabu kali ina yeye aiachaye njia;
Naye achukiaye kukemewa atakufa.
M.P *Mi kotigonet ne ng'wan eng' inendet ne metoi oret:
Ak meei inendet ne wechei keretab kong'.*
- Mithali 15:17 **M.A** Chakula cha mboga penye mapendano,
Ni bora kuliko ng'ombe aliyenona pamoja na kuchukiana.
M.P *Kaigai keam ngwek eng' ole mi chamnyet,
Kosiir eito ne akwai koboto wechet.*
- Mithali 15:20 **M.A** Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye;
Bali mpumbavu humdharau mamaye.
M.P *Iboibo kwanda werit ne ng'om:
Ago sasei kamet chito ne berber.*
- Mithali 16:5 **M.A** Kila mwenye moyo wa kiburi ni chukizo kwa BWANA;
Hakika, hatakosa adhabu.
M.P *Kit ne wechei jehovah ko muguleldo age tugul ne menei:
Agot ngo namgei eunek, ko magimeto ama kibir.*
- Mithali 16: 8 **M.A** Afadhali mali kidogo pamoja na haki,
kuliko mapato mengi pamoja na udhalimu.
M.P *Kaigai tuguk che matia koboto imanda.
Kosiir kehunaikche chang' koboto kertaetab kong'.*
- Mithali 16:10 **M.A** Kukata maneno huwa kwenye midomo ya mfalme;
Kinywa chake hakitakosa katika hukumu.
M.P *Bunu kutitab laitoriat tiletab kiruoget ne bo Kamuktaindet:
Malelei kutinnyi eng' kiruoget.*
- Mithali 16:20 **M.A** Atakayelitafakari neno atapata mema:
Na kila amwaminiye BWANA ana heri.
M.P *Nyoru mieindo ne epchin it ng'olyot:
Ak baibai age tugul ne imang'u Jehovah.*
- Mithali 16:27 **M.A** Mtu asiyefaa kitu huchimba shimo la madhara;
Katika midomo yake mna moto huteketezao.
M.P *Chobei yaitiet chito ne matilei kiy:
Ak mitei kutinnyi kit ne u mat ne beelsei.*
- Mithali 17:3 **M.A** Kalibuni kwa fedha, na tanuru kwa dhahabu;
Bali BWANA huijaribu mioyo.
M.P *Bo teret feda che kitilili, ak bo mat ne o tahabu:
Ago Jehovah ne tiemei muguelwek.*

- Mithali 17:8 **M.A** Kipawa ni kama kito cha thamani machoni pake yeye aliye nacho;
Kila kigeukapo hufanikiwa.
M.P *U koita nebo kamanutiet ne o,
Kitab kagaigaet, eng'taitab inendet ne tinyei:
Borei eng' ui tugul ole tokyingei.*
- Mithali 17:20 **M.A** Mtu mwenye moyo wa ukaidi hatapata mema;
Na mwenye ulimi wa upotofu huanguka katika misiba.
M.P *Manyoru kiy ne mie inendet ne imaasat muguleldo:
Ak ibutyin yaitiet ne tinyei ngelyepta ne imaasat.*
- Mithali 18:2 **M.A** Mpumbavu hapendezwi na ufahamu;
Ila moyo wake udhihirike tu.
M.P *Maboiboitune ne berber kaguiyet,
Ago ibortogei kityo muguleldonyi.*
- Mithali 18:22 **M.A** Apataye mke apata kitu chema;
Naye ajipatia kibali kwa BWANA.
M.P *Nyuru kit ne mie age tugul ne nyuru osotiot ne ituni,
Ak nyuru chamet eng' taitab Jehovah.*
- Mithali 19: 6 **M.A** Watu wengi watamsihi mkuu ili awafadhili
Na kila mtu ni rafiki yake atoaye tunu.
M.P *Rirjin bik che chang' mieindat chito ne toogunot:
Ak chi age tugul ko choruetab inendet ne igoitoi konunoik.*
- Mithali 19:13 **M.A** Mwana mpumbavu ni msiba kwa babaye;
Na ugomvi wa mke kama kutona-tona daima.
M.P *Nyalildab kwandanyi werit ne berber:
U beek che saitoi bolatetab osotiot.*
- Mithali 19:24 **M.A** Mtu mvivu hutia mkono wake sahanini;
Ila hataki hata kuupeleka kinywani pake.
M.P *Unyei eunnyi eng' tabet chito ne choriren,
Ama chamei konde kutinnyi kogeny.*
- Mithali 19:29 **M.A** Hukumu zimewekwa tayari kwa wenye mzaha;
Na mapigo kwa mgongo wa wapumbavu.
M.P *Kipchopchin kiruogutik chotik,
Ak kichopchin bataikab che bereber birutik.*
- Mithali 20:17 **M.A** Chakula cha uongo ni kitamu kwa mtu;
Lakini halafu kinywa chake kitajaa changarawe.
M.P *Anyiny eng' chi amitwogikab lembeita;
Ago ne matia konyi kutinnyi koik.*
- Mithali 20:20 **M.A** Amlaaniye babaye au mamaye'
Taa yake itazimika katika giza kuu.
M.P *Kimisi eng' mesundeito ne o mising'
Taitab age tugul ne sasei kwandanyi anan kamet.*

- Mithali 21:27 **M.A** Sadaka ya wasio haki ni chukizo;
Si zaidi sana ailetapo mwenye nia mbaya!
M.P *Kit ne kiwechei korosiotab kiptengeginik:
Kotam nee anyun ye ibu korosiondonoto,
Kotinyei kabwatutik che yaach?*
- Mithali 22:14 **M.A** Kinywa cha malaya ni shimo refu;
Anayechukiwa na BWANA atatumbukia ndani yake.
M.P *Keringet ne loo kutitab chepkugoniot:
Ibutyin yoto inendet ne nerekyin Jehovah.*
- Mithali 22:27 **M.A** Kama huna kitu cha kulipa;
Kwani ukaondolee kitanda chako chini yako.
M.P *Ngot ko metinye che iyaaktoe, ko amu nee anyun si koibenen
Itogung'?*
- Mithali 23:6 **M.A** Usile mkate wa mtu mwenye husuda;
Wala usivitamani vyakula vyake vya anasa;
M.P *Ameam amitwogikab inendet ne tinyei kong' ne ya,
Amemach amitwogikyik che anyiny:*
- Mithali 23:15 **M.A** Mwanangu, kama moyo wako una hekima,
Moyo wangu utafurahi, naam moyo wangu;
M.P *Werinnyu, ngo ng'om muguleldang'ung''
Kobaibai muguleldanyu, ee, baibai muguleldanyu:*
- Mithali 23:16 **M.A** Naam,viuno vyangu vitafurahi, midomo yako inenapo maneno
mema.
M.P *Ee, boiboitu muguleldanyu, ye kemwa tuguk che bo iman.*
- Mithali 24:11 **M.A** Uwaokoe wanaochukuliwaili wauawe;
Nao walio tayari kuchinjwa uwaopoe.
M.P *Soru ichek che kimuti koba meet'
Ak iet che kimachei kebar.*
- Mithali 24:13 **M.A** Mwanangu, ule asali, kwa maana ni njema,
Na sega la asali lililo tamu ulionjapo.
M.P *Werinnyu, am kumik, amu miach;
Koboto masamek, amu anyiny ye ichamjami:*
- Mithali 24:30 **M.A** Nalipita karibu nsa shamba la mvivu,
Na shamba la mzabibu la mtu asiye na akili.
M.P *Kiabun mbaretab chito ne choriren,
Ak ole negite mbaretab sabibuk ne bo chichoto matinyei naet;*
- Mithali 25:4 **M.A** Ondoa takataka katika fedha,
Na chombo kitatokea kwa mtakasaji;
M.P *Kenende michikyigek eng' feda,
Si kigimit eng' imanda ng'eoberennyi ne bo laitornatet.*

- Mithali 25:13 **M.A** Kama baridi ya theluji wakati wa mavuno;
Ndivyo alivyo mjumbe wa mwaminifu kwao wantumao;
Kwa maana huwaburudisha bwana zake nafsi zao.
M.P *U kaititietab teluchi eng' betusiekab kesisiet,
Chito ne kiyoktoi ne kiyani, eng' ichek iyoktoi inendet;
Amu igoigoi sobonwekab kiptainikyik.*
- Mithali 24:24 **M.A** Amwambiaye mtu mvivu, wewe una haki;
Kabila za watu watamlaani, taifa watamchukia.
M.P *Inendet ne mwachin kiptengekyot, kolenjin, i bo iman;
Kochubei bik inendet, wechei bororiosiok inendet.*
- Mithali 25:21 **M.A** Adui wako akiwa ana njaa, mpe chakula;
Tena akiwa ana kiu, mpe maji ya kunywa.;
M.P *Ngo am rubet bunyondeng'ung', ibai;
Ak ngo am melel, inage koe:*
- Mithali 25:28 **M.A** Asiyetawala roho yake ni mfano wa mji uliobomolewa, usio na kuta.
M.P *U nganaset ne kigebut ama tinyei irimet, chito ne maribegei.*
- Mithali 26:1 **M.A** Kama theluji wakati wa joto, na mvua wakati wa mavuno;
Kadhalika heshima haimpasi mpumbavu.
M.P *Ko u ye manamegei teluchi ak kemeut, ak manamegei ropta ak
Betutab kesisiet,
Ko u noto, manyoljin teegisto chi ne berber.*
- Mithali 26:3 **M.A** Mjeledi kwa farasi, lijamu kwa punda,
Na fimbo kwa mgongo wa mpumbavu.
M.P *Ko u ye bo kipcharitit mbartanyit, ak ko u ye bo karnetab kutit
sigiriet, Ko u noto, bo kirokto chito ne berber.*
- Mithali 26:10 **M.A** Fundi stadi hufanyiza vitu vyote;
Bali amwajiriye mpumbavu ni kama waaajiriye watu wapitao.
M.P *U mwoginet ne iguoteni tugul;
Inendet ne sirei ne berber anan che siirtoi, koboisiechi.*
- Mithali 26:14 **M.A** Kama vile mlango ugeukavyo kwenye bawaba zake,
Kadhalika mtu mvivu katika kitanda chake.
M.P *Ko u ye weegegei kereiywotab kurget karikyik che namei,
Ko u noto weechegei chito ne choriren eng, itogunnyi.*
- Mithali 27:2 **M.A** Mwingine akusifu wala si kinywa chako mwenyewe;
Mtu mgeni wala si midomo yako wewe.
M.P *Ingolosun age, amelosuge;
Ingolosun toondet, amelosuge.*

- Mithali 27:4 **M.A** Ghadhabu ni kali, hasira ni gharika:
Lakini ni nani awezaye kusimama mbele ya wivu.
M.P *Korom nereknatet, koromen mising' neregek;*
Ago ng'o ne imuchi kotonon eng' taitab ng'etkonda?
- Mithali 27:11 **M.A** Mwanangu, uwe na hekima na kunifurahisha moyo wangu;
Ili nipate kumjibu anilaumuye.
M.P *Werinnyu, ng'omitu, ak ibaibai muguleldanyu,*
Si amuch awolji inendet ne itewera.
- Mithali 27:22 **M.A** Hata ukimtwanga mpumbavu Kwa mchi kinuni pamoja na ngano,
Upumbavu wake hautamtoka.
M.P *Agot ngitui chito ne berber eng' kenut koboto bek che kagitartaran,*
Ko maistoigei berberindanyi kora.
- Mithali 27:27 **M.A** Tena yatakuwapo maziwa ya mbuzi,
Ya kukutosha kwa chakula chako'
Na chakula cha watu wa nyumbani mwako,
Na posho la vijakazi vyako.
M.P *Ak mitei chegab ng'ororek che yamei koek amitwogiguk,*
Ak che bo bikab gong'ung;
Ak amitwogik che yamei tibiguk.
- Mithali 28:7 **M.A** Yeye aishikaye sheria ni mwana mwenye hekima;
Bali aliye rafiki wa walafi humwaibisha babaye.
M.P *Werit ne ng'om age tugul neribei ng'atutik:*
Ago iteweri kwandanyi inendet ne choruetab kipkeinik.
- Mithali 28:15 **M.A** Kama simba angurumaye na dubu mwenye njaa;
Ndivyo alivyo mtu mbaya awatawalaye maskini.
M.P *U ng'etundo ne boriseni ak tiondo ne u keerit ne ombenoti,*
Bounindet ne ya ne bou kibananok.
- Mithali 28:21 **M.A** Kupendelea watu si kwema;
Wala mtu kuasi kwa ajili ya kipande cha mkate.
M.P *Ma mie ketiytii bik:*
Anan kobistoe chi kole si konyor kererutiet.
- Mithali 28:23 **M.A** Amkemeaye mwenzake hatimaye atapata kibali;
Zaidi ya mtu ajipendekezaye kwa ulimi wake.
M.P *Tun nyoru chamet inendet ne kere kong' chi*
Kosiir inendet ne chemwai kut
- Mithali 29:3 **M.A** Apendaye hekima humfurahisha babaye;
Bali ashikamaye na makahaba hutapanya mali.
M.P *Ibaibai kwanda age tugul ne chamei ng'omnatet:*
Ago iseerseeri tuguk inendet ne namegei ak chepkugonik.

- Mithali 29:14 **M.A** Mfalme awahukumuye maskini kwa uaminifu;
Kiti chake cha enzi kitathibitika milele.
M.P *Kigimiti agoi koigeny laitornatetab laitoriat
Ne iruokyin kibananok eng' imanda.*
- Mithali 29:17 **M.A** Mrudi mwanao naye atakustarehesha;
Naam, atakufurahisha nafsi yako.
M.P *Itigon wering'ung', si kogonin kamuung'et;
Ee, si kobaibai sobondang'ung'.*
- Mithali 30:1 **M.A** Maneno ya Aguri bin Yake;
Mausia ya mtu huyu aliyomwambia Ithieli, naam, Ithieli na
Ukali.
M.P *Ng'alekab Agur weritab Jake; maoinatet.
Kilenji chito Itiel, ee Itiel ak Ukal.*
- Mithali 30:7 **M.A** Mambo haya mawili nimekuomba;
Usininyime [matatu] kabla sijafa.
M.P *Kasomin tuguk aeng'; Amat ietena kotom amee:*
- Mithali 30:9 **M.A** Nisije nikakusahau, Nikasema, BWANA ni nani?
Wala nisiwe maskini sana nikaiba,
Na kulitaja bure jina la Mungu wangu.
M.P *Si mabiye ak aesien, ak ale, Ng'o jehovah?
Anan si maegu kibanania, ak achorse,
Si mamwa kainetab Kamuktaindennyu eng' tangoi.*
- Mithali 30:23 **M.A** Mwanamke mwenye kuchukiza aolewapo;
Na mjakazi aliye mrithi wa bibi yake.
M.P *Ak kwondo ne kiwechei ye kagitun
Ak chepto ne otwogindetne tun bunjin tugukab kwondo ne bou
inendet.*
- Mithali 31:1 **M.A** Maneno ya mfalme Lemueli;
Mausia aliyofundishwa na mama yake.
M.P *Ng'alekab laitoriat Lemuel;
Maonatet ne kiinet kamet.*
- Mithali 31:4 **M.A** Ee Lemueli, kunywa mvinyo hakuwafai wafalme, hakuwafai
wafalme,
Wala haifai wakuu waseme, ki wapi kileo?
M.P *Manyoljin laitorinik, ee Lemuel, manyoljin divaik;
Manyoljin bounik kole, Mi ano maiyek?*
- Mithali 31:6 **M.A** Mpe kileo yeye aliye karibu na kupotea;
Kampe divai yeye aliye na uchungu nafsini.
M.P *Inage maiyek inendet ne machei kolus,
Ak divaik icheget bik che tinyei ng'wanindo eng'sobonwekwak:*

- Mithali 31:8 **M.A** Fumbua kinywa chako kwa ajili yake aliye bubu;
Uwatetee watu wote waliochwa peke yao.
M.P *Ng'alal agobo ne namat kut,*
Agobo tugul che kagilakta kotebi ichegei.
- Mithali 31:13 **M.A** Hutafuta sufu na kitani;
Hufanya kazi ya mikono kwa moyo.
M.P *Cheng'ei osotiondonoto kororikab kechirek ak katanit,*
Boisei eng' chamnyet .
- Mithali 31:15 **M.A** Tena huamka, kabla haujaisha usiku;
Huwapa watu wa nyumbani mwake chakula;
Na wajakazi wake sehemu zao.
M.P *Ng'eetei kogeny kota ko kemoi, ak kobai bikab gonnyi.*
Ak kogocho tibikyik boisienywa.
- Mithali 31:16 **M.A** Huangalia shamba, akalinunua;
Kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu.
M.P *Ibwati agobo mbaret, ak koal:*
Minei Mbaretab sabibuk eng' keljinet ne konyor.
- Mithali 31:21 **M.A** Hawahofii theluji watu wa nyumbani mwake;
Maana wote wa nyumbani mwake huvikwa nguo nyekundu.
M.P *Maiywei kole tos nyor bikyik kaititietab teluchi;*
Amu ilaachi bik tugul che bo gonnyi ngoroik che biriren.
- Mithali 31:27 **M.A** Huangalia sana njia za watu wa nyumbani mwake;
Wala hali chakula cha uvivu.
M.P *Ribei komie atebosiekab bikab gonnyi,*
Ama amei che bo chorirnatet.

Kiambatisho II: Barua Kutoka Kwa Ofisi Ya Utafsiri Wa Biblia Ya Kapsabet



CHRISTIAN LITERATURE DEPARTMENT



Kalenjin Translations office P.O Box 20-30300 Kapsabet Tel: 020202399492

Founded in 1895

15th December 2015,


RE: KALENJIN BIBLE TRANSLATION

The Kalenjin Bible translation was carried out from 1953 up to 1969 when it was finally printed. This work was carried out by: The late Miss Frances Mumfort, the late Bishop Rev. Ezekiel Birech and Miss A.R Day.

The Kalenjin Union Version is a Kalenjin Bible that was done with the purpose of reaching the whole Kalenjin Community with the word of God. Kalenjin people are 7 groups of dialects i.e. Marakwet, Keiyo, Sabaot, Tugen, Kipsigis, Nandi and Terik. Hence the Bible was written in the Kalenjin language that is easily understood largely by the dialects.

During the translation process, the languages that were largely used to translate were from Hebrew, English, Greek and Kiswahili. Hence the use of Hebrew, Greek, Old English Bible and the Kiswahili Bible. These four languages were used to assist the translators in getting precise meanings for words. This brought the whole success to translation of Kalenjin Union Version.

Yours faithfully in His Service


Pastor William K. Koskey
Director

Blessed is he who reads the words of this prophecy...Rev.1:3

Kiambatisho III: Maswali ya Usaili

1. Je, Biblia imetafsiriwa kwa lugha za kienyeji ngapi nchini Kenya?
2. Je, ni kwa nini Biblia Takatifu ikatafsiriwa kwa lugha ya Kikalenjin na wala si katika lahaja za Kikalenjin?
3. Ni nani watafsiri wa *Bukuit Ne Tilil*?
4. Je, *Bukuit Ne Tilil* ilitafsiriwa kutoka lugha gani?
5. *Bukuit Ne Tilil* ilitafsiriwa mwaka gani?
6. Eleza baadhi ya changamoto zinazowapata watafsiri wa Biblia katika lugha ya kienyeji kama vile lugha ya Kikalenjin.